ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

	MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	**SPIKA**
1.	Mhe.Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2.	Mhe. Riziki Pembe Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake
3.	Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4.	Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5.	Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
6.	Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
7.	Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	Uteuzi wa Rais
8.	Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
9.	Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
10.	Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
11.	Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
12.	Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
13.	Mhe. Amina Salum Ali	-	Uteuzi wa Rais
14.	Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
15.	Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
16.	Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
17.	Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Nafasi za Wanawake
18.	Mhe. Haji Omar Kheri	-	Jimbo la Tumbatu
19.	Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi

20.	Mhe.	Hamad Rashid Mohamed	-	Uteuzi wa Rais
21.	Mhe.	Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
22.	Mhe.	Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
23.	Mhe.	Haroun Ali Suleiman	-	Jimbo la Makunduchi
24.	Mhe.	Harusi Said Suleiman	-	Jimbo la Wete
25.	Mhe.	Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
26.	Mhe.	Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
27.	Mhe.	Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
28.	Mhe.	Issa Haji Ussi (Gavu)	-	Jimbo la Chwaka
29.	Mhe.	Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
30.	Mhe.	Juma Ali Khatib	-	Uteuzi wa Rais
31.	Mhe.	Juma Makungu Juma	-	Jimbo la Kijini
32.	Mhe.	Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
33.	Mhe.	Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	Jimbo la Donge
34.	Mhe.	Khamis Juma Mwalim	-	Jimbo la Pangawe
35.	Mhe.	Lulu Msham Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
36.	Mhe.	Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
37.	Mhe.	Mahmoud Thabit Kombo	-	Jimbo la Kiembesamaki
38.	Mhe.	Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
39.	Mhe.	Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
40.	Mhe.	Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
41.	Mhe.	Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
42.	Mhe.	Maudline Cyrus Castico	-	Uteuzi wa Rais

43.	Mhe.	Mihayo Juma N'hunga	-	Jimbo la Mwera
44.	Mhe.	Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
45.	Mhe.	Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Jimbo la Mkoani
46.	Mhe.	Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
47.	Mhe.	Mohammed Aboud Mohammed	-	Uteuzi wa Rais
48.	Mhe.	Mohamed Ahmada Salum	-	Jimbo la Malindi
49.	Mhe.	Mohammed Said Mohammed	-	Jimbo la Mpendae
50.	Mhe.	Mohammedraza Hassanaali Mohamedali	-	Jimbo la Uzini
51.	Mhe.	Mtumwa Peya Yussuf	-	Jimbo la Bumbwini
52.	Mhe.	Mtumwa Suleiman Makame	-	Nafasi za Wanawake
53.	Mhe.	Mussa Ali Mussa	-	Jimbo la Ole
54.	Mhe.	Mussa Foum Mussa	-	Jimbo la Kiwani
55.	Mhe.	Mwanaasha Khamis Juma	-	Jimbo la Chukwani
56.	Mhe.	Mwanaidi Kassim Mussa	-	Nafasi za Wanawake
57.	Mhe.	Mwantatu Mbaraka Khamis	-	Nafasi za Wanawake
58.	Mhe.	Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini	-	Jimbo la Dimani
59.	Mhe.	Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy	-	Jimbo la Chaani
60.	Mhe.	Nassor Salim Ali	-	Jimbo la Kikwajuni
61.	Mhe.	Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde
62.	Mhe.	Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
63.	Mhe.	Rashid Ali Juma	-	Jimbo la Amani
64.	Mhe.	Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
65.	Mhe.	Saada Ramadhan Mwenda	-	Nafasi za Wanawake

66.	Mhe.	Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
67.	Mhe.	Salama Aboud Talib	-	Nafasi za Wanawake
68.	Mhe.	Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
69.	Mhe.	Said Soud Said	-	Uteuzi wa Rais
70.	Mhe.	Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71.	Mhe.	Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72.	Mhe.	Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73.	Mhe.	Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74.	Mhe.	Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75.	Mhe.	Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76.	Mhe.	Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77.	Mhe.	Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78.	Mhe.	Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79.	Mhe.	Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80.	Mhe.	Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81.	Mhe.	Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82.	Mhe.	Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83.	Mhe.	Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84.	Mhe.	Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake
	Dkt.	Yahya Khamis Hamad	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tano – Tarehe 06 Aprili, 2016

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

KIAPO CHA UAMINIFU

(Wajumbe wafuatao waliapishwa Kiapo cha Uaminifu na baada ya kumaliza walikaa katika sehemu zao).

1. Mhe. Ali Abeid Karume
2. Mhe. Amina Salum Ali
3. Mhe. Hamad Rashid Mohammed
4. Mhe. Juma Ali Khatib
5. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed
6. Mhe. Modlen Siras Castico

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tumemaliza shughuli za kiapo ingawa kuna mjumbe mmoja ambaye alitakiwa aape lakini hakuweza kufika na tutafanya utaratibu ili baadae aweze kupata nafasi yake ya kuapa.

Waheshimiwa Wajumbe, jana pamoja na leo nimefanya mawasiliano na serikali kuhusiana na hii hali ambayo tunayo kuhusu uchangiaji wa hotuba ya Mhe. Rais na tumefikia pahali ambapo sasa napenda nichukue nafasi hii nimwite Mhe. Hamza Hassan Juma ili aweze kutoa hoja.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru sana lakini pia naishukuru serikali kwa kuweza kuizingatia hoja yangu na sasa hivi naomba baraka zote kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili kutumia Kanuni ya 156 kutenga Kanuni kando, Kanuni ya 21, fasili ya 12 ili hotuba ya Rais badala ya kujadiliwa katika kikao kinachokuja na kwa kuwa kikao tunachokwenda nacho ni kikao cha bajeti hakitakiwi kiingiliane na shughuli nyengine yoyote isipokuwa baada ya bajeti. Kwa hivyo, baada ya bajeti itakuwa ile ladha ya kuichangia hotuba ya Mhe. Rais kwa kweli itakuwa imeshatoka. Sasa naomba kutoa hoja Baraza lako tukufu likubali kuweka kanuni kando, Kanuni ya 21, fasili ya 12 ili hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ijadiliwe na Baraza lako tukufu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante mheshimiwa, hoja imetolewa na imeungwa mkono, lakini kabla sijawahoji namuomba mjumbe mmoja ambaye anatakiwa kuapa ameshafika, kwa hiyo nitamuomba…

KIAPO CHA UAMINIFU

(Mhe. Mjumbe anayefuata hapo chini aliapishwa Kiapo cha Uaminifu na baada ya kumaliza alikaa katika sehemu yake)

Mhe. Said Soud Said

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza naomba kutoa shukurani kwa mashirikiano ambayo tumeyapata lakini pia niwakaribishe Waheshimiwa Wajumbe ambao tumewaapisha hivi sasa. Kwanza kabisa labda nichukue nafasi hii kuna hoja ambayo tayari ilikuwa imeshatolewa pale na Mhe. Hamza Hassan Juma. Sasa naomba niwahoji waheshimiwa wale wote wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Hamza wanyanyue mikono yao, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tutakachokifanya ni kwamba hiyo hoja tutaanza kuijadili leo na tutaijadili na siku ya Ijumaa, ingawa siku ya Ijumaa jioni ndio itakuwa siku ya kufunga kikao chetu cha Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, kwa muda tulionao sasa hivi nitakuwa nakaribisha maombi ya waheshimiwa wote ambao walikuwa wanataka kuchangia hiyo hotuba ya Mhe. Rais. Lakini wakati maombi yanakuja nichukue nafasi hii kwanza kutangaza wageni wa waheshimiwa ambao tumewaapisha hivi punde ambao wamefika hapa.

Nianze na mgeni wa Mhe. Juma Ali Khatib; Ndugu Rashid Yussuf Mchenga, Katibu Mwenezi wa Taifa; wageni sita wa Mhe. Hamad Rashid Mohammed wanaoongozwa na Ndugu Kimangale Mussa, Mwenyekiti Bodi ya Wadhamini *ADC;* wageni wa Mhe. Modlen Siras Castico wawili wana familia Ndugu Giftness Castico na Thuwaibah Hania. Ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wajumbe mpaka sasa jina lililofika ni moja kwa hiyo naomba yaweze kuja majina. Nachukua nafasi hii kumpa Mhe. Hamza Hassan Juma awe mchangiaji wetu wa mwanzo katika hotuba hii. Mhe. Hamza Hassan Juma karibu sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kunipa nafasi hii ya mwanzo kabisa kurimbua Baraza hili tukufu la Wawakilishi ambalo wananchi wametupa ridhaa kubwa sana ya kuweza kutuchagua tukawa wawakilishi wao.

Mhe. Spika, pili nataka niwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Shaurimoyo kwa kuweza kunileta hapa Barazani nikaweza kutetea maslahi yao pamoja na Zanzibar kwa jumla.

Mhe. Spika, kwa kuokoa muda naomba moja kwa moja niende katika kuichangia Hotuba hii ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein ambayo aliitoa jana katika ukumbi huu wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, jana Mhe. Rais katika hotuba yake ametoa dira na mwelekeo wa namna gani serikali yake ilivyojipanga katika kuwaletea wananchi wetu wa Zanzibar maendeleo, lakini vile vile kuweza kuwaondolea kero mbali mbali ambazo zinawakabili katika maeneo yetu.

Mhe. Spika, kwanza nataka nianze na suala zima ambalo lilikuwa ni habari ya mjini, maana yake siku hizi mjini kuna habari nyingi maarufu zinaitwa *drip*; wananchi wengi baada ya uchaguzi walikuwa wanatuuliza kwa simu na *message*, wengine wanatuita tuwape ufafanuzi ni namna gani Dkt. Ali Mohammed Shein atakavyoweza kuunda serikali yake. Kwa hiyo, jana ile habari ya mjini tayari ameshaitolea maelezo kwamba, kutokana na maamuzi ya wananchi wa Zanzibar walio wengi ambao wamekipigia kura Chama cha Mapinduzi kwa asilimia zaidi ya 90 na Dkt. Ali Mohammed Shein wakampa kura karibu asilimia 91.4.

Kwa maana hiyo maamuzi ya Wazanzibari kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar kwa makusudi hakuna nafasi ya kuweza kuteuliwa makamu wa kwanza wa rais. Kwa hiyo, ile habari ya mjini sasa hivi nafikiri imemaliza kazi iliyobakia tuendelee kuchapa kazi.

Pia nataka nimpongeze Mhe. Rais kama alivyosema kwamba atafanya kazi bila ya ubaguzi wa rangi, kabila, dini, jinsia au mtu anakotoka. Leo tumedhihirishiwa hapa baada ya kuona jana tu baada ya hotuba yake jioni bomba limetangaza tayari ameteuwa wajumbe saba mashuhuri kabisa, wajumbe maarufu ambao anaongezea nguvu katika chombo chetu hiki cha kutunga sheria.

Mhe. Spika, kama alivyosema Dkt. Ali Mohammed Shein kwamba safari hii serikali yake anaijenga serikali itakayokuwa makini ambayo italeta maendeleo kwa wananchi wetu ambayo haitamfumbia macho mtu yeyote atakayekuwa mbabaishaji au kufanya ubadhirifu ndani ya serikali hii.

Mhe. Spika, naamini vichwa saba tulivyoongezewa leo hii vitaweza kutusaidia sana katika kujenga uchumi wa nchi yetu. Rais katika nafasi zake za uteuzi kuna watu watano amewateuwa ambao tayari wananchi walikwishakuwapa ridhaa ya kuwa-*test* katika kugombania nafasi za urais kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini vile vile kwa Rais wa Zanzibar. Kwa maana hiyo, hawa wanaonekana wanafaa na wataweza kufanya kazi hiyo kwa vizuri sana.

Kwa hiyo baada ya hayo kwa kweli nampongeza sana Mhe. Rais kwa uteuzi wake na tunawaomba wajumbe wapya mlioingia, tutakupeni mashirikiano na nyinyi mtupe mashirikiano ili kuhakikisha kwamba jahazi letu hili tunalivusha kwa salama.

Mhe. Spika, katika hotuba yake Mhe. Rais alieleza mambo mengi ambayo serikali yake inataka kuyafanya ikiwemo kuboresha na kuimarisha maeneo huru ya uchumi. Mhe. Rais tumeona ameeleza eneo la Fumba namna gani serikali ilivyojipanga lakini vilevile eneo la Micheweni serikali yetu namna ilivyojipanga.

Mhe. Spika, sasa hapa naomba sana serikali yetu kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kuna huu mradi mkubwa wa Fumba naomba sana sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tupatiwe taaluma au semina maalum, waje wale wataalamu pamoja na wale waliopewa ile miradi. Kwa sababu mimi kila ninavyoangalia bado eneo la Fumba hatujaweka *strategy* maalum kwa Zanzibar katika kuinua uchumi.

Mhe. Spika, nimejaribu kuangalia ule mradi wa ujenzi wa nyumba zinazotaka kujengwa pale Fumba nimeona nyumba za kawaida ndogo ndogo za chini. Sasa ndio maana nilikuwa ninahisi Zanzibar ni ndogo eneo letu lile angalau tulijenge katika majengo ambayo yatakuwa yanaendea juu; ghorofa 15, 20 mpaka 40 kama inawezekana ili wale wageni au wawekezaji mahoteli au wananchi watakaokaa katika maeneo yale waweze kuangalia ile *sea view* katika hali ambayo inapendeza.

Mhe. Spika, sisi ambao kwa bahati nzuri tumebahatika kutembelea nchi nyingi sana duniani, tumeona na tunapendezewa sana tunapoona majengo yanaendea juu na mengine utadhani labda yanakaribia kugonga... sitaki nimalizie hiyo lugha, nisije nikakufuru. *Astaghafirullah*. Wenzetu wanatoa mifano nchi kama Malaysia, Dubai, Hong Kong, Singapore; ukiangalia mifano hiyo wanayoitoa ni kwa *design* ya majengo ya kisasa ambayo yamejengwa katika maeneo yale. Sasa ndio maana nikasema vizuri wakaja wataalamu ambao wame-*design* ule mji au ile miji lakini vile vile tukapata aina za majengo yanayotaka kujengwa, lakini vile vile na sisi tukaweza kupata nafasi na kuweza kutoa maoni na ushauri wetu ili kuweza kuboresha haya maeneo yetu.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi mradi ule naufurahia sana lakini kama nilivyosema inatakiwa *awareness* kubwa kwa sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na sisi tuweze kuongeza *inputs* katika kuboresha maeneo yale.

Jengine, Mhe. Rais hotuba yake imelenga sana katika masuala ya kuinua uchumi; ameeleza kwamba kuna huu mji ambao umetoka katika jumba la treni pamoja na huu mji ambao umekuja nyuma mpaka kwetu Kwamtipura, ambao sasa hivi unaitwa Shaurimoyo, kwamba ule mji sasa hivi unataka kubadilishwa uje katika majengo ya kisasa. Mfano huu Mhe. Spika, tumeshawahi kuona China. Utakapokwenda China miezi mitatu hii ukiona pale kuna nyumba zipo zimekaa, zimeregea regea basi ukija baada ya mwaka mmoja unakuta tayari *grader* limeshapigwa, tayari kuna nyumba zimeelekea juu. Sasa tunataka vile vile maeneo yetu haya yaendane na *master plan* ya mji wa Zanzibar.

Vile vile na eneo la Bwawani ambalo pia tumeona sasa hivi tayari ameshapatikana mwekezaji ambaye mwekezaji huyu sisi tunamjua; ni mtu mwenye uwezo, mashuhuri na ana uwezo wa kuwekeza katika eneo lile. Lakini upo umuhimu mkubwa kuhakikisha kwamba ile *road master plan* ya Zanzibar sasa hivi inafanyiwa kazi. Tunajua kuna *road master plan* ya Zanzibar lakini naona muda unakwenda na wananchi wanaendelea kujenga katika maeneo mbali mbali. Inawezekana katika yale maeneo ambayo yamelengwa kuja kuboresha mji wetu sasa hivi utakuta maeneo yale yanajengwa, serikali itakuja kubeba gharama kubwa sana kwa ajili ya kuwafidia wananchi wale.

Mhe. Spika, hili najaribu kulizungumza pamoja na kwamba sasa hivi jengo la treni halijaboreshwa, hoteli ya Bwawani haijaboresha na maeneo mengine ya mji hayajaboreshwa tayari kumeanza kuwa na foleni kubwa ya magari, ni foleni ambayo inanishangaza sana katika kuelekea maeneo ya mjini. Sasa leo maeneo haya yakija yakiboreshwa kibiashara bila shaka watu wanaotaka kutumia pesa zao watahitaji sana kwenda maeneo ya mjini. Kwa hiyo *road master plan* hii naona inahitajika sana iweze kuangaliwa kwa haraka ili iendane na malengo ya serikali yetu ya kuwaletea maendeleo wananchi kwa haraka.

Pia tunaipongeza serikali kama alivyosema Mhe. Rais, tumeboresha sheria; Sheria ya *PPP* tayari tumeshaipitisha na tayari ile taasisi imeundwa, bado naomba sana Mhe. Spika, kwenye kamati yangu iliyopita tuliwahi kupendekeza sana suala zima la huyu Mkurugenzi atakayesimamia hii miradi ya *PPP*, bado tumpe nafasi Mhe. Rais aweze kuwa na upeo mkubwa wa kuweza kuangalia, si lazima sisi tuliomo ndani ya hivi visiwa viwili vya Unguja na Pemba na

tumpe nafasi Mhe. Rais na kama kuna haja ya kurekebisha sheria, ili hata kama ataweza kumtoa mtaalam nje ya nchi kwa mkataba maalum kuja kuboresha miradi ya *PPP* ambayo itaweza kuwavutia wawekezaji wengi kuja kushirikiana na serikali na sekta binafsi za hapa Zanzibar katika kuboresha uchumi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, ukiangalia nchi nyingi duniani maendeleo makubwa wameyapata kupitia miradi ya *PPP*. Kuna viwanja vya ndege vinajengwa kwa *PPP*, kuna mabarabara makubwa yanajengwa kwa *PPP*, kuna njia za treni zinajengwa kwa *PPP*. Kwa hiyo, *PPP* hii tunaitaka kiitwe kile kitengo kiwepo na watu wenye upeo mkubwa, wachumi na wenye upeo wa maendeleo ambao wataweza kuja kuisaidia serikali yetu kuweza kukaribisha wawekezaji kuja kushirikiana na serikali katika kuboresha miundombinu yetu ya hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, jengine ninalotaka kulisisitiza hapa katika hotuba ya Mhe. Rais amewapongeza sana wenzetu wa *ZSSF* na taasisi nyengine kwa kazi zao nzuri hata na mimi nawapongeza sana. Lakini naomba *ZSSF* bado na wao wanaweza wakashiriki sana katika ujenzi wa miradi ya nyumba, pamoja na kwamba walianza katika *plot* ya Mbweni lakini bado yako maeneo mengine. Tunguu bado yako maeneo *ZSSF* wanaweza wakashirikiana na taasisi za kifedha kuweza kuhakikisha kwamba wanajenga majengo ya kisasa, mji wa Zanzibar uweze kuwa mji wa kimataifa ambao utaendana na uchumi mpya wa gesi ambayo tunaitarajia hivi karibuni.

Mhe. Spika, vile vile katika eneo la Kariakoo, eneo hili sasa hivi tunaishukuru sana serikali kupitia *ZSSF* vile vile wameweza kuboresha eneo lile na kama tulivyoambiwa kwamba eneo lile linatakiwa liunganishwe, kwamba liwe eneo la kisasa na eneo la kibiashara katika kuhakikisha kwamba wananchi wetu wa Zanzibar wanapata maeneo maalum ya kwenda, hasa watoto wetu wanapata nafasi ya kwenda kucheza. Lakini vile vile kupata burudani na kuimarisha mazingira ya Zanzibar.

Mhe. Spika, Mhe. Rais pia ametaja Karakana ya Matrekta Mbweni na mimi nimeshukuru sana kwa mtazamo wa Mhe. Rais na mikataba ambayo tayari imeshaingiwa na Kampuni ya Mahindra ya India ambayo wataleta matrekta yao kuja kufunga pale katika karakana ya Matrekta. Mimi ninaishauri sana serikali karakana ya matrekta pale kuna mafundi wazuri, wataalamu, lakini vifaa tulivyokuwanavyo kwa kweli vingi ni vya kizamani. Kwa hivyo, taasisi ile tunatakiwa tuiboreshe, lakini ili kuiboresha taasisio ile ya Karakana Mbweni naomba taasisi ile sasa hivi iwe shirika, ikiwa shirika kwa kweli wataweza kubuni mbinu za kujitegemea na wataweza kufunga mikataba na taasisi mbali mbali duniani za kifedha, vile vile za kitaaluma ili kuhakikisha kwamba Karakana ya Matrekta inaboreshwa na inaendana na ile kasi ambayo imekusudiwa na serikali yetu.

Mhe. Spika, eneo la uvuvi. Mimi ninasikitika sana katika Idara ya Uvuvi, kwa nini ninasikitika Mhe. Spika? Tulikuwa tuna mradi wa *MACEMP* mradi ule uliweza kuenea katika vijiji takriban vyote vya Unguja na Pemba. Mradi ule ulikuwa unatoa maboti mengi sana kwa wananchi, ulikuwa unatoa vifaa vingi vya uvuvi kwa wananchi, unatoa mpaka mafriza na mambo mbali mbali lakini katika kipindi hiki mradi ule naona kama unasua sua. Sasa tatizo sijui ni nini mpaka wakulima wa mwani walikuwa wanafaidika sana na mradi ule.

Sasa kwa kuwa hotuba ya Rais imezungumzia suala la kuboresha uvuvi wa bahari kuu pamoja na maeneo haya ya juu, ninaomba sana wale watakaopewa dhamana katika mamlaka hii, wahakikishe kwamba mradi ule wa *MACEMP* tunauboresha kwa sababu ulisaidia sana kupunguza tatizo la umasikini katika vijiji vyetu mbali mbali vya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kwa kweli sio katika eneo hili tu la *MACEMP*, lakini kulikuwa kuna mradi ambao tulipata taarifa ulikuwa unatekelezwa kuletwa maboti kwa ajili ya kwenda kuvua katika bahari kuu. Kwa kweli hiyo tutakuja kuizungumza katika bajeti kuu ya serikali kwa sababu hotuba hii ya Mhe. Rais haijibiwi, hawatakiwi mawaziri kujibu lakini haya tunatoa maoni na changamoto kwa wale watakaokuja kupewa hizi taasisi, hebu wajaribu ku-*review* waangalie yale maendeleo yaliyopatikana katika miradi ya uvuvi kipindi kilichopita. Je, ni hatua gani tunatakiwa tupige katika hiki kipindi kilichobakia.

Mhe. Spika, nimeshakuona unaanza kuikamata *microphone* yako unanitazama kwa dalili kwamba nimechukua muda mkubwa, lakini nilikuwa najaribu kuonesha njia ili na wenzangu wajue maeneo gani ya kuweza kupita.

Mhe. Spika, kwa kumalizia kabisa tunampongeza sana Mhe. Rais kwa kuchaguliwa na wananchi kwa asilimia kubwa, lakini vile vile kwa hotuba yake ambayo inalenga kuleta maendeleo makubwa ambapo maendeleo hayo

yatagusa mpaka jimbo jirani la Chumbuni, ambapo bandari ya mpigaduri tunategemea tumeambiwa ndani ya mwaka unaokuja basi harakati za ujenzi wa bandari ya mpigaduri... Kwa kifupi huu ni mtazamo mkubwa na mimi natoa wito kwa wananchi kwa kumalizia, wasisikilize maneno ya pembeni tusitegemee labda aje mjomba kutusaidia, haya yaliyopangwa na serikali yetu tuyaunge mkono, tuhakikishe kwamba serikali yetu inafanya kazi kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache naiunga mkono hotuba ya Rais kwa asilimia mia moja, ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamwita mchangiaji naomba nichukue nafasi hii kuwatambuwa wageni wa Mhe. Balozi Amina Salum Ali nao ni Balozi Mohammed, Bwana Omar Said na Hamza Mgeni, naomba mnyanyuke hapo mlipo. Ahsante, baada ya hapo tunaendelea kuchangia hotuba lakini kwa maombi maalum nimeombwa na Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali kwa hiyo nitamwita yeye kama mchangiaji wetu wa pili na baada ya hapo Mhe. Ali Suleiman Ali ajiandae ambaye atafuatiwa na Mhe. Mohammed Aboud Mohammed.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii, hatuna budi kumshukuru mwingi wa rehema aliyetupa pumzi ya kuwepo hapa katika Baraza hili tukufu na na nishukuru kwa kunipa nafasi hii kwa heshima na taadhima kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini.

Mhe. Spika, nichukuwe nafasi hii kwa niaba ya wananchi wenzangu wa Jimbo la Uzini pamoja na mimi mwenyewe. Nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa hotuba yake iliyojaa hekima, busara na usikivu. Mimi hotuba hii nasema ni hotuba ambayo imeelekeana na utendaji wetu wa ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Baraza hili Mhe. Spika, utekelezaji wetu ni wa Chama cha Mapinduzi. Mhe. Rais kwa huruma zake na kwa usikivu wake amegusia mambo muhimu sana mengi na mengine nitayaacha, wako wenzangu wengi, lakini kubwa zaidi nitagusia suala la afya, maji, barabara za ndani umeme kilimo na mambo mengine kwa jumla.

Mhe. Spika, serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar imeshafanya mambo mengi sana toka Mapinduzi mpaka tunapoendelea na tulifanya Mapinduzi kuwaletea wananchi wetu maisha bora katika nchi yetu hii. Mmoja alijiona bora tukafanya Mapinduzi ili tupate usawa wetu sisi hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi niombe katika kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi na kwa bahati nzuri Mwenyezi Mungu atawajaalia mawaziri wetu watakuja. Mhe. Spika, awamu ambayo tuliimalizia ya sita chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohammed Shein na Makamu wa Pili wa Rais Mzee wetu Balozi ambaye ndie kiongozi wetu, kuna ahadi nyingi zililotelewa.

Mhe. Rais amefanya ziara katika sehemu mbali mbali na kuzitolea ahadi na tulipofika katika Baraza letu la la Mawaziri na tulipofika hapa baadhi ya Mawaziri walitamka kwamba hili litamalizika kabla siku si zake. Sasa Mhe. Spika, mimi kwa huruma kwa sababu tumekuja hapa kwa niaba ya wananchi, tumekuja hapa kuwatumikia wananchi na matumaini ya Wazanzibari yamo ndani ya Chama cha Mapinduzi.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba Mhe. Spika, zile ahadi ambazo Mhe. Rais amezitoa katika visiwa vya Unguja na Pemba iwe kipaumbele katika bajeti hii inayokuja ili itekelezwe ile ilani yetu kwa sababu serikali yetu ina mambo mengi, hali yetu ya uchumi hai hoi, tunachokipata ndio tunachokitumia. Lakini kuna vitu ambavyo vimeachwa kwa muda mwingi na wizara ambayo inavyoongoza kwa ahadi ni Wizara ya Elimu, najua kuna mambo madogo madogo Mhe. Spika.

Wizara ya Elimu Mhe. Rais ameshaahidi mambo mengi sana mengine matofali tu, mabanda wananchi wajitolee kujenga skuli ili serikali ije kumaliza. Wizara inampeleka Rais anatoa ahadi wizara haina habari kabisa. Lakini anampeleka Rais zile fedha za matayarisho kwenda Rais katika sehemu ile hata milioni ishirini ataendewa Omar Kingi atowe, unajua hii kama Rais anakuja hapa anakuja kuweka ahadi zake hapa. Lakini zile milioni ishirini, ile ahadi aliyoitoa Mhe. Rais katika utekelezaji wa banda la Skuli haifiki hata milioni tatu, mimi nina ushahidi.

Sasa kwa kweli Mhe. Spika, inatutonesha kwamba Rais anapokwenda pesa za ziara zile za ufanikishaji wa kuweka shamiana, ngoma zinapatikana. Lakini pesa ambazo Mhe. Rais ameziahidi kama banda hazipatikani. Sasa kwa kweli

Mhe. Spika, mimi naona tuombe sana kupitia kiongozi wetu mkuu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwamba ahadi zetu tunazozitoa pamoja na sisi viongozi Wawakilishi tuweze kuzitekeleza, ili tuweze kuwapa matumaini Wazanzibari na wananchi wa Tanzania na Zanzibar waliopo Zanzibar kuwa na imani na Chama cha Mapinduzi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kubwa ninalotaka kusema kwamba mimi naunga mkono hotuba yake lakini vile vile suala hili la posho, semina na mambo mengine kwa kweli tulitizame. Sasa hivi tuna kipindi kigumu, mapato yetu yatakuwa ya kiasi. Kwa hivyo, tuhakikishe kila kinachopatikana inatekelezwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa sababu Mhe. Spika, mtu yuko kazini kuanzia saa moja na nusu mpaka saa tisa na nusu. Lakini mpaka saa tisa na nusu anakwambia kuwa kuna semina, kuna posho ndio kama jana aliposema Mhe. Rais kuna vitu lazima tuwaonee huruma wananchi wetu ndio waliotufanya sisi Baraza hili kufika bila ya wananchi Mhe. Spika, Rais asingepatikana kwenye Chama cha Mapinduzi na sie tusingepatikana ndani ya Chama ndio hili Baraza la Wawakilishi tumekuja hapa kuwa watumwa, watumishi, wafanyakazi kwa wananchi wetu bila ya kujali rangi, kabila na dini.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, Mawaziri wanaokuja Mungu akijaalia wawe wasikivu, lakini anakuja waziri anasukuma tu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, matumaini yangu kwa Baraza hili hakuna Bajeti itakayokwama. Lakini jamani tuwaonee huruma wananchi wetu kuna wananchi leo hali zao za umasikini Mhe. Spika, mtu anakula mlo mmoja mimi nimevaa suti hapa, lakini nilievaa suti hii ni mwananchi alienifanikisha nivae suti hii, lakini kuna watu wanakula mlo mmoja tuwafikirie. Kuna suala la ajira ya wafanyakazi, kuna watu masikini ambao wazee wao wamewasomesha watoto wao, mkulima kauza viazi, kauza ndizi, mtoto wa mkulima amemaliza ajira hapati kwa sababu hana umaarufu, hapati kazi.

Sasa Mhe. Spika, hiyo inaumiza sana mimi Mwakilishi hapa niliekuwepo niingize familia yangu, mimi Mwakilishi niingize upande wa mke wangu, hatuwezi kufika. Mapinduzi yetu ni ya wanyonge Mhe. Spika, sio umimi, umimi kesho hapa Mwenyezi Mungu akitujaalia tunamsomea Marehemu Mzee Abeid Aman Karume hitma. Mzee Karume kazi aliyoifanya ni kuwatumikia wananchi.

Kwa hivyo, ninachoomba hizi sehemu za kazi wananchi wetu wale wakulima waangaliwe watoto wao ajira, imekuwa tunaitumia sisi ikiingia kwenye sehemu zote yule mtoto wa mkulima masikini hana nguvu lakini matumaini yake ni ya Mapinduzi yetu Matukufu ya 1964 na sisi ndio tunaokuwa na dhamana. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi niko tayari kwa niaba ya Kampuni zangu pamoja na wafanyabiashara tutaichangia nchi yetu katika kutelekeza ilani ya Chama katika Afya, Maji, Barabara. Tuambiwe tu eti bwana serikali hii hapa ina milioni kumi hapa panahitajika milioni tano Mhe. Spika, sisi bila serikali hii tusingelifika hapa. Mimi nisingefika hapa, mie nisingelifika hapa kama si serikali hii, ndiyo iliyotusomesha sisi na serikali hii ndio iliyotupa nguvu zote hizi, nguvu za Mohammedraza bila ya serikali yangu nisingelifika hapa.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa heshima zote naomba mawaziri watakaokuja wawe wasikivu, wazipitie ahadi za Rais. Kwa sababu itakuwa aibu sana Mhe. Spika, Rais kaahidi mabati mia tunakuja kumzungumza kwa nini Rais wa nchi lakini pesa zinazotaka kutumika kwenye shamiana milioni kumi zinapatikana, anaambiwa tu Omar King, Rais anakuja, hujatoa pesa sherehe hamna. Lakini Rais katoa ahadi mabati mia haitekelezeki.

Mhe. Spika, sote wasikivu ninachotaka kutoa ahadi serikali yetu kila inachofanya kitangazwe hivi keshokutwa tunaelekea katika mwezi wa Ramadhani, serikali yetu maisha yote inawajali wananchi. Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohammed Shein inajali wananchi wake. Kuna ushuru huu unaosamehewa wa mchele, sukari, unga wa ngano; itangazwe wazi ili wafanyabiashara na wananchi wapate neema. Lakini inafichwa karibu na mwezi wa Ramadhani meli zimeshakuwa nje hapo. Sasa hawa wafanyabiashara wadogo wanakuwa wanaumia. Sisi tulikuwa huku na hawa tuwafikishe huku wafanyabiashara tulipokuwa.

Kwa hivyo, ingelikuwa wazi kila serikali inapotoa tamko la kusamehe chakula serikali inafanya mambo mengi. Mhe. Spika, nataka nikuhakikishie mpaka hapa nilipo hakuna ushuru uliopanda, hakuna chochote kilichopanda kwenye *TRA* lakini na sisi wafanyabiashara tujifunze kulipa kodi. Kodi ni muhimu kwa sababu kodi hizi ndio zinakwenda kwa wananchi, zinakwenda kwenye maji, umeme, afya bila ya kodi hatuwezi. Kwa hivyo, tusiwe wajanja unajua Mhe. Spika, mfanyabiashara akipunguziwa faida anaona kama ananyanganywa lakini hakuna ushuru uliopanda, hakuna bidhaa zilizopanda.

Mhe. Spika, lililokuwepo nataka nizungumze wazi kwamba serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar imeeka utaratibu maalum wafanyabiashara wa Zanzibar kupitia *TRA* kodi zetu Mhe. Spika, ni za Zanzibar haimuumizi mtu yeyote. Lakini Mhe. Spika, katika kuvuruga masuala kama haya unaleta gari unalipa dola 1000 halafu gari ile ile wewe unachukuwa unapeleka Tanzania Bara, kule Tanzania Bara ukalipe *difference* huu ni upendeleo kwa Wazanzibari kwa wafanyanyabiashara na wananchi. Lakini haiwezekani yule analipa dola 5,000 halafu wewe unalipa dola 1000 unataka kuichukuwa gari bila ya kulipa nenda pale *TRA* ukamwambie mie bwana gari yangu hii nataka kuichukuwa Tanzania Bara, yule Kamishna Mcha atakwambia bwana ukiitumia Zanzibar dola 1,500 unataka kuipeleka Bara lipia dola 4,000 *that is simple*.

Kwa hivyo Mhe. Spika, hakuna kilichopanda na hata hiki chakula Mhe. Spika, serikali yetu ina huruma toka Mapinduzi matukufu ya Zanzibar. Kwa hivyo, tusifike tukajenga dhana chakula kimepanda, biashara imepanda aje anambie mtu mie nje bwana mimi hapa nimekula hasara, tatizo ni kupunguza na sisi kama wafanyabiashara tunataka kujiongezea. Lakini vile vile tuwe na huruma na wananchi.

Mhe. Spika, kwa taarifa yako nataka nikwambie mie nawapongeza wafanyabiashara bei ya sukari imeshuka leo, sukari kilo tano Shs.7,000/= mpaka Shs.7,500/=, vyakula vingi vimeshuka na tunapokwenda lazima viwe vinashuka tunapokwenda kutoa ushuru kupunguza chakula mwezi wa Ramadhani kodi zitakuwa hazipo. Kwa hivyo, wafanyabiashara waambiwe bwana wee hii sukari mnayouza sasa hivi ni Shs. 7,500/=, sasa hii sukari tunakusamehe tuambie mlaji atapata kiasi gani.

Mhe. Spika, kuna wafanyabiashara ni waungwana wa chakula kina Bombay, Bopar wote. Lakini hawa wa kati hawa wanakwenda kununua biashara yoyote halafu wanaificha ndani ishakwisha Ramadhani biashara ile mtu wa tatu yule mfanyabiashara wa tatu wanaanza kuuza biashara kwa bei kubwa. Kwa hivyo, wafanyabiashara hawa kina Simba chai, Bopar, Bombay Bazar mimi nawapongeza sana wafanyabiashara wote kwa sababu ni watu waadilifu na ambao mimi niliwaendea wakanambia mtu wa tatu wa nne anaekwenda ghalani.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi naomba kwa niaba ya wenzangu tumekuja hapa tuwatumikie wananchi wetu ili Mwenyezi Mungu akitupa uhai na uzima *inshaallah* na pumzi zetu mimi nataka kusema kwamba miaka mitano baadae hapa kutakuwa kweupe kama anavyosema msemo Mzee Kwacha. Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi kwa haya yote nashukuru naishukuru serikali yangu.

Mimi hapa bila ya chama nisingelikaa kwenye kiti hiki. Kilichonileta hapa ni Chama cha Mapinduzi. Kwa hivyo, tunachotaka Mhe. Spika, tutekelezeni ilani unapopeleka barua tuambizane jamani kweli hali yetu iko hivi, ili tuwe na busara ya kumsaidia Rais.

Mhe. Spika, mwisho nataka kusema Rais wa Zanzibar na Makamu Mwenyekiti wa CCM alitubeba mgongoni kuinadi ilani ya Chama cha Mapinduzi. Uchaguzi tumemaliza tukawatumikie wananchi wa Unguja na Pemba bila ya kujali rangi, kabila na mimi nasema nilipokuwa mkereketwa wala sikuwa Mwakilishi alinitia Boznia akanambia Mohammedraza kazi kubwa tuliyokuwa nayo sisi viongozi ni kuwatumikia wananchi. Kwa hivyo, ninachoomba Mhe. Spika, kwa heshima uliyonipa lakini naomba vile vile kwamba mawaziri watakaokuja waone ile bajeti na zile ahadi zilizotolewa na Rais na haya mengine ambayo Rais ametoa, hii ni sawa sawa na ilani ya Chama hiki kitu ambacho kitatuwezesha sote tuwe wakweli.

Kwa hivyo, kubwa zaidi watendaji tuwe wakweli jembe ita jembe, pauro ita pauro. Mhe. Spika, kwa hayo machache nashukuru sana, Mwenyezi Mungu atubakiri, Mungu ampe afya Rais pamoja na wasaidizi wake na sisi ili tuweze kutekeleza ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii na kwa uwezo wake kusimama hapa katika Baraza hili ili kuchangia hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Pili nikupongeze wewe Mheshimiwa katika kiti chako hicho kwa mara ya kwanza kuwepo hapo na kuendelea na shughuli zetu.

Tatu nawashukuru wananchi wangu wote wa Jimbo la Kijitoupele kwa kunipa ridhaa ya kuwaongoza katika Baraza hili na ahadi zangu ambazo nimeziahidi kuwa naamini nitazitekeleza kama nilivyozipanga, sitorudi nyuma.

Mhe. Spika, hotuba ya Mhe. Rais tumeisikia na ina dhana nzito hasa tukizingatia kwamba imekusanya mambo mengi na mambo hayo ya msingi kuna suala kwanza la huduma za jamii, huduma za jamii ndio roho ya serikali, huduma za jamiii ni mkusanyiko wa mambo mengi. Unakuja kwenye maji, umeme, elimu, afya na barabara zetu.

Mhe. Spika, bila ya kuwa na hilo hatuna mafanikio katika kuwasaidia wananchi wetu na panapokuwa na kero katika sehemu yoyote hii ikikosekana huduma hiyo basi patakuwa na dhiki na adha kwa wananchi wetu wanaoishi katika sehemu hii bila ya maji hapakaliki katika eneo, bila ya umeme huna raha ya kufanya maisha yako yaendelee mbele, bila ya barabara hakuna huduma ya daladala hata gari inashindwa kufika. Afya ni sehemu ambayo ya mwisho ina mambo mengi ya kusaidia jamii yetu ili iwe nzuri na kupata afya zao kuendesha maisha yao kila siku.

Mhe. Spika, Mhe. Rais kazungumza mambo mengi sana na azma yake moja tu serikali atakayoipanga mwenyewe anaijua yeye hapa hatuwezi kujua maana kuna siri nzito kaiweka mwenyewe labda na wasaidizi wake sie tutaipokea. Lakini tunaomba tu kwamba mawaziri watakaoteuliwa na wasaidizi wao makatibu wakuu, wakurugenzi wao ni mihimili ya maendeleo katika nchi hii na jamii yetu bila ya kuwa waaminifu na bila ya kuwa ni watu ambao ni wakarimu katika shughuli zao, kuhakikisha tunafanya kazi vizuri tutapata shida na kuwa na adha kwa jamii yetu inayotutegemea katika maeneo yetu.

Namuomba sana Mhe. Rais mawaziri wote watakaowateuwa wawe waadilifu, wawe wafatiliaji wa mambo. Nakumbuka huko ninakotoka wakati mdogo sana Rais wetu wa Zanzibar mzee Abeid Amani Karume nilimkubuka alikuwa mabonde ya mpunga, hatoki kwenye majenzi, kwenye barabara hatoki. Lakini sasa utawakuta mawaziri wetu baadhi zile shughuli zao ziko ofisini, nafikiri hawajui kwamba huko mitaani kuna matatizo ya maji katika maeneo kuna matatizo ya kilimo, kuna matatizo ya ufugaji, unakuwa Mhe. Waziri anaehusika na watendaji wake wafike katika sehemu zile kusaidia jamii yetu ili ifanikiwe.

Mhe. Spika, tatizo kubwa linalotukabili katika nchi yetu ni uchumi na uchumi tuliokuwa nao tunao Mungu alivyotujaalia hivi hivi kidogo tukubali matokeo hayo hayo. Lakini kidogo tulichokuwa nacho ukikidhibiti utafanikiwa. Kwa hivyo, naiomba serikali mapato yanayopatikana yadhibitiwe na bila ya kudhibitiwa mapato hatuna kitu tunachokifanya huko mbele, tunapokwenda naamini tunasikia wakubwa huko nje, Marekeni wanasema wanazuia misaada lakini hiyo ni hiari yao sisi Wazanzibari tunamuamini Mwenyezi Mungu zaidi kuliko Mmarekani. Kwa hiyo, kile utakachokipata, utakachokichuma kwa jasho lako ukidhibiti na kukichunga ili kiwafikie walengwa wetu.

Niseme Mhe. Spika, kama mapato tutayadhibiti tutafanikiwa kwa asilimia kubwa sana, tutagawana kwenye elimu, maji, barabara, afya na mengineyo.

Mhe. Spika, tatizo letu tulilokuwanalo katika nchi. Hivi sasa tunajua tu kwamba Mhe. Rais kachanganya sana katika hotuba yake nzuri, kaona kwamba ipo haja ya kuongeza mishahara. Mishahara ni kichocheo cha maendeleo, lakini mishahara ufanye kazi ili iongezeke. Mimi nimuunge mkono sana Mhe. Rais kwamba wafanyakazi wote wa taasisi zote wafanye kazi kwa bidii ili mshahara aliyoahidi Mhe. Rais uongezeke. Lakini katika vikosi vyetu, yaani Idara Maalum.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa mwanajeshi na nilikuwa nina wivu sana wa maendeleo, na nilikuwa ninachukiwa sana na baadhi ya watu wengine katika sehemu nyengine. Mwanajeshi ana nafasi yake nzuri ya kazi zake, hana muda wa kwenda kulima, hana muda wa kwenda kufanya biashara, yeye kazi yake yuko *standby* kwa lolote litakalotokezea, lakini anaamini kwamba litokee la amani lisitokee la shari, lakini wajibu wake lolote litakalotokea alikabili. Kwa hivyo, vikosi vya SMZ vina jukumu zito na vina jukumu la ulinzi, na tumeona mazingira yetu tuliyokuwanayo katika mambo mbali mbali yaliyotokea hata katika chaguzi zetu, bila msaada wao kwa kushirikiana na vikosi vya SMT basi hawana uwezo peke yao.

Kwa hivyo, namuunga mkono Mhe. Rais kuona taasisi mbili hizi. Wafanyakazi wa serikali kuongezewa mishahara na kufikia shilingi 300,000, na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akitujaalia uwezo huko mbele zitaongezeka zaidi.

Lakini Idara Maalum ni sehemu ambayo na mimi nampongeza sana Mhe. Rais kwa kuwaona askari hawa kuwaongezea mishahara, ili ilingane na wenzetu wa Tanzania Bara.

Naamini vijana wetu wasikivu na vijana wetu waaminifu, hivyo hili litaleta chachu ya maendeleo, tuseme kama nizamu katika kazi zao. Kwa sababu Mhe. Spika, baadhi ya maaskari walikuwa wanajisahau. Anaweza kuacha lindo akaenda kuuza kitu, akamuambia mwenzake nikamatie silaha yangu hii, kumbe ni hatari kwa upande wao. Mimi mbinu nazijua zote. Kwa hivyo, niseme tu kwamba hili ni kichocheo cha maendeleo na vikosi vyetu kufanyakazi zao vizuri, ili kufanikisha masuala yanayotakiwa katika ulinzi wa nchi yetu na wananchi wetu kwa jumla.

Mhe. Spika, kuhusu suala la walemavu; nampongeza kwa dhati kabisa Mhe. Spika, kwa kuliona hili na kaliona wakati mzuri ambapo walemavu wetu wengi wanapata adha kwenye usafiri na kwenye huduma nyengine. Kwa hivyo, nampongeza Mhe. Rais kwa kuliona hili na walemavu wetu wanastahiki kupewa kila stahiki, ili angalau na wao wajisikie kama na wao ni wananchi kama watu wengine. Lakini ukija kwa wanawake, wana makundi mengi. Kwa mfano mimi katika Jimbo langu la Kijitoupele naweza kupata vikundi kama 78 kama sikosei. Nawapongeza kinamama na vijana wa jimbo langu, kwa kukaa pamoja na nimeahidi nitatoa fungu zuri langu mimi mwenyewe, kwa jasho langu, sitowakopesha nitatoa ahsante katika kazi zao ili wajiendeleze katika maisha yao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, dhamira yangu kubwa hapa ni kuisaidia jamii, katika jimbo langu na menginеyo, kwa sababu sisi sote ni Wazanzibari. Usione Shihata unafanyakazi katika Jimbo la Kijitoupele ukasahau kwengine, kumbe na wewe una haki ya kuwasaidia wengine waliokuwa hawana uwezo ule, kuwapa maarifa au kusaidia kidogo kidogo ili na wao wajisikie wananchi wetu.

Mhe. Spika, jengine ni kundi la watoto ambalo lina mashaka makubwa sana sasa hivi. Ubakaji umekuwa mkubwa, vitendo vya utovu wa nidhamu vimekuwa vingi kwa watoto wetu. Ndio maana Mhe. Spika, mimi nilipoingia katika jimbo langu jipya lina mambo mengi. Maana Jimbo la Kijitoupele nimelirithi kutoka sehemu tatu. Kutoka Jimbo la Fuoni, Jimbo la Dimani na Jimbo la Mwanakwerekwe ninakoishi. Lakini bahati nzuri lina mazingira tofauti, ukenda Kwarara Juu, Mhe. Makamu wa Pili keshafika huko kenda kuweka jiwe la msingi kwenye shule, barabara zake mvua kama hii inayoendelea sasa hivi haipitiki.

Maji ya kunywa ni kama togwa, tunalijua wengi hapa. Togwa ni mtama unaochanganywa na mambo mengi linakuwa jeupe hivi, hiyo ni adha wanayopata wananchi wangu na nimekula kiapo ndani ya muda mfupi tukijaaliwa, baada ya kupita mvua barabara ile nataka angalau ipitike vizuri, ifike mpaka kule Kwarara na kule alikokwenda Mhe. Makamu wa Pili wa Rais mpaka kuna sehemu inaitwa Madina. Barabara za Kwarara sitokubali kama mimi ni Mwakilishi wa Jimbo hilo ziishie njia nne. Kuna njia sehemu kunajengwa Msikiti ndio njia nne, nataka zifike Madina. Wananchi wanapata shida, watoto wakienda shule wanapata shida. Suala hili nitakuja kulizungumza kwenye bajeti itakayokuja ili tujuwe la kufanya, lakini mimi mwenyewe kama mwakilishi na mbunge wangu Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, tumejiandaa kuangalia kama *First Aid* kuwaondolea adha wananchi wetu kwenye visima na kwenye barabara zetu.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu watoto. Nakiri kwamba nilazima tuwasaidie watoto kwa hali na mali, wazee wetu tunaoishi nao katika maeneo, walemavu na wazee ni watu ambao wanataka kusaidiwa sana. Kwa hivyo, mimi mwenyewe binafsi pamoja na mbunge wangu tumetoa ushauri wa pamoja, maana mimi bila ya mbunge siko vizuri, maana itakuwa mimi nimekwenda mguu wa kulia na yeye anakwenda mguu wa kushoto. Nataka twende mguu mmoja wa kulia mbele na wa kushoto nyuma, hiyo ndio siri ya mafanikio katika jimbo.

Mhe. Spika, nimekaa Jimbo la Mikunguni miaka 15 na Kwahani, nafikiri mafanikio niliyoyapata nilikaa na wabunge watatu, sikugombana na mbunge mimi, mbunge yuko bungeni mimi niko hapa nafanyakazi. Kwa hivyo, mwenzangu akiwa hayupo mimi nipo kwa niaba yake, lakini tufanye kazi ili tulete maendeleo. Kwa hivyo, wazee inabidi tuwasaidie kwa njia yoyote, tuwasaidie walemavu na watoto yatima tunaoishi nao katika maeneo. Tutafute njia za busara serikali, hawa wenzetu wanaishi katika mazingira mazito. Kuna kinamama wetu wanafiliwa, mama ana watoto wanne, watatu au mmoja, lakini kufiliwa ni suala gumu. Kwa hivyo, tuseme ni lazima utakufa madhali umezaliwa, kila mtu ana tarehe yake anayoijua Mwenyezi Mungu, hatupingani na Mwenyezi Mungu, lakini baada ya kufiliwa inafaa sisi tukae tuwafikirie wenzetu.

Mhe. Spika, mimi nitakuwa na kazi nzito kwa sababu makundi manne haya, vijana, watu wenye ulemavu, wazee na watoto. Nafikiri nitawaweka kundi moja na kufanya utaratibu mbali mbali wa kuwafikia, ili kila muda unavyostahiki kuwapa angalau chochote na kuwaweka pamoja na wao wajisikie kama wanaishi na viongozi wao.

Mhe. Spika, kuna suala hivi sasa limeingia katika nchi yetu; saruji inauzwa shilingi 25,000/- na wafanyabiashara, Mhe. Spika, huu ni ubadhirifu, nafikiri hii ni *sabotage* inafanywa makusudi. Naiomba serikali, saruji leo hii nimekwenda kuuliza bei, kutoka shilingi 15,000/- mpaka shilingi 25,000/-. Mimi kawaida yangu Mhe. Spika, mawaziri watakaokuja tunajuana, nikimuuliza swali la nyongeza basi nina uhakika nalo, nikimuandikia swali mama nina uhakika nalo. Saruji leo hii nimekwenda kuuliza kama kutaka ule ukweli niupate, basi ni shilingi 25,000/- iko madukani kwenye baadhi ya maduka. Sasa hapa pana kitu serikali ni lazima ijidhatiti kuzungumza na wafanyabiashara ili kujua ongezeko hili limesababishwa na nini.

Mhe. Mohammedraza alizungumza neno zuri tu kwamba serikali haijaongeza kodi, lakini wafanya biashara fulani wana muelekeo wa sehemu fulani, nafikiri hawa wanafanya makusudi ili kutaka kuikomoa serikali. Lakini nasema serikali huwezi kuikomoa utakomoka wewe mwenyewe uliyeleta hayo. Kwa hivyo, niiombe serikali hivi sasa tukae tujidhatiti kufanya shughuli zetu ili kujiletea manufaa.

Mhe. Spika, najua kuna mengi, lakini nasema tu ajira ni sehemu muhimu. Najua ajira serikalini hakuna, lakini Mhe. Rais kazungumza habari ya viwanda vya samaki na viwanda vyenginevyo. Kwa hivyo, naiomba serikali tuhakikishe kwamba tunajenga viwanda vya samaki, tumezungukwa na bahari pia na viwanda vyengine, ili vijana wetu wapate ajira.

Baada ya hayo Mhe. Spika, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kijitoupele, yaani jimbo jipya. Napenda kusema kwamba naiunga mkono hotuba hii ya Mhe. Rais kwa asilimia mia moja. Nakushukuru Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Waheshimiwa Wajumbe, kuna mjumbe kaniletea kwa maandishi angependa kujua muda wa kuchangia tunachangiaje. Napenda kumtanabahisha kwamba aangalie kitabu chetu cha kanuni, kanuni ya 58(6) ambayo inasema;

Kanuni ya 58(6)

> "Kila mjumbe anayejadili hoja ataruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika 20 wakati wa mikutano ya kawaida na dakika 30 wakati wa mikutano ya bajeti. Lakini Spika, akiona inafaa, anaweza kumuongezea msemaji dakika si zaidi ya 10".

Kwa maana hiyo wajumbe wote waliozungumza mpaka sasa hivi wamezungumza ndani ya muda ambao umewekwa kwa mujibu wa kanuni, ahsante tunaendelea. Sasa namuita Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, ambaye atafuatiwa na Mhe. Hamad Rashid Mohammed na Mhe. Juma Ali Khatib ajiandae.

Mohammed Aboud Mohammed: Mhe. Spika, kwanza nichukuwe fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tena na kutuwezesha kuwemo katika Baraza hili tukufu. Mwenyezi Mungu ambaye ndiye muumba wa kila kitu, kila kitu yeye ndio tutarajie kutoka kwake. Mwenyezi Mungu sote tuliomo humu ndani atujaalie kheir, mafanikio makubwa, pamoja na wananchi wote wa Zanzibar.

Aidha, nichukuwe fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kusema machache kuhusu hotuba hii muhimu aliyoitoa Mhe. Rais wetu.

Sasa nianze kwa kukupongeza wewe Mhe. Spika, kwa kuchaguliwa na wajumbe wa Baraza hili tukufu kwa kura nyingi sana, nakupongeza sana. Nadhani umekuwa historia na mfano kwa maspika waliopata kura nyingi katika Baraza hili tukufu. Nakutakia kila la kheir wewe, Mhe. Naibu Spika, pamoja na viongozi wote walioteuliwa kutuongoza katika Baraza hili. Nawatakia mafanikio makubwa na maendeleo katika nchi yetu.

Vile vile nichukuwe fursa hii nimpongeze sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi. Nampongeza kwanza kwa sababu ni mwalimu wangu wa siasa. Namshukuru sana alinilea sana kwenye shughuli za

kisiasa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Kwa hivyo, Mhe. Balozi nakushukuru sana na nakutakia kheir na mafanikio makubwa katika shughuli zako za siasa na za kifamilia kwa jumla.

Aidha, niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili tukufu, wale waliochaguliwa na wananchi na wa viti maalum na walioteuliwa na Mhe. Rais, sote tuna wajibu mmoja wa kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atuwezeshe na atupe uwezo mkubwa wa kutekeleza majukumu yetu. Pia niwapongeze wananchi wote wa Zanzibar kwa kufanya uchaguzi kwa amani, usalama na utulivu mkubwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, uchaguzi huu ni wa kihistoria katika nchi yetu, ulifanyika katika mazingira ya amani, uhuru na haki. Kwa msingi huo tuna haki ya kukipongeza sana Chama cha Mapinduzi, kwa namna ambayo kilivyoaminiwa na wananchi kwa kuwa asilimia kubwa tuliomo humu ndani ni wajumbe kutoka Chama cha Mapinduzi.

Nataka nivipongeze vyama vyengine vyote vya siasa vilivyoshiriki katika uchaguzi ule. Kushiriki kwao kumejenga matumaini mapya ya kujenga Zanzibar mpya, yenye maendeleo makubwa. Nawapongeza wote na hasa wale ndugu zangu waliopata fursa pia ya kuteuliwa na Mhe. Rais kushirikiana na sisi katika jukumu hili la kujenga nchi yetu, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa tumemaliza uchaguzi kazi iliyombele yetu ni kujenga nchi yetu, na kwa kuwa hotuba ya Mhe. Rais wetu imeeleza kwa kina namna ambavyo serikali yake imekusudia kuyatekeleza katika miaka mitano. Vile vile hotuba hii imeeleza mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Kwa hivyo, mimi nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Rais na serikali yake kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, na vile vile nimpongeze kwa kazi kubwa anayoelekea kuifanya katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Kwa sababu nimeisikiliza kwa makini jana hotuba ile imegusa sekta zote muhimu katika ujenzi wa nchi yetu.

Changamoto kubwa iliyombele yetu Mhe. Spika, ni kwamba Wazanzibari sote sasa tushirikiane kwa pamoja tukajenga nchi yetu. Sasa uchaguzi umekwisha, kazi iliyombele yetu ni kujenga nchi yetu. Naomba sana tuwache aina zote za siasa ambazo zitarudisha nyuma maendeleo yetu.

Tatizo letu kubwa Wazanzibari Mhe. Spika, ni kurudia siasa za chuki, uhasama na kutumia jambo ambalo halijaleta manufaa yoyote katika kipindi chote ambacho kumekuwa na siasa za chuki. Kwa hivyo, nawaomba Wazanzibari wenzangu wote ili tupate maendeleo makubwa, na ili serikali iweze kutekeleza majukumu makubwa yaliyo mbele yake. Tunahitaji sisi raia wema sote tushirikiane kwa pamoja na kuiunga mkono serikali yetu, na kwa nia njema kila mmoja mahala alipo kutekeleza jukumu lake ili tuisaidie nchi yetu kupiga hatua kwa haraka.

Mhe. Spika, sina shaka yoyote kwa namna ambavyo hotuba imeeleza na kufafanua, yamo mambo ya msingi ya kuleta mabadiliko makubwa kwa Zanzibar. Zanzibar ambayo ina kila matarajio kwamba itapiga hatua kubwa sana na hotuba hii imegusa sana maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa, hapana shaka yoyote mafanikio yapo. Lakini misingi ya yote ni amani na utulivu wa nchi yetu.

Nataka nichukuwe fursa Mhe. Spika, nivipongeze sana vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, vya Jamhuri ya Muungano na vya Zanzibar, kwa mashirikiano makubwa na kwa kazi kubwa waliyofanya katika muda wote wa kipindi cha uchaguzi, kabla na baada ya hapo, kwa namna ambavyo wamesimamia usalama wetu, amani yetu na utulivu wetu. Kwa kweli hatuna budi kuwapongeza majemedari hawa kwa imani kubwa waliyoionesha katika kuitetea nchi yao na kuilinda nchi yao, Mwenyezi Mungu awasaidie na awape moyo zaidi wa kuitumikia nchi yao na manufaa zaidi yatakuwa juu yao, maana mcheza kwao hutunzwa.

Mhe. Spika, maendeleo yote yanahitaji amani na utulivu wa nchi. Rasilimali pekee kwetu sisi Wazanzibari ni kuhakikisha amani, utulivu, umoja na upendo ndio msingi wa mafanikio yetu. Tutakapoweza kuyakamilisha hayo kivitendo na kusahau tofauti zetu za kisiasa, hapana shaka yoyote Mhe. Spika, mafanikio makubwa katika nchi yetu yatafikiwa. Hivi sasa tayari tumeoneshwa kupitia hotuba hii mwelekeo mkubwa wa mashirikiano kati ya serikali na sekta binafsi, sekta ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, nataka nichukuwe fursa hii kuipongeza sana sekta binafsi kwa namna inavyoshiriki katika kujenga uchumi wetu na katika kutoa huduma za jamii, ili iendelee kutekeleza hayo kwa misingi ya uadilifu na kufuata taratibu na sheria za nchi, ili sote tusimame na kamba ya kufuata sheria za nchi yetu. Kwa kuwa tayari Mhe. Rais

ameeleza namna ambavyo amelenga kushirikiana na sekta binafsi katika kukuza uchumi, biashara, utalii, uwekezaji, kilimo, viwanda, ufugaji, uvuvi na kadhalika. Hapana shaka yoyote sote kwa pamoja tukishirikiana basi mafanikio makubwa katika nchi yetu yatapatikana.

Kwa hivyo, kinachotakiwa sote kwa pamoja sasa tujitayarishe upya namna ya kufanyakazi, ili kuleta mabadiliko. Lakini naomba nizungumzie sana kuhusu suala la vijana na ajira, hivyo ninaomba sana ndugu pamoja na vijana wetu wawe na tabia ya kujikubalisha kufanyakazi ambazo wanaweza kuzibuni wenyewe, kazi ambazo ni za ujarisiamali ikiwemo kilimo, uvuvi, viwanda vidogo vidogo, biashara ndogo ndogo pamoja na kazi zote za uzalishajimali. Kwa kweli, naona kuna mipango mizuri ambayo imeandaliwa na serikali kwa ajili ya kuwawezesha wananchi wetu hao kwa lengo la kujitegemea na kufanya shughuli muhimu za uzalishajimali, ili kuongezea pato la taifa.

Mhe. Spika, sina shaka yoyote hasa nikiona kwamba kuna skuli ama vyuo maalum vya amali ambavyo vimeanzishwa na pia vyengine vinategemea kuanzishwa na kujengwa Unguja na Pemba kwa dhamira ya kutoa mafunzo kwa vijana wetu, ili waweze kuelewa namna bora ya kuzalisha mali kwa ajili ya kupata mafanikio makubwa katika shughuli zao za maisha.

Kwa hivyo, jambo la msingi kwa vijana ninalowaomba ni kwamba wawe watulivu pamoja na wastahamilivu wakiiamini serikali yao tutawafanyia mambo mazuri ambayo yatajenga mustakbali mwema wao na wa nchi hii. Shughuli yoyote ambayo itasababisha kuhatarisha amani ya nchi yetu ama maelewano yetu au umoja wetu, basi haiwasaidii vijana wetu na wala sisi tuliozaidi ya vijana na hata wazee wetu.

Kwa maana hiyo, jambo la msingi la nchi yetu ni kwamba tuendelee kumuamini sana Mhe. Rais wetu na dhamira yake njema aliyonayo ya kutaka kuleta mabadiliko makubwa katika nchi hii. Mhe. Spika, tunawaomba sana vijana pamoja na wananchi wote wa Zanzibar, isipokuwa tuendelee kumuamini Rais wetu, tuyaamini aliyoyaeleza katika hotuba hii na iwe kigezo na dira cha maendeleo ya nchi yetu kwa miaka mitano. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwangu mimi kubwa ni kutoa shukurani pamoja na kuwaomba wananchi wote wa Zanzibar waendelee kuwa wavumilivu na wenye subira katika kipindi hiki ambacho Mhe. Rais wetu yuko tayari katika kuleta mabadiliko makubwa katika nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo nakushukuru pamoja na Wazanzibari wote kwa kupata fursa hii ya kuitumikia nchi yangu. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, ahsante. Sasa naomba nichukue nafasi hii kwa heshima kabisa nimwite Mhe. Hamad Rashid Mohammed ambaye atafuatiwa na Mhe. Juma Ali Khatib na Mhe. Machano Othman Said ajiandae. *(Makofi)*

Mhe. Hamad Rashid Mohammed: Mhe. Spika, kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na utukufu kwa kutujaalia katika mikikimikiki yote ya kisiasa leo tupo hapa tayari kwa kuwatumikia Wazanzibari na Watanzania kwa jumla. *(Makofi)*

Pili, nimshukuru sana Rais kwa heshima aliyonipa mimi pamoja na wenzangu aliotuteua ni utashi wake na wala halazimishwi na mtu yeyote, angeweza kabisa kuteua wajumbe wengine wanane wa CCM na hakuna lolote litakalotokea. Lakini ni kwa sababu amethamini mchango wetu katika taifa, kuwatumikia watu pamoja na uwezo wetu katika kufanya kazi hizo. Kwa kweli, tuna kila sababu ya kumshukuru kwa uteuzi wake na sisi kubwa tunalokuahidi na wenzangu watapata fursa ya kusema ni kutoa ushirikiano wa hali ya juu kabisa kwa madhumuni ya kuwatumikia Watanzania pamoja na Wazanzibari. *(Makofi)*

Mhe. Spika, bahati nzuri katika maisha yangu nimepata bahati ya kufanyakazi katika mfumo wa chama kimoja. Tulikuwa na Bunge kama hili ambalo lilikuwa la chama kimoja. Lakini nilichojifunza wakati huo ilikuwa Bunge ni kwamba serikali ni serikali na wabunge wengine ni *backbenchers* au *opposition*, ndio *almost* inafanana na taswira tuliyonayo hapa. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, jambo letu la kwanza ni kumuomba Mhe. Rais serikali atakayoiunda ajue huku ndani kuna *backbenchers* na ni *opposition* kwa maana ya kuisimamia serikali. *(Makofi)*

Nawashukuru sana msemaji wa kwanza aliliweka wazi hilo kwamba Baraza hili litajitahidi kadri ya uwezo wake kufanya kazi yake ya kikatiba, ili kuhakikisha kabisa linawatumikia Wazanzibari wote bila ya ubaguzi wa aina yoyote, ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Jambo la tatu, jana Mhe. Rais alifanya kazi kubwa sana kwa kutoa hotuba nzuri sana, lakini hotuba ni jambo moja na utekelezaji ni jambo la pili. Kwa kweli, sisi sote tunao wajibu mkubwa sana wa kuona ni namna gani tutaisaidia serikali, tutawasaidia wananchi katika kusimamia haya yaliyosemwa mazuri sana yaliyomo ndani ya kitabu cha hotuba ya Mhe. Rais, yaliomo katika *Vision* 2020 pamoja na *manifesto* nyengine za vyama ambavyo ninahakika kabisa pamoja na ushahidi Mhe. Rais anasema lile zuri analichukua na amelichukua na tumeyaona humu ndani yamo. Mhe. Spika, nasema ni uzalendo wa hali ya juu alioutumia, isipokuwa tunahitaji kujipanga katika kutekeleza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, yote haya yaliyosemwa kwanza lazima tujielewe kwamba tunajenga uchumi wa aina gani Zanzibar, kwa sababu uchumi wetu sisi kwa wataalamu wa uchumi waliobobea akina Mhe. Amina Salum Ali wanaita *service economy*. Sasa uchumi ambao unatoa huduma unahitaji uwe na watu ambao uwezo wao wa kutenda ni wa mia kwa mia. Kwa mfano, hiyo tunayoisifia Singapore pamoja na wengine ni kwa sababu ya utendaji wao ni wa hali ya juu sana, kila mmoja anaweka siasa mbali na utendaji mbali, bado tunalo tatizo la kufanya siasa kwa kila kitu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, juzi nilimsikia kiongozi mmoja akisema ni vizuri watu waendelee kugomeana wasizikane na wala wasisaidiane, kwanza si imani, si uislamu na wala sio dini yoyote hata utu haupo. Sasa katika hali hiyo hamuwezi kupata maendeleo katika mazingira hayo, na wala hamuwezi kujenga uchumi ambao unahitaji kutoa huduma wakati huduma zenyewe watu wengine wanazigomea na hawapati ushirikiano, hivyo lazima hili tulisimamie kwa nguvu zetu zote. *(Makofi)*

Kwa mfano, unakwenda kuuza karafuu kwa sababu unatoka chama chengine, mtu anasema tumpunje kidogo kwa sababu hayupo kwenye chama chetu tutoe kwa sababu ya siasa tu. Kwa kweli hii ni kasoro moja kubwa tuliyonayo Zanzibar na lazima kama viongozi tujielekeze kuondokana na siasa na uchumi uweke pembeni tufanye kazi, ili wananchi wapate maendeleo. *(Makofi)*

Sasa, ili tulitekeleze hili kuna jambo moja la msingi sana lazima tulifanye na tukubali kupambana nalo wataalamu wanaita *law enforcement*, kwamba yeyote anayevunja sheria tusimtizame kwa rangi au sura yake isipokuwa achukuliwe hatua *immediately* ndipo tutapata mafanikio haya. *(Makofi)*

Kwa kweli, suala la *law enforcement* ni jambo ambalo limetukwamisha katika maendeleo yetu yote. Kwa mfano, sehemu inapita umeme unaambiwa nyumba hii ibomolewe na mtu analipwa *compensation* mtu haondoki na wala hakuna mtu anaweza ku-*exercise* kutumia nguvu zake za kisheria na kumuondoa, matokeo yake tunakwama kimaendeleo. Kwa hivyo, suala la *law enforcement* lazima tulisimamie kwa nguvu zetu zote, na tukilipuuza hilo basi tutakwama na tutarudi tena kwenye nyumba hii na kulaumiana. Mhe. Spika, tumepitisha sheria hapa hivyo kila mmoja awajibike kwa nafasi yake sheria ile inapomtaka asimamie. *(Makofi)*

Mhe. Spika, unapojenga uchumi wa aina hii ni lazima uhakikishe rasilimali zilizopo zinatumika kikamilifu. Kwa bahati mbaya tusijione ni masikini, lakini sisi ni matajiri sana, isipokuwa bado hatujatumia rasilimali zetu vizuri na Mhe. Rais wa Zanzibar jana amezieleza vizuri rasimali zilizopo na tulikuwa tunatoa mifano sana sisi.

Kwa mfano, kwa uvuvi wa bahari tu kuna rasilimali za kutosha za kupata kuendelea, lakini huwezi rasilimali hii kuifanyia vizuri kama huna taasisi za fedha zilizokuwa tayari kuendeleza hizi taasisi na ndio maana maneno hayo yote tumeyazungumza na hata huko Bara wameyazungumza, lakini hakuna taasisi iliyokubali kumsaidia mvuvi yeyote kumkopesha, nendeni mukafanye utafiti.

Mhe. Spika, ukienda kwa mvuvi atasema sekta hii sisi tuna wasiwasi nayo, nataka kuagizia meli, atakwambia hii meli inaweza ikapotea huko baharini na wala hakupi fedha, sasa huwezi kuendeleza taasisi yoyote bila ya kuwa na taasisi ya fedha ambayo iko tayari kuangalia mazingira yenu ya uchumi na kuweza kuwakopesha watu. Lakini,

taasisi zetu zote hizi wanawakopesha akina Mhe. Mohammedraza kwa sababu wanafanya biashara na hawataki kwenye *investment*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nafikiri Mhe. Waziri wetu wa fedha atakapoingia jambo la kwanza aangalie hizi taasisi ambazo tunazo, *People's Bank of Zanzibar* pamoja na taasisi nyengine za fedha kwa kiasi gani ziko tayari kusaidia kukuza uchumi kwa maana ya watu kuwapatia mikopo nafuu kwa ajili ya kuweza kujiendeleza, bila ya hilo tutarudi tena kwenye nyumba hii hakuna lolote litakalofanyika. Kwa kweli, hakuna biashara, wala *investment* bila ya mitaji. Mhe. Spika, nasema hotuba ni nzuri sana, lakini lazima tukaliangalie hilo kwamba litafanyika na lipo na litusaidie kutuondoa tulipo.

Jambo la tatu, ili ufanye vizuri lazima uwe na watu walioelimika na ambao wako tayari kulielimisha. Kwa bahati mbaya sana, nenda kwenye taasisi zetu za taaluma nimesikiliza hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar vizuri sana, kwamba tunasema tunakwenda kuanzisha vyuo vyengine pamoja na kujenga vyuo vya ghorofa, je kwenye taasisi hizo kuna walimu wazuri, vitabu. Sasa leo unakwenda kujenga taasisi nyengine ya taaluma lakini ile iliopo haina vifaa vya kutosha.

Mhe. Spika, jambo la kwanza la kufanya ni kuchukua takwimu hichi tulichonacho je, tumekifikisha hapa kilipo . Kwa mfano, kama ni kiwanda cha matrekta usijenge kipya katizame kilichopo je, kina wataalamu wa kutosha, vifaa vya kutosha na halafu wale watu waambiwe sasa nakukabidhini mukivunja hilo sisi tutakushtaki, basi huyo unaweza kumshtaki na wala tusijetukapambana na kushtakiana kumbe mtu hukumpa zana za kufanyia kazi, hana wataalamu wala taaluma ya kufanyia kazi na hili nalo ni jambo la msingi sana katika kuendeleza uchumi na bila ya kufanya hilo tutarudi tena katika nyumba hii na kulaumiana.

Jambo jengine ambalo ni la msingi sana ni kuhusu makusanyo ya mapato. Mhe. Spika, ukipitia takwimu za Zanzibar hapa misamaha ya kodi inashinda hata *revenue*. Kwa kweli, huwezi ukaendesha nchi bila ya kuwa na mapato, kwa sababu mapato unayoyapata halafu unayasamehe, matokeo yake watu wetu wote wamejazwa fikra za misaada na mikopo, yaani ukipita huko njiani, Marekani amezuia misaada basi wewe unalia utakufa njaa, amekwambia nani utakufa njaa, ni *mindset*! *(Makofi)*

Mhe. Spika, misaada duniani kote inakotoka hawa wanaoahidi hawatoi zaidi ya asilimia 26 au 27, kaangalie *commitment*s wanazotoa na kwa kiasi gani wanatoa, utakuta ina asilimia 25 au 26 ama 27. Hizo wamekuahidi na hizo unazozipata *check list*, yaani ule utaratibu wa kukwambia fedha hizi zitoke kila siku inabadilika. Mfano, mzuri nakumbuka wakati mmoja tulikuwa kwenye Kamati ya Bajeti wakaja wakubwa hawa wanaotoa fedha wakaja na *check list* ya kwanza, basi nikawauliza *check list* ya pili munayo au itakuja siku nyengine. Kwa maana hiyo, ile ya kwanza muna-*tick* hiki tumekubali na hiki tumekubali na wakija siku ya pili wanakuja na *check list* nyengine na mwisho wanakwambieni muowane wanaume kwa wanaume, inahusu nini na msaada. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kwanza wanaomba Wazanzibari wote tuondokane na fikra za kutegemea misaada kwamba ndio itaendesha Zanzibar hakuna na wala musishangirie au kufurahia fulani amezuia msaada, lakini mimi nasema akizuia msaada anakusaidia kujenga uchumi wake. Kwa mfano, ndugu zetu Kenya hapo walizuiwa msaada na waliteremka kutoka asilimia 33 mpaka asilimia tano (5) kutegemea msaada walijibana wenyewe na kufanya kazi, na leo Kenya hawana shida ukimpa msaada sawa na kama hukumpa anaendelea. *(Makofi)*

Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar jana alisema hivyo kwamba tutatumia rasilimali zetu sisi wenyewe na anayetaka kutusaidia aje na wala hatumkatazi. Lakini tusijenge mawazo na fikra kwamba sisi hatuwezi kuishi eti kwa sababu msaada wa Marekani au wa nani, potelea mbali, kwa sababu sisi tunaishi kwa rehma za Mwenyezi Mungu aliyetuumba na kutupa uhai wake. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, tutaishi kwa kutumia rasilimali zetu tulizonazo, rasilimali watu na zile nyengine ambazo Mwenyezi Mungu ametupa, tukizitumia vizuri tutaishi vizuri bila ya wasi wasi wowote na bahati nzuri tunazo nyingi, tuna gesi na mafuta kesho.

Mhe. Spika, ombi langu tusijetukapata *Dutch disease*, kwamba Wa-*Dutch* walipogundua mafuta waliacha kilimo na kila kitu, wakati mafuta na gesi yalipoteremka bei wakaanza kulala na njaa. Sasa na sisi bahati nzuri ile sheria ilipitishwa kwenye Bunge na itakapokuja hapa nafikiria inakuwa ni *same thing*, kwamba itatenga mapato ya mafuta

na kwa kiasi gani mapato hayo yaje yasaidie kwenye bajeti ya serikali, ili mapato ya ziada yaje yasaidie vizazi vinavyokuja mbele ya safari.

Kwa maana hiyo, tukifanya hivyo tutaendeleza kilimo chetu, ufugaji wetu pamoja na uvuvi wetu bila ya kutegemea zaidi mafuta na iwe ni rasilimali ya kuwasaidia watu wetu mbele ya safari, basi tukifanya hivyo tutafanya vizuri. Kwa sababu rasilimali tunazo; tunao watu lakini bado hawajapata taaluma ya kutosha ya kuweza kusimamia uchumi, tunazo rasilimali bado hatujaweka *investment* vizuri kwa ajili ya kusimamia uchumi na bahati mbaya wawekezaji wetu wote wa ndani wanafanya biashara hawawekezi.

Sasa kazi yetu moja kubwa ni kuwaita wafanyabiashara wenzetu tuwawezeshe wawekeze na Mhe. Rais wa Zanzibar jana alisema vizuri, kwamba tuanze kuekeza angalau kwenye viwanda vidogo vidogo, vya kati na ikiwezekana twende kwenye viwanda vikubwa, lakini bila ya kuwa na *proper plan* ya hiyo, basi hotuba hii tutakuja miaka tutajisifu kwa mambo ya jumla jumla, lakini hakuna cha maana kilichofanyika.

Jambo la tano Mhe. Spika, ni uwajibikaji na tumelizungumza sana suala hili. Kwa kweli, kuna maeneo ambayo mtu hatakiwi jambo lolote, ni kwamba amekuja kutaka huduma tu, lakini unao uwezo wa kummalizia muda huo huo na unamwambia njoo kesho.

Kwa mfano, wenzetu Ghana wamefanya jambo moja zuri na naiomba serikali inayokuja ijitahidi kuliangalia hilo, kwamba mtu yeyote anayekwenda afisini, kuna fomu maalum anapewa anajaza kwamba wewe unakuja afisini unashida gani, inaelezwa shida yake anambiwa mtu fulani ndiye atakayeshughulikia shida yako na tarehe fulani, saa fulani njoo uchukue majibu na kama hutaki kuja basi tunakuletea kwenye *email* mwenyewe ukipenda. Nimekuta Ghana na wala hakuna foleni ya pahala. Lakini hakuna mtu anasumbuka kwa kupata huduma, lakini nenda leo hapa!

Mhe. Spika, nimeleta mradi mmoja wa ndege na Wachina wameleta *MOU* na huu ni mwezi wa tano bado hatujasaini *MOU* tu, wakati *MOU* karatasi zenyewe ni tano tu na kubwa linalosemwa muturuhusu sasa tufanye utafiti, ili hatimaye tukubaliane tuanzishe shirika au lisianzishwe basi na huu ni mwezi wa tano, halafu munasema munataka kukuza uchumi, munakuzaje uchumi namna hii! *(Makofi)*

Kwa hiyo, suala la kuwajibika ni la msingi sana na *time frame* ya kuwajibika, kwamba tumekubaliana saa fulani jambo limalizike, basi limalizike kwa wakati tuliopanga na kama hakuna hiyo, itakuwa tunadanganyana bure tu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nashukuru sana Baraza lako hili saa tatu ni dua na wala hatujamkuta Spika kuja saa tatu na dakika tano hapa, isipokuwa saa tatu kamili amesimama pale anasoma dua, utachelewa wewe lakini yeye hachelewi, tunataka tuwe namna hiyo. Hivyo, ni lazima tujifunze kuheshimu wakati pamoja na kutumia wakati, yaani kuthamini wakati wa mtu, kama mwenzako amesafiri amekuja anataka majibu unamwambia bwana mkubwa amekwenda kwenye mkutano hayupo, haya haya yakiondoka watu watapata huduma na huduma zitakuwa nzuri.

Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Mohammed Aboud alizungumzia sana amani na utulivu, bila ya amani na utulivu hakuna maendeleo yoyote. Tunavishukuru sana vyombo vya ulinzi na usalama, vimefanya kazi hiyo na viendelee kufanya kazi hiyo, lakini niwaombe sana wananchi tuache utaratibu wa kuchukua sheria mikononi mwetu wakati mwengine unavilazimisha vyombo vya ulinzi kutumia nguvu kwa sababu wewe umeanza kutumia mkono wako, kama fulani kakosa nenda karipoti na hatua zitachukuliwa.

Kwa hivyo nasema vyombo vinafanya kazi yake vizuri na sisi kama raia tunahitaji vile vile tuheshimu sheria na utaratibu wa sheria pale ambapo tutatumia nguvu nje ya utaratibu wa kisheria nguvu zikitumika msiseme haki za binaadamu zinavunjwa, ni kosa kabisa kabisa na hili ndio watu wanalolitegemea sana, anafanya halafu anasingizia *Human Right Violation*, tuachane na hilo kabisa tuheshimu sheria ndio nchi hii itatulia. Uchaguzi umeisha tuendelee na kazi, tupendane, tusaidiane, tuongoje 2020 ili tuingie kwenye uchaguzi mwengine. *(Makofi)*

Mhe. Spika, watu wetu ni masikini sana kiwango cha walionacho na wasionacho kinapanuka kila siku na kinapanuka kwa sababu ajira bado hazijakuwa za kutosha na jana nashukuru sana Mhe. Rais ameliona hilo, amelizungumza vizuri…..

Mhe. Spika: Mhe. Hamad Rashid umebakiza dakika tatu.

Mhe. Hamad Rashid Mohammed: Dakika tatu, nakushukuru sana Mhe. Spika, sasa dakika zangu tatu Mhe. Spika, naomba kwanza nikishukuru sana chama changu cha ADC, kwa kunipa heshima kubwa sana ya kuweza kuwa mgombea wa Urais, kwa bahati mbaya kura hazikutosha nikategemea nitapata nafasi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kura nazo hazikutosha, lakini Rais akazithamini juhudi hizo na akaniteua kuwa Muwakilishi.*(Makofi).*

Naomba niwaahidi wana ADC popote walipo kama kawaida yangu nitaendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote, kutumia taaluma yote na uzoefu wote nilionao, kujenga chama ambacho madhumuni yake ni moja tu, kushika dola. Na dola inashikwa kwa kupitia uchaguzi haishikwi kwa kwenda Kibanda Maiti na ndio maana tukaamua kushiriki katika uchaguzi, kwa sababu hakukuwa na njia nyengine isipokuwa tushiriki uchaguzi, ili tupate nafasi tulizopata. Tunawashukuru sana waendelee wananchi wote wa Tanzania kutuunga mkono na sisi tutaendelea kupambana katika mazingira ambayo ni ya kidemokrasia kabisa na hatutorudi nyuma katika hilo Mhe. Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Juma Ali Khatib: Ahsante Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa leo tukiwa katika hali ya afya njema na wazima, na napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuniamini na kuniteua kuwa mmoja katika Wawakilishi katika nafasi zake kumi, ametumia busara na hekima na ameonesha kwamba yeye ni Rais wa vyama vyote vya siasa. Na hata wale waliokuwa hawana vyama vya siasa pia ni Rais wetu sote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka kusema tumemaliza uchaguzi sasa hivi tufanye kazi sote, tuna kila haja na sababu ya kushirikiana ya kujenga nchi yetu sisi sote ni wamoja, sisi sote ni Watanzania na Wazanzibari tunatakiwa tushirikiane tuinyanyue nchi yetu, tuisaidie Serikali yetu, yale malengo yaliyotegemewa tuyafikie. Napenda kumshukuru Mke wangu Bi. Amrat kwa kunipa ushauri mzuri sana, napenda kuwashukuru viongozi wa chama changu cha TADEA kwa kushirikiana nao na kufanya kazi kwa uzalendo wa nchi yetu na leo kufanya kwamba mimi nikawa mmoja katika Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi nataka kusema kwamba hotuba ya Mhe. Rais aliyoitoa jana katika ufunguzi wa Baraza letu tukufu la Wawakilishi hii iwe ndio dira ya maendeleo ya nchi yetu ya Zanzibar hususan kwa hawa Mawaziri watakaochaguliwa muda wowote kutoka sasa, hata sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tukitumia hutuba ya Mhe. Rais tutapata vitendea kazi vizuri, kwa sababu kuna mambo mengi mule ambayo Mhe. Rais amegusia na mimi nataka nizungumze kidogo.

Mhe. Rais alizungumzia sekta ya utalii; kwanza nampongeza pale aliposema kwamba kile Chuo cha Utalii cha Maruhubi sasa kitaunganishwa na Chuo Kikuu cha Zanzibar, tukifanya hivi tutaweza kuwafanya vijana wetu tuwe na wanafunzi wazuri wenye elimu ya juu na wawe wabunifu zaidi hasa tukizingatia kwamba Zanzibar tunategemea sana sekta ya utalii na Zanzibar ni kivutio duniani cha mambo ya utalii.

Mhe. Spika, ukichungaza utakuta kuna matajiri wakubwa sana wanatoka nje kama Marekani, Uingereza, Canada wanakuja Zanzibar kimya kimya, hata ukiangalia wafanya biashara wakubwa mashuhuri wanakuja Zanzibar. Kwa hivyo sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuna kila haja na sababu ya kuboresha ile hotuba ya Mhe. Rais, kwa kutia nyama na kutia vionjo ili sasa kuhamasisha hii sekta ya utalii ikawa kubwa zaidi na ikawa na tija zaidi na tukaendana na mfumo wa kisasa.

Mhe. Rais alizungumzia sekta ya utalii kwa kujenga mahoteli, hotuba hii ilikuwa ni nzuri unaposema kwamba utajenga mahoteli kwanza ni kupanua wigo wa ajira kwa vijana, ni kupanua wigo kwa wafanya biashara. Kuna watu wengi wataneemeka kwa sekta hii ya utalii, tunapojenga hoteli kubwa za kisasa za nyota tano na kadhalika hapo uchumi wetu itakuwa tumeunyanyua na lile tatizo kubwa ajira kwa vijana litakuwa limepatiwa dawa. Jana tumeona katika hotuba ya Mhe. Rais, imeeleza jinsi gani vijana waliopata ajira, si chini ya vijana elfu tano katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na taasisi binafsi karibu elfu ishirini na tano, kwa hivyo hili ni jambo jema na jambo zuri.

Pia kuna sekta ya viwanda katika kukuza uchumi, tuna kila sababu ya kuweka viwanda. Mimi nilikuwa mmoja katika wafanyakazi wa viwanda vidogo vidogo hapa Zanzibar, nataka kusema kwamba Zanzibar tulikuwa tuna kiwanda cha umeme, tunatoa waya bora kwa Afrika nzima, tulikuwa tuna wataalam wazuri, tulikuwa tunatoa vifaa

vizuri na mashine nzuri, vitendea kazi vizuri na wakati ule ulikuwa ukitaka waya mzuri basi ni ule waya unaotoka Zanzibar. Kwa hivyo ni vizuri sasa tukazingatia kama kuna haja sasa ya kufanya kila njia tukafufua hivi viwanda kwa ajili ya kupata tija kwa sababu kila siku tunakusudia sasa kufanya ujenzi, unapofanya ujenzi kama ukitengeneza vifaa vya ujenzi vipatikane hapa hapa ndani, utakuwa na unafuu kwa wananchi katika kujenga. Kutakuwa na unafuu hata kwa wafanya biashara sasa kuchukua vifaa kwenda kuuza sehemu za nje, tukifanya hivi Mhe. Spika, uchumi wetu utanyanyuka na utaimarika.

Tulikuwa na kiwanda cha kutengeneza mafuta; tulikuwa na kiwanda cha kutengeneza samli, tulikuwa na kiwanda cha kutengeneza vyombo, tulikuwa na kiwanda cha kutengeneza nepi za watoto, fulana na taula n.k.. Kwa hivyo tukizingatia hotuba hii ya Rais basi tunaweza tukakaa kwa pamoja tukatafuta mbinu mbali mbali mbadala za kuhakikisha kwanza kuangalia je, namna gani tunaweza kufufua hivi viwanda vyetu ili kupata yale malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Spika, pia jambo jengine hapa tulikuwa na kiwanda cha ngozi, kiwanda cha viatu kwa hivyo tunajua kwamba Zanzibar tunakula nyama sana, ng'ombe wanachinjwa sana, kwa hivyo hii sasa ni kuweza kuwafanya wale wachinjaji wa ng'ombe wakaweza kupeleka hizi ngozi hapa hapa na zikafanyiwa kazi tukaweza kutengeneza viatu. Tuna viokosi vya SMZ wakaweza kutengenezewa viatu, tuna wananchi mbali mbali wakaweza kutengenezewa viatu, ajira itakuwa kubwa zaidi na hata bei ya kiatu itapungua. Tutaweza kutoa vitu vingi sana kwenda kuuza nje, tutanyanyua uchumi wetu, tutaongeza mapato ya Serikali kwa kupata pesa za kigeni.

Mhe. Spika, vile vile mimi nataka kusema jambo moja; amesema Mhe. Hamad hapa na Mhe. Hamza nafikiri aliligusia, hili suala lililoko sasa kwamba kuna baadhi ya nchi zinajaribu kutaka kutikisa zile nchi wanazoziona wao ni ndogo, mimi nataka kusema kwamba Zanzibar ni nchi yetu sote na tumeshapata uhuru, tusikubali itokezee nchi mmoja ijione kwamba wao ni taifa kubwa wajaribu kutaka kututisha tisha, lazima tushikamane sasa tukamatane mikono tujenge nchi yetu. Sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunahitaji sasa tutoe elimu ya uraia kwa wale wapiga kura wetu, kwa sababu inaonekana bado kuna watu hawana elimu ya uzalendo, leo kuna watu wanafurahi wanaposikia kwamba labda kuna taasisi fulani itaondoa msaada kwa Zanzibar. Kusema kweli ni jambo la kuwasikitikia wale ambao kwa namna moja au nyengine wanahimiza eti Tanzania izuiliwe kupata misaada, hawa si watu wema wala si watu wazuri.

Mhe. Spika, tukumbuke China ilivyokuwa ilikuwa nchi masikini sana duniani lakini China waliweza kukaa pamoja wakashikamana, wakafanya kazi kwa bidii na leo China ni taifa kubwa sana Duniani. China sasa inatoa misaada, tunaweza kusema kwamba uchumi wake uko juu sana. Kwa hivyo na sisi sasa kupitia hotuba ya Mhe. Rais jana basi tushikamane tujenge nchi yetu tuwe wamoja tufanye kazi kwa bidii. Wale watakaobahatika kuchaguliwa kuwa Mawaziri basi waweke uzalendo mbele zaidi, na wafanye kazi kwa uadilifu ili kulipia kodi, tuweze kuvuka hapa na lengo letu lifikiwe.

Mimi nataka kuwapa moyo wananchi kwamba tusidanganyike, hatuna pengine pa kwenda zaidi ya Zanzibar. La kufanya na nikushirikiana na Serikali yetu iliyo madarakani kwa lengo la kuondoa matatizo ya mwananchi mmoja mmoja. Tunajua kuna watu walioko vijijini wana shida nyingi sana, kuna watu wanapata matatizo ya afya, kinamama na watoto, kuna watu uchumi wao uko chini kabisa, maisha magumu kabisa. Sasa dawa ya mambo haya ni kufanya kazi kwa bidii tukashirikiana na Serikali iliyokuwepo madarakani. Tumemaliza uchaguzi, tumemaliza kampeni, sasa hivi tufanye kazi, tusaidie watu wetu, ahsante Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia amani katika nchi yetu, lakini pia kutupa uhai na kuweza kuja hapa katika Baraza letu tukufu la Wawakilishi.

Pili Mhe. Spika, naomba nikupongeze sana kwa ushindi wa kishindo uliopata katika uchaguzi wa Spika, pamoja na Naibu wako Spika, na wenyeviti wetu wa baraza. Aidha nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Mhe. Rais wetu wa Zanzibar kwa ushindi wa kishindo wa asilimia 91.4 alioupata katika uchaguzi mkuu wa tarehe 20 Machi, 2016. Ushindi wa Mhe. Rais ni ushindi wa CCM kwa hivyo hatuna budi wana CCM wenzake kumpongeza na kusherehekea kwa ushindi huu. Lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kuteuliwa tena kuendelea na nafasi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, jana Mhe. Rais alikuja kutuzindulia Baraza letu rasmi na katika uzinduzi wake amezungumza mambo mengi sana, muelekeo wa Serikali awamu ya saba kipindi chake cha pili na haya mambo aliyozungumza Mhe. Rais uhakika tukiyajadili kwa kina kuyafanyia kazi basi tija kwa wananchi wa Zanzibar itakuwepo.

Pia nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa jimbo la Mfenesini kwa kunichagua kuwa muwakilishi wao kwa mwaka 2015 mpaka 2020, uchaguzi umepita na wamefanya kazi nzuri na mimi nawaahidi kufanya kazi nzuri katika shughuli zetu za maendeleo.

Pia nichukue nafasi hii kuwashukuru na kuwaaga rasmi wananchi wa Jimbo la Chumbuni ambao nimefanya nao kazi kwa vipindi vitatu kama muwakilishi wao, nasema asanteni sana. Tulifanya kazi pamoja na bahati nzuri haiko wazi nafasi, yuko Muwakilishi mwengine Mhe. Miraji, ni matarajio yangu kwamba atashirikiana nao wananchi, atafanya nao kazi vizuri, atawaletea maendeleo kwa pamoja ili nchi yetu isonge mbele.

Mhe. Spika, kitabu cha Mhe. Rais jana kimezungumzia shughuli za maendeleo, shughuli za ustawi wa jamii na shughuli za kisekta, lakini kwa ujumla katika miaka mitano ya kwanza ya Mhe. Rais amejitahidi sana kuleta maendeleo katika nchi yetu. Amejenga sana mambo ya miundombinu, amesaidia sana shughuli za jamii kama sekta ya afya na sekta nyengine. Kwa hivyo ni matarajio yetu kwamba katika awamu ya pili uongozi wake kama alivyoahidi jana kwenye hotuba yake, shughuli hizi zitashika kasi na zitakwenda kwa vizuri zaidi kwa manufaa na maslahi ya wananchi wa Zanzibar na maslahi ya wanachama wote wa Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Spika, waheshimiwa wengi wamezungumza hotuba hii ya Mhe. Rais, kila mmoja kazungumza kwa ufasaha, kazungumza kwa umahiri na kila mmoja alikwenda katika sehemu ambayo aliiona yeye inafaa lakini ukiangalia kitabu cha Mhe. Rais kabla ya kuzungumzia sekta moja moja alizungumzia mambo ya jumla, miongoni mwao ni utawala bora na utawala bora ni neno pana sana.

Mhe. Spika, tumemaliza uchaguzi kwa bahati mbaya tulifanya uchaguzi tarehe 25 Oktoba lakini ukawa na figisu figisu nyingi na ukaharibika, kwa bahati nzuri Mwenyekiti wa Tume Ndugu Jecha akatutangazia kwamba uchaguzi ule umefutwa na akatutangazia tarehe ya kurejea uchaguzi tarehe 20 Machi. Chama cha Mapinduzi kimeshinda vizuri sana Unguja na Pemba, tumeshinda kwa kishindo, ni matarajio yetu kwamba hawa ambao tumeshindana nao au vyama vya siasa vitakubali kwamba uchaguzi umeisha na jana Mhe. Rais katwambia hakuna uchaguzi mwengine mpaka 2020. Kwa hivyo wale ambao wanafikiria kwamba April 25 kuna uchaguzi, nafikiri waamke wafanye kazi tushirikiane kujenga nchi yetu, hakuna jambo jengine zaidi isipokuwa kujenga nchi.

Bahati nzuri uchaguzi wa tarehe 20 ulikuwa wa amani sana, ulikuwa wa haki sana na ulikuwa na fursa kwa kila mgombea na kwa kila chama kushiriki bila ya kubughudhiwa na nafasi ile Chama cha Mapinduzi tumeitumia vizuri sana na tukashinda vizuri sana, kwa hivyo katika utawala bora lazima kuna kushinda na kushindwa, wale walioshindwa wakubali kwamba uchaguzi umepita na sasa washirikiane na chama cha Mapinduzi kujenga Zanzibar yetu mpya. Nimshukuru Mhe. Rais kwamba jana katika hotuba yake alizungumzia kwamba yeye kama Mhe. Rais ama kama kiongozi wa Zanzibar hatokuwa mbaguzi wa dini, hatokuwa mbaguzi wa jinsia, hatokuwa mbaguzi wa eneo na hatokuwa mbaguzi wa kisiasa. Jana tu amedhihirisha kwamba yeye ni mkweli kwa yale ambayo anayazungumza. Jioni ya jana amechagua vyama vya upinzani kuingia Barazani, kachagua watu wa dini mbali mbali kuingia Barazani, kachagua watu wenye jinsia mbali mbali kuingia Barazani, hongera sana Mhe. Rais. (*Makofi*)

Matarajioa yetu kwamba wale ambao wameteuliwa na Mhe. Rais na sisi ambao tumeingia kwa milango mengine, kama jimbo na viti maalum tutashirikiana kwa pamoja kufanya kazi za Baraza la Wawakilishi, kuisaidia serikali yetu, lakini pia kuwasaidia wananchi wa Unguja na Pemba katika shughuli za maendeleo za kila siku. Maana tukiingia humu Baraza la Wawakilishi sote tunakuwa wawakilishi, hakuna mwakilishi bora, hakuna mwakilishi wa jimbo kwamba yeye ni bora au viti maalum au wa Rais. Sote humu tutakuwa sawa na tutafanya kazi za kujenga nchi yetu.

Mhe. Spika, jengine ninawashukuru nchi rafiki, watu wanasema rafiki yako atakutambua zaidi wakati wa shida. Kwa hivyo, mimi naomba niwashukuru zaidi nchi ya China baada ya uchaguzi tu walitoa tamko la kutuunga mkono kwamba wao walishuhudia uchaguzi ulikuwa wa haki na taratibu zote zilifanyika na wakamtambua Rais, na wametambua ushindi wa Chama cha Mapinduzi. Lakini pia tuwashukuru nchi ya India, Japan na hata Msumbiji nao

walikuwa bega kwa bega. Kwa ujumla nchi zote za Afrika na nchi za Asia zimetuunga mkono sana na tunatarajia hata hizo nchi za Ulaya baadae zitakaa na kuamua kwamba kweli uchaguzi ulikuwa wa haki na Zanzibar iendelee. Hata Marekani nasikia sio kwamba wamekata misaada yote bado ni *MCC* tu na mambo mengine yanazungumzika.

Mhe. Spika, nije katika sekta moja moja ambazo naona ni muhimu katika hotuba ya Mhe. Rais. Kwanza nianze na viwanda. Mhe. Spika, nchi yetu ya Zanzibar katika miaka ya 70 mpaka 80 tulikuwa na viwanda vingi kidogo, ingawa havikuwa viwanda vikubwa sana. Vilikuwa ni viwanda vya kati, Kiwanda cha Viatu, Kiwanda cha Sigara, Kiwanda cha Soda na baadae viwanda vidogo vidogo *COTEX* n*a BANCO*. Viwanda hivi vilichukua ajira ya wananchi wengi sana, lakini kwa mabadiliko ya kidunia ya uchumi kati kati ya miaka ya 90 viwanda hivi karibu kimoja baada ya kimoja vyote vilifungwa.

Kwa sababu kwanza uwezo wa soko ulikuwa ni mdogo, wizi ulikuwa mkubwa lakini na wafanyakazi walikuwa wengi. Kwa hivyo, ni matarajio baaada ya serikali hii ya awamu ya saba kufanya juhudi na tafiti mbali mbali na kuona umuhimu wa kuwepo viwanda, ni matarajio yangu kwamba tutaanza tena kuanzisha viwanda vya saizi ya kati na vidogo vidogo. Hii ni sehemu ambayo inaweza ikaleta ajira kwa vijana wengi sana, hata kama kiwanda kitachukua wafanyakazi 20,30,10 tukiwa na viwanda visivyopungua 50 basi watu wengi watakuwa wamepata ajira.

Pia itapunguza utegemezi wa kila bidhaa kutoka nje ya Zanzibar, uwezo wa kuzalisha bidhaa Zanzibar upo na tukasafirisha bidhaa bado masoko yapo. Kwa hivyo, ni matarajio yangu kwamba tutazalisha bidhaa ambazo zitakuwa na *brand* nzuri ya kusafirisha nje ya nchi. Lakini zaidi kama alivyosema Mhe. Rais tujielekeze katika viwanda vya uzalishaji wa mazao baharini vikiwemo vya samaki na mambo mengine. Zanzibar ni nchi ambayo imezungukwa na bahari kwa asilimia 100. Kwa hivyo, uwezekano wa kuanzisha viwanda vya samaki na viwanda vyengine vya mazao ya baharini upo mkubwa na nafikiri hii ndio *target* ya Mhe. Rais katika miaka mitano ijayo.

Mhe. Spika, sekta hii ya viwanda inategemeana sana na sekta ya utalii, kwa bahati nzuri Zanzibar ni sehemu ya utalii kwa asilimia karibu 80. Na ilivyokuwa tumemaliza uchaguzi kwa salama nchi yetu iko kwenye amani ni matarajio kwamba *season* ya utalii itakuwa nzuri na uchumi wetu utaimarika kwa kupitia sekta ya utalii. Tunashukuru kwamba lipo wazo la serikali la kuimarisha Chuo cha Utalii na kukiunganisha na *SUZA* ili sasa tutoe wataalamu bora wa shughuli za utalii. Ni jambo la kuungwa mkono, la kushukuriwa lakini pia la kufanyiwa kazi kwa haraka. Ukipita pale Chuo cha Utalii sasa hivi wameanza kuwa na ujenzi mwengine pale pale kwenye chuo, nafikiri ni moja ya shughuli za kuimarisha hicho Chuo cha Utalii.

Mhe. Spika, lakini pia katika sekta hii bado sisi watu wa Zanzibar nahisi hatujautambua vizuri utalii, wamo humu wengine wataalamu wa utalii ndani ya Baraza, wengine wako nje lakini watu bado wanaona kama ajira za utalii ni kama ajira za kihuni baadhi ya sehemu. Lakini nafikiri tukitambua kwamba utalii sio uhuni, utalii ni sehemu moja ya uchumi wetu, basi wananchi wengi wanaweza kuweka heshima na kuwa katika shughuli za utalii.

Mhe. Spika, naomba niendelee na sekta ya michezo, nashukuru kwamba jana Mhe. Rais amezungumzia kwa kina umuhimu wa kuimarisha michezo. Kama nilivyosema viwanda vilianguka katika miaka ya 80 na 90 na sekta ya michezo mimi nahisi nayo mpaka miaka ya 90 ilikuwa iko vizuri sana. Lakini miaka hii ya 2000 kuendea juu tumekuwa na migogoro mingi zaidi kuliko mafanikio ya michezo. Kila siku watu wanachaguana hawamalizi miaka mitatu wanafukuzana, michezo haina mwenyewe. Kwa hivyo, ni matarajio yangu na nimeshukuru kwamba mfano *ZFA* ambao wanashughulikia mpira; mpira ni mchezo ambao unapendwa na wananchi wengi sio Zanzibar tu karibu dunia nzima.

Lakini kwa miaka miwili mpaka mitatu Zanzibar tumekuwa tunayumba sana katika mambo ya mpir, kuanzia uongozi na mafanikio yenyewe. Leo Zanzibar zinachezwa *league* mbili tofauti, kuna *league* ya Pemba na kuna *league* ya Unguja, leo Zanzibar kuna vyama *ZFA* ina Kamati Tendaji Pemba, ina Kamati Tendaji Unguja chama ni kimoja. Sasa uzuri wenyewe nashukuru kwamba wanafanya uchaguzi na uzuri wenyewe nasikia umesogezwa mbele uchaguzi wao mpaka pengine Juni, Mwenyezi Mungu akipenda tayari tutakuwa na Waziri wa Habari pengine na michezo siwezi kujua vipi. Huyu waziri atakuwa na kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba hili tamko la Mhe. Rais la kuimarisha michezo linafanyiwa kazi kwa uhakika kwa sababu asilimia kubwa ya wananchi ama vijana ama wazee ama wanawake au wanaume ni wana michezo. Kwa hivyo, lazima sekta hii nayo ishughulikiwe vizuri ili kuendeleza maslahi ya vijana na maslahi ya Wazanzibari kwa ujumla.

Mhe. Spika, sekta nyengine muhimu katika kuimarisha uchumi ni miundombinu na bahati nzuri Mhe. Rais nayo kaizungumzia hii. Tunayo miundombinu mingi; jana amezungumzia barabara nne ambazo zinatarajiwa kujengwa katika kipindi hiki, lakini pia umalizaji wa *Airport* na ujenzi mpya wa Bandari ya Mpigaduri, bandari muhimu sana katika uchumi wetu. Na kwa bahati nzuri haina mashaka maana yake wanayoishughulikia au wafadhili wakubwa watakuwa ni wale wale rafiki zetu wa China. Kwa hivyo, hatutarajii mradi huu kuambiwa kwamba nao umesitishwa, ni matarajio yetu kwamba Bandari ya Mpigaduri itajengwa na itasaidia sana shughuli zetu za maendeleo ili Bandari ya Malindi tuiache kwa shughuli za abiria na mizigo midogo midogo. Ni matarajio yetu kwamba shughuli hii itafanyika vizuri. Lakini pia kwenye sekta ya umeme na maji huko nako juhudi za serikali ni nzuri, tumpongeze Mhe. Rais na mipango ya kuimarisha sekta hizi naona inakwenda vizuri.

Mhe. Spika, pia nizungumzie Baraza la Wawakilishi maana yake hapa ndio nyumbani kwetu. Mheshimiwa kama nilivyoanza mwanzo niwashukuru na kuwapongeza waheshimiwa wote waliopitia majimboni, waliopitia viti maalum na waliopitia kundi la Rais. Hapa sasa Baraza limetimia na uzuri wenyewe ukiangalia tu unaona kwamba Baraza limetimia. Ukumbi umejaa na nina hakika wote watajitahidi kuchangia kwa uadilifu.

Mhe. Spika, kuna hofu ya baadhi ya watu wanafikiria na wanauliza Baraza lote ni la CCM kabla ya kuingia waheshimiwa watatu hawa, hivi Baraza hili si litakuwa ni doro doro. Mimi nafikiri niwatoe shaka, mimi niliingia Baraza hili kwa mara ya kwanza 2000 na tulivyoingia ilikuwa kama hivi, kidogo ilikuwa tofauti na hivi, kwamba sisi tulichaguliwa na CUF walichaguliwa lakini CUF wao wakasusa. Sasa ikawa kususa kwa CUF ikawa sisi tuko kidogo sana CCM pale, sio sana lakini sio kubwa kama hili na kukawa na *backbencher* na kukawa kuna mawaziri. Lakini Baraza ambalo lilikuwa na *pentagon* kwamba lilikuwa ni Baraza hai sana lilikuwa ni wana CCM peke yao na mawaziri wakati ule walitoka kijasho sana, na Mhe. Spika wewe ulikuwa ni waziri wakati ule, lakini siku yako ilikuwa lazima urowe mwili mzima. Ikifika Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi lazima unaroa kwa sababu wajumbe walikuwa hatari.

Sasa natarajia na Baraza hili ni CCM tutakuwa na akili ya kuchangia lakini nafikiri haitokuwa Baraza mfu, litakuwa hai. Sura nikiziona humu naona watu wako makini na watachangia vizuri sana. Na tumewasihi wale wapya uzuri hakuna uchoyo katika Baraza hili, ukiwa na jambo unataka kumuuliza mwenzako muulize atakusaidia, sisi tulijifunza kwa kina Mhe. Shihata, Mhe. Haji Omar wakati ule Mhe. Ame Mati, Mhe. Marehemu Ramadhani Nyonje hao ndio walikuwa watu unachangia, unasoma unaambiwa hapana Baraza la Wawakilishi ukichangia usisome, unatazama kidogo hivyo hivyo unakwenda mbele.

Kwa hivyo, nina hakika na hawa watajifunza lakini naona kuna vigogo humu ukiwaangalia usoni kina Mhe. Said Soud unajua kwamba vitu vipo kichwani moja kwa moja. Kwa hivyo, sitarajii Mhe. Hamad Rashid ni mzoefu kabisa sana wa siasa na Sheikh Juma pale na yeye sio mgeni wa siasa na huku ukitazama pembeni Balozi Ali Karume hapa karibu wote Mhe. Castico, Mhe. Amina wote ni watu ambao wanaweza kufanya kazi vizuri. Kwa hivyo, Baraza hili nina hakika litasaidia serikali. Maana yake kazi ya Baraza ni kuisimamia serikali, kupitisha bajeti, watafanya kazi nzuri na kwenye kamati pia watafanya kazi nzuri. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nizungumzie pia katika sehemu ambayo Mhe. Rais…

Mhe. Spika: Mheshimiwa umebakisha dakika mbili.

Mhe. Machano Othman Said: Sawa mheshimiwa namalizia hili la miji mipya.

Nashukuru sana kwamba Mhe. Rais kazungumzia kwamba ili kuulinda Mji wa Zanzibar au kuutanua kutakuwa na miji mipya mitatu; Chuwini, Tunguu na Fumba. Chuwini kwa ajili ya kukabiliana na Kaskazini ya Unguja, na Tunguu kwa ajili ya kukabiliana na Mashariki ya Unguja, na Fumba kwa ajili ya kukabiliana na Kusini Unguja. Mheshimiwa hili jambo jema sana, pale Chuwini kuna maamuzi ya serikali karibu miaka 30 nyuma kwamba iwe Makao Makuu ya Serikali, lakini kwa bahati mbaya tumechelewa, lakini matarajio yangu kwamba pale Chuwini sasa kutakuwa pengine na mji mpya mdogo. Tunataka stendi ya magari, tunataka masoko na vitu vyengine vya maendeleo. Mimi ni mwakilishi wa jimbo nitashirikiana na serikali kuhakikisha kwamba Chuwini unakuwa mji.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nivishukuru vikosi vyetu vyote vya ulinzi na usalama, vya SMZ na SMT wamefanya kazi nzuri sana na ya mfano na tunaomba waendelee na kazi yao nzuri. Mhe. Spika, naomba nimalizie hapo, nashukuru sana hotuba ya Mhe. Rais. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Juma Makungu Juma: Mhe. Spika, ahsante kwanza kabisa na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu kwa kutujaalia uhai tukaweza kukutana hapa leo kwa kujadili hotuba ya Mhe. Rais.

Mhe. Spika, lakini la pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na tatu niwashukuru wajumbe ambao wamepata uteuzi wa Mhe. Rais jana na leo tayari muda mfupi tu wamekula kiapo na kuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kusaidiana katika mambo yetu.

Mhe. Spika, hotuba ya Mhe. Rais jana ilikidhi haja kwa sababu imegusa kila mmoja wetu, imemgusa kila mmoja wetu kwa maana ya kwamba kama alivyokuwa amebainishwa akina mama, vijana, wenye ulemavu na watoto. Na kama ilivyo katika Baraza lako tukufu watu wa namna yote kasoro watoto tu hawamo, lakini vijana tupo, wazee wapo ambao tutachota hekima kwao, akina mama wapo na wenye ulemavu pia wapo. Mhe. Spika, nasema imekidhi haja kwa sababu ilikuja na majibu ya maswali na changamoto ambazo zinatuzunguka katika jamii.

Mhe. Spika, kama nilivyosema awali kwamba inamgusa kila mmoja wetu na mimi Mwakilishi wa Jimbo la Kijini pamoja na wananchi wangu inatugusa moja kwa moja, kwa sababu Kijini ya sasa inayotegemewa baadae, jana imezungumzwa kwenye hotuba hapa, kwamba kutakuwa na hoteli moja kubwa ya Kimataifa. Lakini itakuwa ina Uwanja wa Ndege miaka 200 iliyopita hatukuwa na mawazo, hakukuwa na hata wazo la kwamba kungekuwa na hoteli ya Kimataifa au Uwanja wa Ndege. Mhe. Spika, inawezekana siku moja nimechelewa nyumbani mimi au mwakilishi mwengine itategemea Mwenyezi Mungu atapanga vipi nitakuja kwa Chata kutoka Kijini na kuja kutua *Karume International Airport,* nafika hapa bila ya kuchelewa.

Mhe. Spika, kundi la vijana lina matumaini makubwa na hotuba ya Mhe. Rais, kwa sababu kama tunavyojua vijana ndio nguvu kazi ya Taifa na wapo kwa asilimia kubwa katika nchi yoyote duniani na tatizo la ajira limezungumziwa na tuna matumaini makubwa kwamba litafikiwa.

Mhe. Spika, lakini kuna suala la ardhi ambalo Mhe. Rais jana kalizungumza kwa msisitizo ukilinganisha na sekta nyengine. Hili suala ni kubwa sana katika nchi yetu kwa sababu kila mtu anaitegemea ardhi kwa asilimia mia. Sasa watendaji katika wizara hii ni lazima kila siku wazidishe juhudi kuona namna gani linaweza likapunguza mzozo. Ukiangalia katika jamii yetu si wengi waliokuwa wana uelewa ama sio wote.

Sasa tunawazungumzia hawa ambao hawana uelewa inawezekana serikali imesema kwa nia njema tu labda eneo hili lisitumike kwa matumizi ya raia. Lakini kutokana na ama hapana kitambulisho ama kitambulisho kimeondolewa na wale wajanja wanaotaka serikali yetu iingie katika migogoro na wananchi wake, basi utakuta mwananchi anatumia ile ardhi lakini badala ya kwamba akazuiliwe katika muda ule wa kabla hajaathirika sana, anaachiwa anatumia mpaka tayari ashaathirika sana ndio anakwenda kuchukuliwa hatua. Sasa hili jambo halipendezi na hasa tukichukua kwamba serikali ndio mlezi wa raia wake wote.

Mhe. Spika, mimi niliombe Baraza lako tukufu kwa umoja wetu kwamba tuwe na nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba hotuba ya Rais inatufikisha pale palipokusudiwa, kwa sababu imekidhi kila haja. Mimi sioni pakukosoa lakini jambo moja tu sikuliona kwa mtazamo wa kawaida hivi, labda inawezekana inaingia katika ile dhana ya ujumla ya kwamba hapa kazi tu, kwa sababu mna maneno yalisemwa kwamba inatosha na sasa majipu yatatumbuliwa na moyo wake.

Sasa lile suala la watu waliokuwa wanalipwa hewa, kwa mfano nimewahi kusikia vyombo vya habari kwenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano zaidi ya 1000 wapo. Sikuliona hapa likitajwa *live* lakini kwa maana ya kwamba kila aliyekuwa ana dhamana amwajibishe wa chini, si hivyo atawajibika yeye labda inaingia hapa, na hapa mimi ninapashukuru sana kwa sababu na ndio hapo nataka Wajumbe wa Baraza lako tukufu kutoa ushirikiano wa hali ya juu pamoja na wananchi kwa ujumla kuhakikisha kwamba kila changamoto ambayo inasababishwa na watendaji wa serikali waibainishe, wazungumze kwa Wajumbe wao wa Baraza la Wawakilishi kusudi isemewe na ipatikane ufumbuzi wake.

Mhe. Spika, baada ya hayo kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kijini naunga mkono hotuba ya Mhe. Rais kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, ahsante na mimi nianze kwa kumpongeza Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa hotuba nzuri aliyoitoa jana. Nimepokea pongezi nyingi nikafikiria ni pongezi za kwangu, lakini watu wakasema kwamba ile hotuba ni darasa na inawezekana ni katika hotuba ambazo kwa miaka mingi na siku za mbele kuwezekana kuwa ni hotuba moja ya kihistoria. Pia, inawezekana hotuba hii kwa wanafunzi wetu kutoka vyuo vikuu wakaijadili kwa undani na kina ili wapate kujua ni yepi ambayo serikali yao inataka iwatendee kwa awamu hii ya mwaka 2016 kuelekea mwaka 2020.

Pia, nichukue fursa hii kukupongeza wewe Mhe. Spika, kwa kura nyingi ulizozipata lakini pia tangu ulipoanza umeonekana kwamba hicho kiti ni cha kwako. Wazungu wanasema '*you deserve'*. Kwa hiyo na sisi tutakuunga mkono tutakuwa na wewe pamoja.

Mhe. Spika, lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. John Pombe Magufuli kwa ushindi mkubwa aliyoupata mwaka jana, lakini pia nichukue fursa hiyo kumpongeza Makamu wetu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hasa akinamama wote Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka historia ndani ya nchi yetu. Kwa kweli hili ni jambo pekee la kujivunia sisi Watanzania kupata mwanamke na kina mama kuona kwamba yale ambayo yamekuwa kilio chao yanakuwa.

Vile vile, nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Tunguu nikianza kutoka Dunga Kinyongo, Gogoni**,** Dunga Bweni, Kiembeni, pia Mwera Pongwe, Ubago, Mtakuja, Binguni, Jumbi, Tunguu, Kikungwi, Ungujaukuu Kaebona, Ungujaukuu Kaepwani pamoja na Tindini na nyumbani kule Uzi pamoja na Ng'ambwa. Nasema ahsanteni sana.

Mhe. Spika, katika jambo ambalo amezungumza jana Mhe. Rais, utaona kwamba ana dhana kabisa ambayo ameikusudia kutaka serikali yetu na nchi yetu kuweza kujitegemea.Katika malengo ambayo Mhe. Rais ameyataja ni kuwa tukifikia mwaka 2020 taasisi zetu za kupokea na za kukusanya kodi waweze kufikia lengo la kupokea shilingi 800 bilioni. Hili jambo linawezekana na litahitaji kufanyiwa kazi kwa pamoja baina ya Baraza pamoja na serikali yake ambayo ataiunda na wengine tunaona sura za mawaziri zinaanza kuelekea maana yake viti vyao wameshaanza kuvijua.

Mhe. Spika, lakini mambo mawili ameyagusia ambayo nahisi yatakuwa ni muhimu ndani ya serikali yake, moja ambalo Mhe. Hamad Rashid, pia ameligusia ni sera ya bahari kuu. Hii ni rasilimali kubwa sana ambayo tunayo katika nchi yetu na ya pili ni rasimu ya mafuta na gesi. Suala hili limekuwa linazungumziwa sana katika miaka ya nyuma na nimeona katika mtandao, maeneo tofauti na taarifa zimetoka, lakini maeneo haya mbali ya kwamba serikali itahitaji kuyatekeleza lakini pia tutahitaji ushirikiano wa wananchi wetu, hatuna budi kutoa mawazo yetu na pia kuishauri serikali kwamba katika yale yote ambayo serikali itakayoundwa na watakayokusudia kuyatenda basi ni vyema wananchi wetu wapate elimu, taaluma na taarifa za kutosha.

Mara nyingi kule Ulaya kuna kitu wanakuwa wanafanya, wanazungumza na wanaita *public enquiry*, yaani kabla hujatekeleza jambo katika eneo husika unawaita wananchi ili waelewe, wafahamu, wasomeshwe ni kitu gani ambacho serikali yao inakusudia kuwafanyia ili lile jambo liweze kufanikiwa kwa asilimia mia moja.

Pia, katika kuyatekeleza haya yote ambayo yametajwa katika hotuba yake ambayo yamegusia masuala ya viwanda na wachangiaji wengi wamezungumza, kuna kitu muhimu nahisi ni vyema tukakiangalia ni suala la *Legal Framework* na hizi Mahakama zetu pia tusisahau kuhakikisha yale yote ambayo yatatendwa basi Mahakama zetu zinakuwa zimejitayarisha kwa migogoro, ushauri na matatizo yoyote yatayojitokeza basi ziwe ziko tayari. Lakini pia nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Rasi katika hotuba yake aliposema kwamba kuanzia mwezi wa Aprili wazee wetu wenye umri wa miaka 70 wataanza kupokea ruzuku zao au pencheni na waweze kusaidiwa. Kwa kweli hili anastahiki kupongezwa sana.(*Makofi*)

Vile vile, amezungumzia suala la kuanzisha Mahakama za watoto, laiti kama tutakuwa tumefuatilia katika miaka ya karibuni watoto wetu wamekuwa wanaharibiwa katika mazingira ambayo mengine hayafai hata kuzungumza humu ndani, zipo taasisi zinafanya kazi vizuri kabisa kwa kushirikiana na serikali, lakini mikoa ambayo inaongoza ni

Mkoa wa Kaskazini Unguja.Tumefika hata unaposikia watoto ambao ni walemavu wanaharibiwa, kwa kweli hili suala la Mahakama lifanywe haraka ili haya matendo tuweze kuyatokomeza katika nchi yetu.

Jana Mhe. Rais, alizungumza, naomba nimnukuu hapa katika *speech* yake amesema hivi:

"Kama hayo ni majipu basi nataka niahidi nitayatumbua na moyo wake tutautoa".

Mhe. Spika, kuna mambo madogo madogo mengi lakini yana umuhimu wake katika yale ambayo Mhe. Rais pengine na serikali yake atakusudia kuyafanya. Kuna masuala ya rushwa, lakini pia masuala ya mtu kujua majukumu yake anapoingia kazini (Uadilifu). Kwa kweli naweza hata mimi mwenyewe nikaleta masikitiko yangu au nikasikitika mwenyewe kwamba, huwezi ukajenga mazingira bora kazini ikiwa uadilifu haupo na uadilifu unaanza kwa kiongozi mwenyewe, yaani Rais, serikali yake, yaani mawaziri wake, makatibu wakuu, wakurugenzi na wengine wote, haiwezekani mwananchi anakwenda katika sehemu ya serikali anahitaji huduma, anapewa majibu kwamba, subiri nimalize kula mbatata zangu za urojo au natoka mara moja nakwenda nje nisubiri. Haya ndio majipu yenyewe, kwanza wananchi wanataka waone, yaani suala la uadilifu.

Mhe. Spika, lakini uadilifu huu pia unakwenda kwenye mavazi, ndani ya serikali yetu ni vizuri pia mavazi yakajulikana juu ya watendaji ni mavazi gani ambayo mwananchi aliyeajiriwa ndani ya serikali anatakiwa avae, huwezi ukamkuta dereva wa waziri anavaa *sandals* au malapa, shati kifungo wazi, mbona wenzetu kule Bara hawavai hivi. Kwa hivyo, uadilifu kwanza lazima urudi ndani ya serikali uonekane ili wananchi wajenge matumaini ndani ya serikali yao na yale mengine yote ndio yatakapofuatwa.

Pia, niseme jana katika hotuba nzuri ya Mhe. Rais, jimbo langu lilitajwa mara tatu, naweza nikasema kwamba kwa ile serikali atakayoiunda mimi nikiwa Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu kwa kushirikiana na Mbunge wangu maarufu Mimina na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mimi ndiye mpakabasi, hivyo, sisi katika jimbo letu tuna mimina mpakabasi. Kwa hiyo, inawezekana sana, maana yake jimbo letu tuna bahari, maeneo ya kale, kisiwa, maeneo ya kulima, tuna wananchi wenye rika, madhehebu na makabila tofauti, tunaweza tukasema kwamba baada ya Jimbo la Malindi, basi jimbo langu la Tunguu ni kama Ulaya, tumechanganyika madhehebu na makabila tafauti na karibuni sana Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika, ninapozungumza hivyo, maeneo ya barabara aliyoyazungumza na wachangiaji waliopita walizungumzia hiki kitu kinachoitwa utalii. Kwa kweli utalii ni katika eneo moja muhimu sana la uchumi wetu sote tunatambua, lakini utalii si eneo la Muungano kama mazingira lakini linatugusa visiwa vyetu vya Zanzibar; Unguja na Pemba kwa pamoja na pia kwa kushirikiana na wenzetu kutoka Tanzania Bara. Asilimia 35 ya wageni wanaokuja Tanzania huwa wanakuja kutembelea visiwa vyetu, nasema kwa Kizungu *bush* halafu *beach*, yaani nenda mbugani halafu njoo katika fukwe zetu uje kupumzika. Kwa hiyo, athari yoyote inayotokezea Tanzania Bara basi na sisi pia huasirika na yale ambayo yanatokea huku Zanzibar basi na wenzetu kule Tanzania Bara nao wanaathirika.

Sasa niseme katika hili ni yepi ambayo tunaweza kufanya kazi kwa ushirikiano, kuna umuhimu na juhudi au bidii za makusudi lazima serikali yetu kwa ukaribu kabisa kuanzisha kitengo cha ushirikiano pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais wa Tanzania Bara ili kuangalia ni maeneo yetu wanaweza kufanya kazi kwa pamoja. Sisi kwa mfano upande wetu Zanzibar hatuwezi kuanzisha Shirika la Ndege kwa sababu masuala ya usafiri na anga ni masuala ya Muungano, hata tukiamua pia Serikali ya Zanzibar inunue hisa katika hizi kampuni binafsi, basi hizi ambazo tunaita *Air Service Agreement*, hizi *routes* zote zipo ndani ya Muungano ambapo mwenyewe ni Shirika la *Air Tanzania*.

Mhe. Spika, ili tuweze kufanikisha haya tuna bodi zetu huku Zanzibar, tuna bodi kule ndani ya Jamhuri ya Muungano *CCB* na huku kuna *Zanzibar Tourism Board* ambayo pia inaitwa Kamisheni ya Utalii, lakini hakuna kitu ambacho kinatuunganisha sisi kuweza kufanya kazi kwa pamoja. Taasisi zetu zikiondoka na zikienda nje kila moja inakwenda yenyewe, Kamisheni watakwenda kwa upande wao kufanya *marketing* na *promotion* na sisi kwa upande wa Zanzibar tutakwenda kwa upande wetu pamoja na hizi jumuiya zilizokuwepo na mahoteli tuliyonayo.

Sasa ikiwa sisi ni nchi moja na utalii ni sehemu moja muhimu, kwa hiyo kuna umuhimu ili kuondoa changamoro zilizokuwepo ndani ya Muungano tuweze kufanya kazi kwa pamoja, basi hatuna budi kwamba yale yote ambayo Rais amekusudia kuyafanya na serikali yake katika eneo hili aweze kuziorodhesha changamoto zile ili tuweze kufikia yale malengo.

Kwa mfano, naweza kutoa mfano hai, huu ni mwezi wa Aprili unakuta kipindi hiki tunaita *low season*, wageni wanaanza kupungua. Lakini katika eneo moja ambalo nahisi na naamini linaweza kutusaidia sisi kwa upande wa Zanzibar na hasa katika yale ambayo Mhe. Rais ameyataja ni masuala ya *visa*. Tanzania sisi tume-*border* na nchi tano, yaani ni wanachama ndani ya *East African Community;* Nairobi, Kigali, Bunjumbura na Kampala. Nairobi kuna wafanyakazi ambao wao wanatoka nje, Wazungu hawa kutoka Marekani, Uingereza, wafanyakazi katika mashirika ya *United Nation* za Umoja wa Mataifa na taasisi zao wapo Kenya na wale wana haki ya kuishi pale kwa kupatia hizo *resident permit* zao. Lakini sisi kwa upande wetu Tanzania tunawachukulia wale kama bado ni Wazungu na ni wageni.

Leo sisi kama Watanzania tunataka vitanda vyetu visilale vitupu havitusaidii kitu, kwa nini hawa Wazungu ambao wanaishi Afrika Mashariki na Nairobi kuna John na mkewe anaitwa Jenifer wana watoto watatu wakitaka kuamua kuja *weekend* hapa Zanzibar, kila mmoja analipa *visa US$* 100 ni sawa na *US$* 500, tukiondoa *visa* na serikali yetu ikaenda kule ikafanya *promotion* nzuri pamoja na jumuiya zetu tulizokuwanazo hapa na mahoteli tutauza *packages* nyingi kuliko vitanda vyetu kulala vitupu. Basi ni vizuri tukaangalia tuondoe *visa* kwa nchi ambazo ni jirani kwa wale wageni ambao wanaishi.

Mhe. Spika, jambo hili halihusiani na nchi katika *East African Protocol* na *community* yetu halimo kabisa. Sisi tunakwenda kuwatambua wale kama Wazungu wanaoishi na ili jambo hilo lifanikiwe ndio maana nikasema hii ni changamoto ambayo ipo ndani ya Muungano kwa sababu sisi hatuwezi kuamua. Masuala ya mambo ya ndani ni masuala ya Muungano na Wabunge wetu kwa bahati mbaya au nzuri mambo kama haya siwasemi vibaya, lakini nasema ukweli sijawahi kumsikia Mbunge wa Zanzibar kutetea masuala haya kule Bungeni, naamini wale Wabunge watano wataotoka katika Baraza letu mara hii watakwenda kutufanyia kazi ambayo na sisi pia tutafurahi.

Mhe. Spika, pia, nataka niseme jambo ambalo mheshimiwa mmoja ameligusia hapa, ni suala linalozungumzwa sasa hivi katika mitandao la *Millennium Challenge Corporation (MCC),* kwamba Serikali ya Marekani imeamua kuzuia hizi *US$* 400 *millions.*

Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe, mimi nashukuru hapa tumepata Wajumbe wapya ambao naweza kusema kwamba Balozi Ali Karume ni kama baba yangu pamoja na Balozi Amina Salum Ali na wanaweza wakalizungumza hili kwa undani. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ninavyofahamu mimi tumezungukwa na nchi karibu nane; kuna Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Mozambique, Malawi, Congo, sijui kama zote nimezitaja. Lakini Tanzania hii imeshiriki katika ukombozi wa nchi nyingi za Afrika Mashariki pamoja na Kusini, tumeshiriki sisi katika kupinga ubaguzi wa South Africa na Makao Makuu ya *NC* yalikuwa hapa Tanzania.

Mhe. Spika: Mheshimiwa, una dakika mbili.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, tumeshiriki pia katika ukombozi wa nchi tofauti katika *liberation struggle*. Heshima yetu inajulikana hizi nchi zote, uchaguzi uliofanyika juzi Uganda hatuwezi hata kuufananisha kwenye hii kucha yangu baina ya uchaguzi wa Oktoba, 2015 na uchaguzi wa 2020, wapinzani wamepigwa, wametiwa ndani, wamenyanyaswa, lakini Marekani anasema kwamba uchaguzi ule watu waendelee kuzungumza na waheshimu *to prime court* maamuzi yao waliyotoa, hivi leo sisi Tanzania tumefanya kosa gani kubwa. Tunalo tatizo la kisiasa na linazungumzika, kwa hiyo na sisi hatutotetereka kama Tanzania, tunaunga juhudi zote za viongozi wetu, tumemsikia Rais John Pombe Magufuli alivyozungumza na pia jana tumemsikia Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tutaunga mkono.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache niliyozungumza na muda mdogo ulionipa nilikuwa nina hamu ya kuzungumza mengine, basi niishie hapo kwa leo, nikushukuru kwa nafasi ulionipa. Pia, nimalizie kuwashukuru wazee wangu akiwemo marehemu Bwana Mohammed Said pamoja na mama yangu Bi Zulfa kwa malezi mazuri na baada ya kushiriki chaguzi nne, najipongeza mimi mwenyewe sasa nimefika mjengoni. Ahsanteni. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Spika, naomba kumshukuru *Allah* (*S.W*) kwa kunijaalia uzima na kutujaalia Wajumbe wote kuwa wazima na wale waliokuwa wanaumwa au wana matatizo Mwenyezi Mungu awape uzima Tanzania nzima.

Mhe. Spika, naomba kushukuru sana wazee wangu pamoja na familia yangu yote kwa kushirikiana na mimi kwenye suala hili la uchaguzi pamoja na kampeni zilizopita, nawashukuru sana pamoja na baba yangu mzazi alieni-*support* sana kwenye suala hili.

Vile vile, nawashukuru pia viongozi wote wa Chama cha Mapinduzi walionisaidia kwa njia yoyote ile na kunifundisha na kuniongoza nawapongeza sana, vile vile, nawashukuru na nawapongeza sana wananchi wangu wa Jimbo langu Chaani kwa kunichagua kwa kura nyingi na *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu niwatekelezea ahadi zao kama nilivyoahidi ndani ya miaka mitano. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba kuchangia hotuba ya jana ya Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dokta. Ali Mohammed Shein, jana ametuhutubia tunashukuru sana kwa ujio wake na ni Rais ambaye amekamilika na mwenye hekima na ukweli na nampongeza sana kwa ahadi zake ambazo alizozitoa ndani ya Kampeni na sasa hivi ameanza kuzitekeleza na vile vile kuahidi kuwa zitafanyika *Inshaallah* ndani ya muda wake wa miaka mitano.

Mhe. Spika, mimi nitazungumzia katika hotuba ya jana suala la Mhe. Rais alililoliahidi la mshahara wa kima cha chini wa kima cha shilingi laki tatu kwa wananchi wote wa Zanzibar walioajiriwa katika serikali.

Mhe. Spika, Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi inaonesha dhahiri kwamba hana mchezo wa kauli zake na anatekeleza ahadi zake kama alivyoahidi na inaonesha dhahiri kwamba wananchi wote anawathamini hasa wenye kipato cha chini kuwapandishia mshahara wa shilingi laki tatu na ni mshahara naamini mzuri sana kwa nchi yetu kwa hali tuliokuwa tunayo na *Inshaallah* baadae pengine mambo yakiwa mazuri atawaongezea atakapoona mwenyewe sawa. Hili mimi nampongeza sana na wananchi wote wajione kwamba Mhe. Rais anawathamini sana na anawakumbuka na anawatakiwa katika maisha yao.

Mimi sitozungumzia mengi, mimezungumzia *points* zangu za kushukuru pamoja na kumpongeza Mhe. Rais kwa ujio wake na mambo mengi aliyoyazungumza jana yote yanakubalika na ni mazuri na yanatekelezeka kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu *Inshaallah* atayatekeleza na serikali ya Mapinduzi Zanzibar itatekeleza kama ilivyoahidi.

Vile vile, nampongeza Mhe. Rais kwa kuteuwa viongozi au Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi saba katika nafasi zake kumi, naamini hawa aliowateuwa kama ni vyeo vya majeshi basi ni majenerali na mabregedia wa siasa na wana uzoefu mkubwa na *Inshaallah* na mimi naomba vile vile nije niwe kama wao nifikie kiwango kama hicho na humu waliokuwemo Wajumbe wezangu vile vile wana uzoefu mkubwa, lakini ameona tu atuongezee majenerali wengine ili tuje tupate na sisi siasa zaidi na tujifunze zaidi katika masuala yetu.

Mhe. Spika, vile vile, nakupongeza na wewe kwa kupata nafasi ya uspika na naamini *Inshaallah* tutashikirikiana uzuri na una-*fit* katika kiti chako katika kutuongoza sisi na sisi *Inshaallah* tutakuwa pamoja katika kushirikiana na wewe kwa pamoja.

Vile vile, nawapongeza Wajumbe wote walioteuliwa katika nafasi zao za viti maalum; nafasi za Mhe. Rais na wale wote walioshinda katika majimbo yao nawapongeza sana na vile vile, nampongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Idd kwa kuteuliwa tena kwa mara pili na Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri katika kutekeleza wajibu wake.

Ahsante sana na mimi hotuba hii ya Mhe. Rais nai-s*upport* asilimia mia kwa mia, ni nzuri sana, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kutoa mchango wangu juu ya hotuba iliyo mbele yetu ambayo tunaijadili hivi sasa.
Awali ya yote napenda nitoe shukurani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Mkoani Pemba kwa kuonesha moyo wa kuniunga mkono na kuwa na imani na mimi katika kuwatumikia.

Aidha, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa watu wa Kisiwa Panza, Chokochoko, Michenzani, Mkanyengeni, Shidi, Mtuhaliwa, Changaweni, Kwachangawe, Mbuguwani, Kironi, Kionwa, Uweleni, Ngombeni, Mbuyuni, Jondeni na Makombeni. (*Makofi*)

Sasa nichukuwe nafasi hii kutoa maelezo yanayohusiana na hotuba yetu hii. Kwa kweli niliisikiliza kwa makini hotuba hii jana na baadae nikapata fursa kuisoma neno kwa neno, kurasa kwa kurasa hadi mwisho. Na nimekuwa nikifanya hivyo kwa sababu mara zote ile ladha yake haimaliziki katika fikira zangu. Sasa baada ya kuisoma kwa makini na baadae kupata fursa ya kusoma nyaraka nyengine kwa kulinganisha, nikagundua kwa kweli hotuba hii ni ufupisho wa mambo ambayo yanatokana na Ilani ya Chama cha Mapinduzi, MKUZA II, Dira ya Maendeleo 2020, pamoja na *International Convention and Commitment*. Kwa hivyo, haikuacha kitu, yale mambo muhimu yanayozungumzwa katika nyaraka hizo na nyenginezo kwa kweli yanagusiwa katika hotuba ya Mhe. Dr. Ali Moh'd Shein.

Kwa hiyo, kwetu sisi viongozi Wawakilishi wa wananchi tuna wajibu gani katika hotuba hii. Uhakika nilivyoisoma naona kuna mambo mawili muhimu, hotuba huu imezungumzia masuala jumla jumla ya kitaifa na sehemu chache imetaka maeneo mahasusi. Lakini sisi Wawakilishi tunahusika katika sehemu hii ya jumla lakini pia tunahusika katika sehemu nyengine mahasusi, yaani katika majimbo yetu.

Je, tutaitekeleza vipi hotuba hii katika majimbo yale, ni hilo jambo la kutafakari na kuzingatia. Mathalani amezungumzia suala la mazingira, sisi Wawakilishi katika maeneo yetu tutaitekeleza vipi malengo haya yaliyoelezwa katika hotuba hii kama ni elimu katika majimbo yetu tutaitekeleza vipi, kama ni afya katika majimbo yetu tutaitekeleza vipi, kama ni kuimairisha vyama vya ushirika na *SACCOS* katika majimbo yetu tutayatekeleza vipi. Hili ndilo jambo muhimu la kulizingatia kwetu Wawakilishi.

Mhe. Hamad Rashid, pale alizungumza vizuri kwamba hotuba ni jambo mbali na utekelezaji ni jambo mbali. Kwa hivyo, sisi Wawakilishi mkazo wetu uwe kufikiria namna gani ya kubuni mikakati ya kuweza kuisaidia serikali, lakini wakati huo huo na sisi wenyewe Waheshimiwa Wawakilishi wa wananchi tutafanya nini ili kuitekeleza hotuba hii *100 percent*, hilo ni jambo muhimu sana.

Mhe. Spika, nieleze kwamba kuna kipengele hichi cha mapato, nchi yoyote duniani inaoendeshwa kwa mapato na lazima tubuni mikakati sahihi ya kuimarisha mapato katika nchi yetu, kwa sababu hili lengo letu la kujenga nchi ya uchumi wa kati ifikapo 2020 halitaweza kufanikiwa kama hatujawa na mikakati sahihi ya ukusanyaji ya mapato. Mikakati ambayo itajaribu kuziba mianya yoyote ambayo inasababisha kupotea kwa fedha zinazotokana na mapato. Jambo hili lazima tuishauri serikali kubuni mikakati sahihi.

Vyenginevyo, mambo yetu mengi haya ambayo tumeyapanga au mambo mengi ambayo Mhe. Rais ameyataja yatakuwa ni vigumu kutekelezeka. Lakini "penye nia pana njia" na hili linawezekana kwa ninavyoona Wawakilishi wenzangu walivyoimara kwa kweli hili linawezekana.(*Makofi*)

Mhe. Spika, kuna suala jengine ambalo mara nyingi japo kuwa sikuwa mwanasiasa wa muda mrefu lilikuwa linanikereketa kidogo suala la kuimarisha vitendea kazi na maslahi ya vikosi vya ulinzi, yaani vikosi vya SMZ. Kwa kweli hotuba imeeleza vizuri na sisi Wawakilishi kwa kweli tuna wajibu wa kuisaidia serikali kukusanya mapato ili mapato hayo yaweze kutumika kuwalipa vizuri walinzi wetu hawa ili angalau malipo yao yalingane na walinzi wenzao wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Kwa mujibu wa nidhamu ya kiaskari si dhani kama wao wana pa kusemea, lakini sisi Wawakilishi wa wananchi na askari ni rai wetu pia kwa namna fulani. Kwa hiyo, hatuna budi kuwasemea ili maslahi yao yaimarishwe. Lakini si maslahi tu na vitendea kazi tunahitaji kuwa na jeshi imara na la kisasa. Vijana wameonesha nidhamu, wana nidhamu vizuri sana, wana usikivu, kwa hivyo na sisi tusiwaangushe katika maslahi yao na katika kuwatafutia vitendea kazi, tunataka jeshi lenye umahiri na lenye kutosheka katika nafsi zao. (*Makofi*)

Hotuba ya Mhe. Rais, pia iligusia suala la Vyama vya Ushirika pamoja na *SACCOS*, ni jambo jema na kwa kweli tunahitaji kumuunga mkono Rais kuvisaidia na kuvifufua na kuviimarisha vikundi hivi. Mara nyingi sana inaonekana kama vimeanzishwa bila ya kuwa na nyaraka muhimu ya hati muhimu zinazowatambulisha. Nilikuwa nikifanya utafiti kidogo usio rasmi nikagundua vingi havijawa *registered*. Kwa hivyo, nafikiri tumsaidie Mhe. Rais kuvisaidia vikundi hivi vipate usajili ili vipate kujulikana rasmi na kuweza kupatiwa mikopo katika taasisi zinazohusika, hili ni jambo muhimu sana kuvisaidia vikundi hivi.

Lakini pia tuvisaidie kwa kuimarisha elimu ya ujasiriamali katika vikundi hivi kwa sababu elimu ya ujasiriamali inakuwa kama ni nyimbo inatajwa tu ujasiriamali, ujasiriamali, ujasiriamali. Lakini kwa kweli maarifa hasa ya ujasiriamali hayajawafikia hawa wananchi wetu. Kwa hivyo, katika kuitekeleza hotuba hii na katika kufanya kazi katika majimbo yetu tuhakikishe kwamba vikundi hivi tunavipatia elimu ya kutosha, elimu ya vitendo ya ujasiriamali hiyo ni mihimu sana. Mafunzo ya unadharia sana huwa hayawasaidii watu wa kawaida. Kwa hivyo, nafikiri tutoe mafunzo ya vitendo.

Mhe. Spika, kuna suala jengine ambalo limo katika hotuba ya Mhe. Rais, ni suala ambalo linahusiana na masuala ya ajira kwa kupelekea *green house* katika kila wilaya za Unguja na Pemba. Hili ni jambo zuri kabisa kwa sababu zitasaidia, si ajira peke yake lakini pia kuongoza mazao yanayohusika. Napenda kusema kwamba kwa bahati nzuri katika jimbo langu la Mkoani tumeshaanza sasa hivi tuko katika hatua za mwisho za kujenga mashamiana. Kwa hivyo, nadhani na majimbo mengine yajitahidi kufanya jambo hilo na ni jambo zuri na la kumaendeleo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nataka kuzungumzia masuala ya jumla ambayo yamo katika hotuba ya Mhe. Rais, nayo ni masuala ya elimu. Kwa hakika ipo haja ya kuongeza fani mbali mbali za elimu ya juu katika nchi yetu ya Zanzibar ili kuweza kukidhi soko la ajira la Zanzibar, la Tanzania, la Afrika Mashariki na kwengineko, hili ni jambo muhimu. Lakini kuna suala ambalo tunahitaji sisi Wawakilishi na serikali tulifanyie kazi.

Je, hii elimu ambayo tunatoa inasaidia kujenga muamko kwa wananchi wetu, kwa namna nyengine nataka kusema kwamba kuna hitilafu fulani katika kutoa elimu, elimu ya muamko kwa kweli iko chini hapa Zanzibar. Ninaposema elimu ya muamko maana yake nini, hakuna somo linaloitwa elimu ya muamko. Kwa hiyo, tusije fikiria kwamba tuanze kusoma sio, ni ile namna wanavyosomeshwa wanafunzi ndio wanaanza kujenga muamko hatua kwa hatua, nasema hivyo kwa sababu utashangaa utakuta mwanafunzi au mwananchi ambaye amemaliza masomo ya Chuo Kikuu anazungumza masuala kama; sisi hatuwezi kuendelea mpaka tupate misaada, hii maana yake kwamba hana muamko huyo.(*Makofi*)

Mhe. Spika, utamkuta vile vile anasema kwamba, tukea Mapinduzi hakuna maendeleo yoyote, hii ni dalili ya kutokuwa na muamko, utakuta mwananchi anapingana na sheria, hiyo ni dalili ya kutokuwa na muamko, utakuta mwanafunzi amemaliza masomo ya *Master degree* anaongoza na mjomba wake kutafutiwa kazi, mjomba wake ana darasa la nane au hakwenda skuli kabisa, hakika nimeikuta hiyo ndio maana nikasema. Sasa hii ni dalili ya kutokuwa na muamko. (*Makofi*)

Kwa hivyo, tunawajibu serikali na Wawakilishi tuna wajibu wa kutoa elimu ambayo itasaidia kujenga muamko na mwananchi anapokuwa na muamko anakuwa yuko tayari wakati wowote kusaidia nchi yake. Niliwahi kutembelea nchi moja wakasema kwamba, kutokana na muamko wa kimaendeleo waliokuwa nao wananchi haoni tabu kusaidia kwa alicho nacho, nimeambiwa kwamba kulikuwa na watu ambao wana herini tu moja ya dhahabu akasema naitoa hii isaidie kununulia vitabu skuli au natoa hii isaidie jambo fulani, kile ni kiwango cha muako.

Kwa hivyo, tuwawezeshe wananchi wetu wapate muamko. Na tukijenga fikira za muamko hata lile tatizo ambalo tunalipigia kelele sana la ukosefu wa ajira litapungua. Mwananchi akiwa na muamko wa kimaendeleo basi atajua afanye kazi gani katika mazingira yake ambayo itamkwamua. Lakini katika hali hii ya sasa kwa kweli tuna kazi kubwa ya kuwaelimisha wananchi wetu ili kupata elimu ya muamko.

Mhe. Spika, niendelee kuzungumzia suala la mazinngira. Jimbo langu mimi ni moja ambalo kwa kiasi kikubwa limeathiriwa na tatizo hili la mazingira kwa sababu kuna sehemu za visiwa kama Makoongwe na Kisiwa Panza na hata katika hotuba ya Mhe. Rais imetaja Kisiwa Panza, kwa kweli serikali kuu ina wajibu wake lakini pia na sisi Wawakilishi wa wananchi katika majimbo tuna wajibu wetu. Tuna wajibu wa kuisaidia serikali katika suala la upandaji wa miti, kuwaelimisha wananchi wetu kupunguza ukataji wa miti usio wa lazima. Lakini pia tuna wajibu wa kuyafufua maeneo ambayo hapo awali yalikuwa ni vianzio vya maji sasa maji yametoweka kuyarejesha na hili linawezekana chini ya nguvu ya pamoja kati ya wananchi na Mwakilishi wao, hakuhitajiki rasilimali kubwa sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nimalizie mchango wangu kwa kusema kwamba baada ya kuitafakari kwa makini hotuba ya Mhe. Rais, kwa ujumla wake nimeona mbali na masuala ya uchumi na ustawi wa jamii inatoa wito wa mambo matano muhimu.

(1) Uharaka katika utekelezaji.

Mhe. Hamad Rashid, pale amezungumza vizuri kwamba unaweza kwenda katika ofisi hujui muda suala litamaliza siku gani. Kwa hivyo, kuanzia sasa ni muhimu kuwa na uharaka katika kutoa maamuzi na katika kutekeleza, hili ni muhimu. (*Makofi*)

(2) Ubunifu

Hili Mhe. Rais amelitaja kwamba, lazima viongozi watakaoteuliwa na sisi Wawakilishi wa wananchi tuwe wabunifu katika kufanyakazi zetu, tuwache kufanya kazi kwa mazowea. Ubunifu ni muhimu, tusisubiri maelekezo kama alivyosema mwenyewe, maelekezo ya Rais au Makamu wa Rais, sisi wenyewe tuwe wabunifu, kwanza katika maeneo yetu au katika majimbo yetu, lakini na wale wa serikali pia katika sekta zao au katika taasisi zao na katika idara zao, hilo ni jambo muhimu na tukifanya hivyo kwa kweli tutafika tunapokusudia.

Jambo la tatu, ni suala la uadilifu, hotuba inahimiza umuhimu wa viongozi kuwa waadilifu na uadilifu sio kauli ni vitendo. Kwa hivyo, tufanye uadilifu ili wananchi wetu wakitutizama waseme kweli wawakilishi wetu na viongozi wetu ni waadilifu.

Jengina ambalo Mhe. Rais amelitaja katika hotuba yake ni suala la uajibikaji. Mara nyingi tunaposema uajibikaji tunaelekezea vidole labda viongozi wa serikali, yaani mawaziri, hapana. Huu uwajibikaji unatuhusu sote; wawakilishi wa wananchi, viongozi wa serikali wa idara, sekta na kila sehemu kwa kweli tunahitajika kuwa wawajibikaji. Uwajibikaji uko wa aina nyingi; kuna uwajibikaji wa kisiasa *political accountability*, kuna uwajibikaji mwengine *technical accountability*. Hii mwenzangu mmoja aliwahi kuitaja kwamba hata mtaalamu awajibishwe kitaalamu. Kama daktari kafanya uzembe fulani kwa sababu ya *profession* yake awajibishwe. Kwa hivyo, uwajibikaji usibakie katika siasa lakini uende mpaka katika ngazi nyengine za kitaalamu.

Mhe. Spika, jengine la mwisho kabisa ambalo linahusiana na hotuba hii ni suala la matumizi sahihi ya rasilimali tulizonazo...

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, una dakika mbili.

Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri: Ahsante. Rasilimali tulizonazo tuzitumie kwa usahihi na hasa rasilimali watu na wataalamu bado hawajatumika vya kutosha. Nimalizie kwa kusema kwamba naiunga mkono hotuba ya Mhe. Rais kwa udhati wa moyo wangu na kwa ukomo wa fikra zangu, ahsanteni. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri, hotuba yako imekuwa nzuri sana. Naomba sasa nimwite Mhe. Mgeni Hassan Juma, ambaye atafuatiwa na Mhe. Shadya Mohamed Suleiman na kama muda utaruhusu Mhe. Modlen Siras Castico ajiandae. *(Makofi)*

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii adhimu kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma, aliyetupa uhai, uzima na ambaye ametuwezesha leo hii kuwepo hapa na kuja kufanya shughuli zetu tulizojipangia. Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia machache yanayotokana na hotuba ya Rais.

Mhe. Spika, vile vile, nichukuwe fursa hii kuwashukuru Umoja wa Wanawake wa Tanzania wa Mkoa wa Mjini, kwa kunichagua kwa wingi kwa kura nyingi sana na kunitaka nije niwatumikie ndani ya Baraza hili, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia, nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Rais kwa kuchaguliwa na wananchi wa Zanzibar kwa kura nyingi sana zenye asilimia 91 na zaidi. Mhe. Rais amehakikishiwa na wananchi kwamba yeye ndio chaguo lao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pamoja na hayo sasa naomba kidogo nichangie hotuba ya Mhe. Rais ambayo iko kwenye meza yetu. Mhe. Spika, kama wenzangu walivyotangulia kusema na mimi naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, nina sababu nyingi sana ambazo zimenifanya nione kwamba hotuba hii ina umahiri mkubwa, lakini

nimeona kwamba hotuba hii imeweza kudadavua utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, imeweka bayana na wazi mambo ambayo Mhe. Rais, amekuwa akiyazungumza katika kipindi cha kampeni na kusema kwamba haya ndio yatakuwa mambo yangu muhimu katika serikali yangu, nampongeza sana Mhe. Rais. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Rais, amezungumzia masuala mengi yakiwemo ya kiuchumi, elimu, suala la huduma za jamii, lakini vile vile amezungumzia dira ya mipango ya vitega uchumi mbali mbali ambavyo vinatarajiwa kutekelezwa katika kipindi hiki. Lakini pia ameelezea mambo ambayo ameona yana umuhimu mkubwa katika kuyaendeleza yaliyotendwa na kipindi kilichopita.

Mhe. Spika, suala la uchumi linategemea sana ukusanyaji wa mapato, na nchi yoyote duniani maendeleo yake hutegemea sana mapato ambayo yanakusanywa ndani ya nchi. Kwa kuwa bado hatujafikia hatua nzuri katika ukusanyaji wa mapato ndio maana wenzetu wengi sasa hivi na hususan inasikitisha sana kwamba hata wasomi wanasema kwamba Tanzania haitaweza kuendelea kama hatutokuwa na misaada kutoka nje, hilo ni kosa kubwa sana.

Mimi Mhe. Spika, nina imani kabisa kwamba hii ndio njia pekee ambayo itaweza kutusaidia kujing'amua kutokana na matatizo ambayo tuliyonayo, hebu tuwaonyeshe kwamba tunaweza bila ya wao.Kwa sababu tumekuwa tunawategemea sana wafadhili, sasa wameanza kuingia ndani ya nyumba zetu, wanatufundisha nini cha kufanya. Wenzetu bahati mbaya ndugu zetu wanaliunga mkono hili, na wanatetea, kwa kweli ni hatari kubwa sana katika maendeleo ya Taifa letu.

Mhe. Spika, niseme katika kipindi kilichopita tulizungumzia sana suala la ukusanyaji wa mapato na tuliomba hapa ndani ya Baraza kwamba, sasa mapato yawe yanakusanywa kwa njia ya *electronic*, hiyo itawezesha sana mapato yale yasivuje. Kwa bahati nzuri kuna baadhi ya maeneo tayari kazi imeshaanza kufanywa, lakini *speed* yake haitoshi. Tunachokitaka ni kwamba katika kila eneo linalokusanya mapato basi njia hizi ambazo zitasababisha kwamba hakutokuwa na uvujaji wa mapato zitumike.

Mhe. Spika, kuna wengine hawazitaki hizi wanaweka sababu zilizokuwa sio za kweli na hii ndio inayotusababishia tunarudi nyuma. Nasema kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu hakuna lisilowezekana. Suala hili namuomba sana Mhe. Rais alisimamie na ninaamini mimi napato yetu yatakapokusanywa vizuri, basi naamini kwamba mambo mengi tutaweza kufanya wenyewe. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naiomba serikali hili litekelezwe haraka iwezekanavyo.

Jengine Mhe. Spika, ninalotaka kulizungumzia katika suala hilo hilo naomba nikumbushie kitu kimoja, kinachotokea na hasara nyingi ambazo tunazipata serikalini kumekuwa na manunuzi mabaya. Sheria ipo lakini manunuzi ya vifaa yamekuwa ni mabaya hayako kwenye *standard*. Serikali inatiwa hasara na nimeshukuru sana hotuba hii, Mhe. Rais, amesema hatokuwa mvumilivu tena. Lakini nataka niwaambie, kwa sababu sisi hapa kati yetu ndio watakaokuwa viongozi wa wizara na watakaokuwa mstari wa mbele kumsaidia Mhe. Rais, nawaombeni sana nyinyi ambao Mwenyezi Mungu atawajaalieni mtaingia katika nafasi hizo, nawaombeni sana mlisimamie hili, fedha nyingi za serikali zinapotea kwa sababu ya ununuzi holela wa vifaa.

Mhe. Spika, hapa katika kipindi kilichopita tulizungumzia suala zima la kununua samani katika maofisi. Tukasema kwa nini hakiwezeshwi Chuo cha JKU, kule kuna ufundi maalum walionao wanachonga *furnitures* za maofisini. Lakini kwa nini *furnitures* zote zitoke China, halikufanyiwa kazi hilo, na tulisema basi tuwawezeshe JKU ili waweze kuwa na mashine ambazo watatoa samani bora. Lakini inasikitisha sana kwamba hilo jambo mpaka leo halijafanyika na hiyo itapunguza ununuaji wa samani ambazo sio bora, lakini pia itapunguza fedha ambazo tunazitumia kwa kununua vifaa hivyo. Sasa ningeiomba sana serikali suala hili lisimamiwe.

Mhe. Spika, jengine ambalo linahusu sana suala zima la uchumi na bidhaa za ndani. Mhe. Spika, katika kitabu cha Mhe. Rais nimeona kwamba katika suala la uwekezaji vitega uchumi, kumekuwa na mipango mizuri sana ya kuhakikisha kwamba kuna miradi mingi, hususan kama ya ujenzi wa hoteli na miradi mingine ambayo imetajwa hapa. Mhe. Spika, naiomba sana serikali, utayarishwaji wa mipango ya uwekezaji katika maeneo haya yaende sambamba na kutoa taaluma, alizungumza Mhe. Mmanga, hapa kutoa taaluma kwa wajasiria mali yaende sambamba, ili basi wajasiriamali wetu wa ndani wawe na bidhaa bora zitakazoweza kuuzika kwa wawekezaji hawa.

Mhe. Spika, hilo ni tatizo, kina mama wengi sana wanazalisha bidhaa ambazo bado ni duni, na matokeo yake ni kwamba kina mama wale wanajishughulisha na kazi zile wanatupa muda wao mwingi, pamoja na fedha zao. Lakini bidhaa zile hazinunuliki katika maeneo ambayo wanataka kuzitumia. Sasa ningeomba sana kinamama wawezeshwe lakini pamoja na vijana, hizi zitakuwa ni ajira tosha kwa vijana na akinamama.

Kwa hivyo, ningeomba sana hilo serikali iliangalie upya na iwe basi hawa wawekezaji ikiwa kama sisi tutaona kwamba hilo jukumu hatuwezi kulichukua, tukubaliane na wawekezaji wanapokuja kuwekeza waweze vile vile kuwekeza katika *skills human resources* zetu, wawekeze huko pia ili kuhakikisha kwamba wananchi wanafaidika katika uwekezaji huo. Hilo naamini mimi kwa wawekezaji linawezekana. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nafikiria suala hilo serikali ikijipanga vizuri na naamini kwamba itajipanga vizuri na litaweza kufanyiwa kazi.

Jengine Mhe. Spika, jengine ambalo nataka nilizungumzie ni suala zima la elimu. Mhe. Spika, kama mjumbe mwenzangu aliyepita hapa amelizungumza na kwenye hotuba ya Mhe. Rais hapa inasema kwamba, serikali yake imejipanga katika kuhakikisha kuwa elimu bora inatolewa, kwa maana hiyo Mhe. Spika, mimi naamini kwamba tuna wataalamu wa kutosha wa kuweza kusimamia ubora wa elimu hapa Zanzibar, naamini hilo kabisa. Lakini Mhe. Spika, lazima Waswahili wanasema; "kata pua uunge wajihi". Tuna tatizo kubwa la vifaa katika maskuli yetu, pamoja na skuli zetu kuwa mbovu, pamoja na kuwa hatuna maabara za kutosha, pamoja na kuwa hakuna motisha kwa walimu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ningeomba sana serikali, na ninasema hili kwa moyo wa dhati kabisa, hebu tumfuateni Mhe. John Pombe Magufuli, tukate baadhi ya matumizi ambayo hayana umuhimu, ili tuweze kutekeleza yale mengine ambayo ni muhimu kwa Taifa letu. Tuna shughuli mbali mbali ambazo tunazifanya ndani ya serikali. Kwa mfano sherehe, tunaweza kufanya sherehe ikawa ya kitaifa lakini tukafanya katika maeneo, zikawa sherehe hizo ni ndogo, lakini tukachagua kila baada ya kipindi fulani ndio tunafanya sherehe kubwa, hilo litatusaidia sana kubana matumizi. Kwa hivyo, ningeiomba sana serikali, kwa kuwa tuna haja kubwa na kwa kuwa sasa hivi umeshafika muda wa kujitegemea wenyewe, na kutokana na hotuba hii inaonesha Mhe. Rais ndio azma yake, tunakwenda mwendo wa kujitegemea wenyewe. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ningeomba sana Mhe. Spika, katika yale makusanyo ambayo fedha ambazo tutaziweka zilizotokana na vile vitu ambavyo tumepunguza tupeleke kwenye elimu, ili tuboreshe elimu yetu. Watoto wanataka kusoma, vijana wengi sasa hivi wamehamasika katika kusoma. Kwa hivyo, naiomba serikali iangalie umuhimu wa hilo na basi tuone iko haja ya kukata matumizi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Rais, hapa alisema kwamba kuna watu wanatengeneza safari na maposho. Hilo ni kweli kabisa Mhe. Spika, na linasikitisha sana kuwa linafanyika na sisi tunaofanya mambo hayo wananchi wanatuona. Unapoingia katika nafasi yoyote, mabadiliko yako ya maisha ulivyokuwa nyuma na ulivyo sasa watu wanaona. Mimi nimefurahi kwamba kutakuwa na sheria ya maadili ya wafanyakazi. Nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wenzangu tusitumie nafasi hii tuliyopewa, ambayo tumeaminiwa na wananchi basi tukaitumia vibaya kwa kujinufaisha wenyewe, tutakuwa tunatenda dhambi kubwa sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Rais, alizungumzia suala la rushwa katika hotuba yake. Hakuna mjumbe hapa kati yetu sisi asiyeichukia rushwa, lakini bado tunaipokea na bado tunaitizama na tunainyamazia. Rushwa tunajua kwamba ni 'adui wa haki'. Nampongeza sana Mhe. Rais kwa maneno yake aliyosema mpaka ameweza kunukuu *Qur-an* pamoja na hadithi ya Mtume Mohammad (*S.A.W*), kwa kuona kwamba rushwa haina nafasi katika maendeleo ya wananchi wake na isiwe na nafasi katika maendeleo ya wananchi wake. Tukiendelea kuwa tunapokea rushwa na tunajilimbikizia sisi basi watu wanakosa imani na sisi. Kwa hivyo, naomba Baraza hili liwe mfano, naiomba serikali ya Dkt. Ali Mommed Shein, inayokuja na mawaziri watakaochaguliwa wawe wasafi, hivyo, tuhakikishe kwamba suala la rushwa kwao liwe ni mwiko kwa ajili ya kumsaidia Mhe. Rais wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sina mengi zaidi, kwa sababu yangu yalikuwa ni machache sana, isipokuwa naomba kusema kwamba hotuba hii ya Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein ni dira ya maendeleo ya nchi yetu. Lakini, hii pia inatuonesha au inatupa muongozo sisi Waheshimiwa Wawakilishi ni wapi tuwaangalie sana, kwamba ni kitu gani tukifuatilie, ili kumsaidia yeye kwa sababu sisi ni wasaidizi wa Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein. *(Makofi)*

Sasa kama tunataka na tumekubali kumsaidia Mhe. Rais wa Zanzibar basi kitabu hiki nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe, kiwe ni kitabu ambacho kila mara tunarudi na kukitazama ili tujue tumeelekezwa nini. Kwa kweli, ni muhimu sana kwani huu ni muongozo na ndio ambao utatufikisha katika maendeleo mpaka kufikia mwaka 2020. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa muda wako ulionipa. Vile vile, mwisho kabisa nikupongeze na wewe kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Baraza hili kwa kishindo kikubwa na ninakuombea Mhe. Spika, uuweze uspika wako na Mwenyezi Mungu akujaalie uwe unashirikiana na Waheshimiwa Wajumbe wako pia na akujaalie mema katika kazi zako kwenye kipindi hichi mpaka kufikia mwaka 2020. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mgeni Hassan Juma, ahsante sana. sasa naomba nimwete Mhe. Shadya Mohamed Suleiman na Mhe. Modlen Siras Castico ajiandae.

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kuweza kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia machache katika hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein.

Kwanza naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha mchana huu kusimama hapa nikiwa katika hali ya uzima na afya njema. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, naomba nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kuwapongeza wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba kwa imani yao juu ya yangu kwa kuweza kunirudisha tena katika Baraza lako tukufu kwa mara ya pili. *(Makofi)*

Nikiendelea na pongezi zangu naomba nichukue nafasi hii kukupongeza wewe Mhe. Spika, binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Mhe. Spika wa Baraza letu tukufu. Vile vile, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Naibu Spika pamoja na wenyeviti wetu wapya wa Baraza hili na ninawaombea kwa Mwenyezi Mungu awape uwezo pamoja na mafanikio katika kuendeleza Baraza letu tukufu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda tena kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi za vishindo na wananchi wa Zanzibar na wameonesha imani kubwa juu yao. Kwa hiyo, tumuombe Mwenyezi Mungu ampe hekima, busara, umri pamoja na afya njema kwa ajili ya kuweza kutekeleza kazi zake katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niseme kwamba hotuba ya Mhe. Rais imekamilika vizuri, yaani imetimia na wala haina dosari, isipokuwa jambo kubwa kwetu ni kuichangia kwa ajili ya kumpongeza Mhe. Rais. Lakini hilo Mhe. Spika, halitoshi la kumpongeza pamoja na kuichangia tu, isipokuwa jukumu letu sisi Mhe. Spika, ni kumsaidia Mhe. Rais pamoja na wale mawaziri watakaoingia katika serikali hii tuwe kitu kimoja kwa ajili ya kumsaidia Rais wetu, ili tupate mafanikio ya nchi yetu na kuzidi kusonga mbele. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nianze kuipongeza serikali kwa kuweza kuboresha maeneo mengi ya kiuchumi ambapo amezungumzia Mhe. Rais katika kitabu chake hiki kwenye sehemu za Fumba na Micheweni na naomba kugusia kidogo sehemu ya Micheweni.

Kwa kweli, tunashukuru sana serikali kwa kuliona hili na tunaifahamu sote hali ya Micheweni ilivyo, yaani kisiwa kile bado ni cha hali ya dhiki kidogo. Kwa hivyo, naamini kwamba sehemu ya Micheweni itakapoboreshwa kwa kuwekwa mambo mbali mbali wananchi wetu hawa watapata ajira na kuweza kujikimu katika maisha yao ya kila siku.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba niende kwenye zao la karafuu. Vile vile, hapa naomba nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kuboresha zao la karafuu na serikali itaendelea kuwalipa asilimia 80 wananchi wake. Kwa kweli, hilo ni jambo la kutia moyo pamoja na faraja, pia, naamini kwamba wananchi wetu zao hili wanajua kuwa ni uti wa mgongo wa nchi yetu ambapo tunategemea mapato halitokwenda tena kimagendo, isipokuwa naamini kwamba wananchi wote watatumia fursa hii kupeleta zao hili katika taasisi husika ya *ZSTC*. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nitumie nafasi hii kuiomba serikali, kwamba wale wote wanaotumia njama za kuichoma mikarafuu kisiwani Pemba, nalikemea sana pia ninaomba serikali iwachukulie hatua wale watu wote ambao ni waharibifu wa maisha ya nchi yetu, kwa sababu kama tunavyofahamu kwamba karafuu ndio tegemeo letu Zanzibar. Kwa hiyo, naiomba serikali iwachukulie hatua wale wote wanaohusika kwa njia moja au nyengine vyombo vya sheria vifuate mkondo wake. *(Makofi)*

Sasa naomba nizungumzie kuhusu sekta ya maji. Mhe. Spika, naipongeza sana serikali kwa kupeleka maji mijini na vijijini. Lakini nataka niseme kwamba tatizo la maji bado ni mtihani, yaani sehemu nyingi zina ukosefu wa maji, wananchi hawapati maji na wanasumbuka.Kwa hiyo, naiomba serikali izidi kulitafutia ufumbuzi suala hili la upatikanaji wa maji safi na salama.

Mhe. Spika, katika kitabu cha hotuba ya Mhe. Rais pia imezungumzia kuhusu suala zima la utalii, kuboresha Chuo cha Maendeleo ya Utalii Maruhubi, tunafahamu kwamba hivi sasa chuo hiki kinatoa mpaka ngazi ya *diploma* tu. Kwa hiyo, tunaiomba serikali iongeze juhudi zake pale kwa ajili ya kupatikana wataalamu tuweze kutoa *degree* pamoja na *master*, ili wananchi wetu wapate elimu pamoja na ajira. *(Makofi)*

Kwa kweli, kama tunavyofahamu Mhe. Spika, kwenye mahoteli wananchi wetu nafasi za *manager* na nyengine kubwa ama za maamuzi hawazipati kutokana na ukosefu wa elimu. Kutokana na hali hiyo, tunaiomba serikali izidishe juhudi pamoja na bidii katika suala hili zima la utalii na tukiangalia kwamba utalii ndio uti wa mgongo wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa naomba niende kwenye mazingira na hotuba ya Mhe. Rais imezungumza suala zima la mazingira. Mhe. Spika, kipindi cha miaka iliyopita kwenye miaka miwili na nusu nilibahatika kuwa Mjumbe wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa, katika kusimamia ofisi hizo, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilikuwa ni miongoni mwa ofisi tunazozisimamia, ambayo ofisi hii ilikuwa inashughulika na mambo ya mazingira.

Katika majukumu yetu kamati hiyo tulibahatika kwenda Pemba na tulivuka kwenda mpaka kisiwa Panza. Mhe. Spika, kisiwa Panza kinasikitisha na hali sio shuwari na wananchi wakati wowote isipokuwa Mwenyezi Mungu awanusuru, lakini hali sio nzuri. Kwa hivyo, ninaiomba serikali ichukue juhudi za makusudi kwa ajili ya kukiokoa kisiwa kile.

Vile vile, naomba nitumie fursa hii kuwataka wananchi wa kisiwa Panza, kwamba waache kukata miti ovyo, ujenzi wa kiholela pia nao wapunguze, kwa sababu mambo haya yanachangia katika kuhatarisha mazingira. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nimuunge mkono kaka yangu Mhe. Hamad Rashid Mohamed, wakati alipokuwa akichangia alilizungumzia suala zima la wananchi wetu katika kuteseka kwenye kipindi hichi baada ya kumaliza uchaguzi mkuu. Mhe. Spika, ni ukweli usiopingika wananchi wa kisiwa cha Pemba wako tabuni, mashakani ama idhilani, yaani wanasusiwa si kwenye magari, wala kwenye maduka, kwa kweli kukicha wewe unapata simu leo kuna hili na lile. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, tunaiomba serikali jambo hili walichukulie hatua, ikiwa dereva amesusa kuwapakia wana-CCM, nafikiri leseni tumempa sisi kutoka mawasiliano, basi tuchukue leseni yetu akae nyumbani na aamue atakalo amua na ikiwa ni muuza duka basi leseni tumempa sisi, na katika hili pia tunaiomba serikali achukuliwe hatua. Mhe. Spika, tumeshachoka na sasa tunaiomba serikali sasa basi, kwa sababu wananchi wetu wananyanyasika na kwa nini wanyanyasike wakati serikali ni yetu, hivi tuna hofu nini au tunaogopa nini. Kwa maana hiyo, naiomba serikali jambo hili walifanyie haraka sana na kuwachukulia hatua hawa wote wenye vitendo hivi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimalizie kwa kuvipongeza vikosi vyetu vya SMZ pamoja na SMT. Kwa kweli, vikosi hivi vyote vya pande mbili vimeshirikiana kwa umahiri mzuri sana katika kipindi cha uchaguzi na hadi hivi sasa bado tumo katika amani na utulivu na wao wakiwa bado wanaendelea katika kulinda raia pamoja na mali zetu. Kwa hiyo, naomba kutoa pongezi za pekee kwa vikosi vyetu hivi pamoja na kuwaombea kila la heri Mwenyezi Mungu awape mafanikio mema katika kazi zao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya hayo machache kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba, naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Rais kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Mhe. Shadya Mohamed Suleiman, ahsante sana kwa mchango wako na sasa naomba nimwite mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo Mhe. Modlen Siras Castico, tafadhali.

Mhe. Modlen Siras Castico: Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba nichukue nafasi hii ya kumshukuru kwanza Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi ya kuweza kuwepo miongoni mwenu na pia kupata kibali machoni kwa wananchi wote na hasa kwa Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein, ambaye aliona naweza kusaidia kuchangia katika maendeleo ya serikali. *(Makofi)*

Vile vile, nisiache kuwashukuru wanachama wote wa Chama cha Mapinduzi, naweza niseme hivyo, kwa sababu ndio chama ambacho kimechukua dhima kubwa sana kwa ajili ya usalama wa nchi yetu. Pia, ni watu ambao hawakutaka kubadilika hata pale tulipokuwa katika misukosuko ya masuala ya kurudia uchaguzi, walikuwa tayari kuhakikisha demokrasia inafanyika pasipokuwa na hofu ya kutishwa na mataifa ya nje. Naomba niwapongeze wote kuanzia watu wa ngazi za chini na juu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nimpongeze Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi. Hivyo, napenda kusema kwamba Mheshimiwa, unastahili kupata nafasi hii tena kwa mara nyengine, kama kulikuwa na mtu ambaye anapigwa madongo, kusemwa na watu wa upinzani pamoja na maneno mengi kama angekuwa hana moyo wa kustahamili ilikuwa mmoja wapo ni wewe. Kwa kweli, majina yote ulipewa lakini ulistahamili na Mwenyezi Mungu aendelee kukupa moyo huyo uendelee kutuongoza. *(Makofi)*

Nikiendelea na pongezi sasa naomba nivipongeze vyombo vya ulinzi na usalama vilivyoshirikiana, vyombo vya serikali, Tume ya Uchaguzi pamoja na wale wote walioona inafaa Zanzibar kubakia katika hali ya amani. *(Makofi)*

Kwa kweli, kama kuna mtu anasema kwamba huwezi kujua lini utaanza kupata sifa basi ni ile siku ambayo Mwenyezi Mungu ambayo ameikusudia. Hivi sasa, kila mtu anayetaka kuzaa mtoto wa kiume anaambiwa humwiti Jecha, yaani utaona imekuwa kama ni utani, lakini ni mtu ambaye anastahili heshima na tunapenda kumshukuru kwa kuwa na moyo wa uzalendo, kwa sababu pasipokuwa na uzalendo, mtu yeyote hawezi kutetea nchi yake kwa hali na mali kwa gharama yoyote itakayokuwepo.

Mhe. Spika, naomba niwashukuru akinamama wenzangu, ndugu zangu, familia yangu pamoja na viongozi walioko karibu na mimi ninakoishi Kiembesamaki na shehia iliopo pale, kwa sababu ninaishi katikati ya ndugu zangu ambao ni wapinzani, lakini kwa pamoja tunaendelea kufanya kazi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hotuba hii ilioko mbele yetu imeanza kuisikiliza hata kabla ya kuteuliwa. Wakati alipokuwa akizungumza Mhe. Rais wa Zanzibar, alizungumza mambo mengi sana ambayo yalikuwa na vipendele zaidi ya 36, ambavyo vingi wenzangu wameshavieleza na wamechangia kwa ufafanuzi.

Lakini yangu ni machache tu katika kuongezea kwa wale wenzetu ambao tayari wameshachangia na nikisema naanza kuichambua naweza kuanza mwanzo mpaka mwisho.

Jambo jengine ambalo limenifurahisha katika hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar ni pamoja na kuzungumzia suala la uvuvi. Kwa kweli, Zanzibar ni nchi ambayo tumezungukwa na maji na maji ndio mali yetu halisi ama ni mashamba yetu na hiyo ndio rasilimali yetu. Sasa ikiwa uvuvi utarekebishwa na kusaidiwa watu kupewa mafunzo kwa wale wanaohusika pamoja na wale wenye kufanya masuala ya mwani, nadhani tutakuwa tumepata heshima kubwa. Nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kusema kwamba hawa watu watapewa nafasi ya kujengewa majengo pamoja na vyumba vya kutunzia samaki, kwa sababu mara nyingi wamekuwa wakivua samaki wanaotumika kwa siku moja na siku ya pili ukienda sokoni samaki hawatoshi. Lakini kutokana na hali hii ameona jambo ni zuri zaidi.

Mhe. Spika, pia, kuhusu suala la ardhi Mhe. Rais wa Zanzibar amezungumzia sana suala hili, aidha serikali itaendelea na kazi ya upimaji wa viwanja, utoaji wa hati kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya kiuchumi, kijamii pamoja na kuzingatia mpango wa kitaifa wa matumizi bora ya ardhi, ambayo hayo tunaendelea kuamini kwamba hayatakuwa na ubaguzi, wakati watu watakapokuwa wanaomba nafasi ya kupata ardhi kwa matumizi wanayohitaji ambayo yatafaa kwa ajili ya Taifa, sidhani kama kutakuwa na bughudha wala mashindano ya kusema kwamba labda kile unachoomba hakifai.

Vile vile, katika masuala ya miundombinu wala hayasemeki, labda mtu asiyeona tukisema maendeleo hakuna Zanzibar, nadhani atumie *microscope* ili aweze kuona vizuri. Kwa mfano, barabara zimejaa, ndege ukienda Pemba, yaani unaweza kufanya kazi Zanzibar na unakwenda kulala Pemba na unaweza kufanya kazi Pemba ukarudi kulala Zanzibar, kwa kweli ni kitu ambacho hakina hoja, kinaonekana na usafiri na tumeutumia hata katika kipindi cha uchaguzi, yaani watu wamekwenda usiku na mchana bila ya kuwa na hofu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala la nishati tunaendelea kuona kwamba jinsi gani tunaendelea kupata umeme na ule mgao kidogo umepotea na tunaendelea kwa amani, kwamba hivi sasa mtu anaweza kupanga mipango yake na kutumia vifaa vya kisasa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

Mhe. Spika, suala la uchimbaji wa mafuta kama alivyokwishasema Mhe. Rais wa Zanzibar mwenyewe, pia, ninamshukuru Mhe. Rais Mstaafu wa Serikali ya Jamhuri ya Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kuhakikisha kwamba suala hili limekwisha, kwa sababu lingekuwa kama ndio jambo la kutushikia ubavuni, yaani kila ukisema wapinzani hivi sasa hawatakuwa na hoja. Hivyo, kama ni mafuta tunaomba Mwenyezi Mungu atupe mafuta na kisima kitakachokuwa kinatosha na wala kisikauke, hilo shimo la mafuta lielekee Zanzibar na wala lisielekee mahala pengine popote na Mwenyezi Mungu atusaidie katika hilo, ili tuweze kuwa na uhakika wa kuweza kupata mafuta. *(Makofi)*

Jambo jengine ambalo limenifurahisha sana ni pamoja na masuala ya *DNA* katika masuala ya afya. Mhe. Spika, *DNA* itasaidia sana kupunguza unyanyaswaji wa watoto pamoja na wanawake wanaopewa mimba na halafu mwanamme anaruka. Sasa kamba ya kuwakamata na kuwafananisha kwamba hizi kazi nzuri wanazofanya za kuongeza Taifa zitajulikana kwa uhalali. *(Makofi)*

Nikiendelea katika sekta ya afya ni kwamba amesaidia sana Mhe. Rais wa Zanzibar, amepunguza gharama za matibabu na hasa kwenye vyombo au vifaa vikubwa kama vile *CT-Scan* pamoja na *Ultra-sound*. Kwa mfano, ukienda kwenye *private hospital* hivi sasa Zanzibar iko kwenye shilingi 400,000/- kwa ajili ya kupata huduma kama hiyo, lakini kwa hospitali yetu ya Mnazimmoja ni shilingi 100,000/-, ambapo mtu anaumwa lakini hawezi isipokuwa kuna sehemu chache ambazo gharama zao ni kidogo na mahitaji yanakuwa ni mengi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nimenipa matumaini kuhusu mpango wa pencheni kuanzia watu wenye umri wa miaka 70 na kuendelea watafikiriwa. Kwa kweli, hili ni jambo ambalo linatia moyo sana, kwa sababu hata wazee wenzangu wataanza kuwa na matumaini ya kuishi vizuri, ili angalau waje wapate hizo pencheni pamoja na kujitunza afya zao na kuendelea kukiunga mkono Chama cha Mapinduzi, kwa sababu ndio chama chenye sera zinazoeleweka pamoja na kutekelezeka.

Mhe. Spika, napenda kusema kwamba nimpongeze tena Mhe. Rais wetu wa Zanzibar kwa kuwa na hofu ya Mwenyezi Mungu ndani yake, ametuongoza vizuri kwa amani na utulivu, pia, amewanyamazisha wale wote waliodhani kwamba itakuwa ni kipindi cha kukoga damu Zanzibar hakiko. Kwa hivyo, tunaendelea kuomba amani iendelee na Mwenyezi Mungu atusaidie. *(Makofi)*

Napenda pia kuwashukuru sana watu wote waliohusika kwenye masuala ya kuombea amani kwa ajili ya nchi yetu ya Zanzibar na Tanzania nzima, kuna watu walikuwa wanakesha wanaomba usiku na mchana kuhakikisha kwamba tumepita salama. Naamini viongozi wote hapa mlipo kila mmoja anapofika jioni anasema ahsante Mungu, maana yake hata nyie kufika hapa mmependeza sana waheshimiwa na hasa tukiwa ndani yetu tumepata na viongozi wengine ambao wametoka kwenye vyama vya upinzani, imenitia moyo sana, na kuona hekima ya Mheshimiwa, sio ya kawaida, angekuwa mtu mwengine angesema wale sitawatambua kwa sababu hawakukidhi haja ya kuweza kupata heshima hiyo.

Hapa tunaye *AFP* ambayo nilikuwa namuuliza hapa jirani yangu yuko hapa Mheshimiwa, anapendeza kabisa na ndevu zake, kuna ndugu yetu *ABC* amechangia pale, kuna *TADEA* amechangia, ni vitu ambavyo vinatia moyo, nadhani Zanzibar itakuwa ni kisiwa cha kujifunzia siasa, tulipokuwa kwenye Serikali ya Muungano ya umoja walikuwa wanadhani hatutofika hata leo lakini tumefika na tumemaliza.

Mhe. Spika: Una dakika mbili Mheshimiwa.

Mhe. Modlen Siras Castico: Dakika mbili ahsante sana, wamemaliza na sasa hivi tunaanza hatua nyengine ambayo kwa bahati nzuri hata wale waliokuwa na hofu kwamba wasingeweza kuingia Barazani Mungu amewabariki wameingia.

Mhe. Spika, naunga mkono hotuba ya Rais kwa asilimia mia, ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hapo awali niliashiria kwamba Mhe. Modlen Siras Castico kwamba, ndio atakuwa mchangiaji wa mwisho, lakini bado tuna zaidi ya robo saa hivi ambayo ingeweza kumtosha mchangiaji mmoja wa mwisho ili tuwapate wengine jioni, kwa hivyo, kama atakuwa anaweza kuchangia sasa hivi Mhe. Suleiman Sarahan, basi nafikiri ukiitumia nafasi hii itakuwa vizuri sana.

Mheshimiwa, karibu sana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, mimi jina langu naitwa Suleman Sarahan Said, natokea Jimbo la Chake Chake Pemba, Chake Chake Mjini pale. Kwanza awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu aliyeumba mbingu na ardhi na vilivyomo vyote, tumtakie kheri Mtume wetu (*S.A.W*), tuwatakie kheri ndugu zetu na wazee wetu waliotangulia mbele ya haki Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi *Amin*.

Mhe. Spika, napenda nitoe shukurani zangu kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, nimpe hongera sana kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kwa wananchi wake wa Zanzibar, Mwenyezi Mungu ampe maisha marefu na ampe kila hekima ya kuongoza nchi hii. Pia, nikutakie kheri wewe Mhe. Spika, kwa ushindi wako mkubwa, nakutakia kila la kheri na viongozi wenzako wote walio karibu yako. Pia, nitoe shukurani kwa mama yangu mpendwa Fatma Suleiman Salum na mama zangu wengine ambao wameninyonyesha kama watatu hivi; Maymuna na Zuwena. Lakini pia Mhe. Spika, nitoe shukurani kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Chake Chake, nawapa hongera sana nawatakia kila la kheri aliye mgonjwa Mwenyezi Mungu ampe nafuu na aliye na mashaka Mwenyezi Mungu amuondoshee.

Mhe. Spika, mimi kwa kuchangia hotuba ya Mhe. Rais, kwa sababu ya muda, nilikuwa nataka nitoe tu ufafanuzi kidogo kwa hali niliyoiona, tumesoma hotuba lakini pia na Mheshimiwa mwenyewe kama mwenyewe alionekana kwa muonekano wake, mimi nataka niseme kwamba Dk. Ali Mohammed Shein katika hotuba yake na yeye mwenyewe amesema imetosha, kwa hivyo, nataka nichukue tu na kuwaelekeza wale watendaji na watu wote ambao hawamtendei mema Dk. Ali Mohammed Shein, ni kwamba amesema basi, ataanza majipu mpaka vipele atavitumbua. Tumekuwa tukimsema kwa muda mrefu na watu wengi wakimsema sema ni mtu mtulivu, mtu nini, lakini utulivu una mwisho wake na kila jambo lina mwisho wake sasa hivi kazi tu, kwa hilo nimeisifu hotuba hiyo kwa sababu Dk. Ali Mohammed Shein ameonesha mwangaza wa hali ya juu na jinsi anavyowapenda wananchi wake hasa walio masikini nini atawafanyia katika kipindi cha miaka mitano iliyobakia.

Mhe. Spika, mimi nataka niseme kwamba matatizo yaliyo mengi katika sehemu zetu mara nyingi hata sisi tunaokwenda kwenye wajumbe ambao tunatoka katika majimbo umasikini kule umekithiri, na tatizo kubwa tumeliona kwamba nchi yetu haiwezi kwenda haina biashara, wala viwanda dhidi ya Serikali. Mishahara yetu ya Serikali au mishahara yetu ya wafanyakazi ndio inayoendesha nchi kwa muonekano unaoonekana, kama serikali haitoe pesa basi na nchi haina pa kwenda, wananchi wake wengi wanakuwa hawana matumizi, hili jambo nimeliona na nimeona katika hotuba kwamba Mheshimiwa ataliondoa kutokana na kazi za nje ambazo zitafanyika,. Kwa hivyo, hapa nilikuwa namshukuru Dk. Ali Mohammed Shein ameliona hilo.

Lakini Mhe. Spika, nataka niseme na nyongeza nyengine hili suala la wafanyakazi ambao wameshafika miaka 60, halafu bado wanaongezwa muda, mimi nilikuwa naliona Mheshimiwa wale vijana wetu ambao wameshamaliza masomo wanasubiri muda na wanasubiri nafasi za kazi tutakuja kuwatumia lini wale, hili suala Mheshimiwa tulitakiwa tulitizame vizuri, mtu kama ameshafika miaka 60 ukimtizama na ukimpima ana sukari, ana chumvi, ana kila kitu, huyo tumuweke pembeni Mheshimiwa, tuwatafute vijana tufanye kazi sio kama ana mazoea yule na mwengine atazowea.(*Kicheko*)

Lakini pia Mhe. Spika, nataka niseme tokea enzi hizo mpaka leo ili uwe Mwakilishi, hili sijui niseme uwe nani, ukitaka kujitapa useme nitawapa maji, barabara, nitawapa sijui na kitu gani, hili suala liondoke, barabara

ikitengenezwa muda wa miaka 20 haiji tena, mimi ninavyofikiri barabara za Zanzibar Mheshimia hazifiki hata kilomita elfu moja zote, hakuna haja ya kuzisubiri barabara hizi kila siku tukenda kuwaombea watu, hizi barabara zingetengenezwa kwa wakati mmoja, hayo mabarabara makubwa kama ni msaada tukaomba kwa wenzetu Wabara hapo, wana barabara moja tu ambayo tunaweza kugawana Zanzibar nzima na Pemba.

Kwa hivyo, tugawaneni ziondoke kwenye kuomba kura na maji kama alivyosema Mhe. Shadya, Mhe. Spika, maji Zanzibar yapo na tukiyapasua tutazama, kwa nini maji hayapatikani vya kutosha, kila siku tatizo ni maji, umeme na barabara, umeme sasa hivi umekuwa mambo mazuri, lakini miundombinu yake sio mizuri, mara unazimwa zimwa, huko kwa wenzetu umeme ukizimwa mtu anaona kama leo ndio Kiyama, saa kwa nini kuwa hatufikii huko. Kwa hivyo, Mheshimiwa, nikisema kwamba utekelezaji wa maji, umeme na barabara tungevifanyia kazi ya ziada hivi tukaviondosha hasa katika hisabu hiyo, tukawa tunafanyia ukarabati tu hilo moja.

Lakini Mhe.Spika, jengine afya inatusumbua sana katika mahospitali yetu, mimi ninavyoona kwamba Serikali inajitahidi sana kutengeneza mambo ya afya, lakini bado majipu yapo kwenye Wizara hizo, ndio ambayo yanatusumbua, madaktari hawapatikani kwa wakati, imekuwa bure ndio bure kweli kweli, na ndio tukawa tumeyapa nguvu mahospitali ambayo yanatumia pesa.

Kwa hivyo, ningeshauri hao watakaopewa dhamana za afya wakatizama hasa mahospitali yetu kwa nini hayafanyi kazi, hapa juzi tu tulikuwa na mfuko wa hifadhi ulikuwa unazungumza suala la Mnazimmoja, Al-Rahma inachukua sijui milioni mia ngapi sijui, wakati pale Mnazimmoja inachukua milioni mia mbili, mabilioni yanakwenda Al-Rahma kwa matibu ya mfuko wa hifadhi, hivi tunakwenda vipi, wakati hawa hawa Al-Rahma wakishindwa wanampeleka Mnazi Mmoja. *(Makofi)*

Kwa hivyo, hili tungeliangalia kama tutaifanyia ukarabati hospitali yetu na mipangilio, pesa hizo za mfuko wa hifadhi zingekwenda pale pale zikasaidia mambo, kwa hivyo, ningeshauri tu watu wa afya wakalitumia hili, hospitali zetu zote kubwa zikafanya kazi na mfuko wa hifadhi na wale ambao wamekata ile *BIMA* yenyewe na pesa zile zinarudi Serikalini na zinafanya mambo mengine kwa hivyo, na hilo nilikuwa naliangalia vile vile.

Lakini Mhe. Spika, nasema watu wote humu ndani tuna habari ya kuwatakia nafuu watu wetu. Mhe. Spika, nyama ya ng'ombe imekuwa ghali shilingi elfu kumi kilo, samaki imekuwa balaa, Mheshimiwa, ng'ombe Bara wanatupwa hawana walaji, hatufanyi mpango wa kuleta ng'ombe kwa meli wakamwagwa hapa ili watu wakala nyama kwa elfu mbili, bado ng'ombe wamekuwa tatu, ikifika Sikukuu hamna ng'ombe ila wako Bara na nafasi zipo, ni wenzetu wale tukiwaambia watatuletea kwa meli na wao watafurahi mifugo yenyewe haina nafasi kule, kila siku wanachinjana kwa mifugo ilivyokuwa mingi, tufanye utaratibu. Wizara ya Kilimo ifanye kazi kuleta ng'ombe, watu waje wachinje hapa kilo elfu mbili watu wote watanenepa, watakuwa wazuri kabisa, mtu akitaka kula nyama hapa Mheshimiwa mpaka ije dhikiri, kwamba leo nyama watu wote waitane, haiwezekani Mhe. Spika, kwa hivyo, na hilo naomba lifanyiwe ukarabati kabisa.

Mhe. Spika, usafiri wa Pemba, Pamoja na kwamba tumepata meli, usafiri wa Pemba haujapatikana wa *Express*, ndege laki nzima masikini ataitoa wapi, hebu tufanyeni hao watu ambao wana biashara hizi ndege ziletwe kubwa, ndege zote zilizokuwepo pale ukiingia ni rehema ya Mungu mpaka unafika wee, ndege injini moja wee unasema; *La haula wala quwwata illa billah*. Mhe. Spika, ndege zilizopo zinatusaidia tu lakini ukiingia wee bwana mpaka unafika mdomo haufiki chini, kuzungumza na mwenzako hutaki, kwa sababu ni ndogo na zinafanya vile kwa sababu ndio zikachukua pesa nyingi, zikija *Boeing* na ndege nyengine ambazo zitasaidia bado uwanja una nafasi Sh. 50 elfu tu mtu atapanda ndege hapa na mapato yataongezeka, kila siku mauzo yangekuwa mazuri.

Lakini sasa hivi tunakaa na meli kutoka asubuhi, Mhe. Spika, wakati ni ukuta, siku nzima mtu anamaliza kwenye meli kutoka asubuhi mpaka usiku, basi kama Wapemba ulivyokuwa unajua wanavyozaa ana watoto 10 ngoja wamlilie humo kwenye meli.Hili nalo litizamwe tatizo la usafiri bado Pemba lipo, kama kuna mfadhili au kuna mtu ambaye anataka kuleta meli za haraka haraka aachiwe kule Pemba bado usafiri ni mzito Mhe. Rais kajitahidi alipoliona hili kaleta meli ile moja, lakini meli moja ndio meli moja, hivi nyengine ukitaka kupeleka gari Pemba kama huna milioni huipeleki wakati hapa ni mahali pa mapantoni, inavyotakiwa tufanye vitu rahisi na laini vya kuwasaidia wananchi wetu.

Mhe. Spika, nasema haraka haraka kidogo kwa sababu najua ulivyonipa muda umenipa bila ya kutosha, nasema na hawa Mawaziri wetu watakaoteuliwa Mwenyezi Mungu akiwajaalia, Mhe. Rais hapa ameshasema kuhusu habari ya kwamba nini wananchi wanataka, ikiwa mtu ana ndugu yake, ana jambo lake anamfumbia macho kwa kuwa ndugu yake, anasema nitakula wapi mtu atalaumiwa, zile pesa zake za mkopo anazozipata amfanyie biashara, lakini pale ikiwa hatufai aondoke, tusitizamane. Mhe. Spika, Wazanzibari sote ni ndugu, kila utakayemtizama ni ndugu lakini kama hatuwezi kazi tuwekane pembeni, wapo vijana wanaoweza kazi wakatusaidia. Kwa hivyo, nasema viongozi watakaoteuliwa wakiona kwamba huyu ndugu yangu nataka nimsaidie na amtafutie nafasi nyengine, hizi nafasi za Serikali za utendaji waachiwe watendea kazi, ndio hali tulivyo sasa hivi.

Kwa hivyo, mimi sisemi sana, naweza kusema na mimi nachukua fursa hii kumpongeza Makamo wa Rais, kwa sasa hivi mimi naweza kusema Balozi simtaji tena Makamo wa Pili, naona wa kwanza hayupo, Balozi ni Makamo wa Rais tu, maana yake Makamo wa Kwanza hayupo, kwa hivyo, ningeshauri kama Bunge litakubali tumuite Makamo wa Rais tu, maana yake naona Makamo wa Kwanza hayupo na ufafanuzi umeshatolewa kwamba hatoteuliwa tena, kwa hivyo, hakuna haja ya kuitwa Makamo wa Pili, tumwambie Makamo wa Rais basi, mimi ningeomba tu hilo kama itawezekana lakini kwa heshima yako.

Mhe. Spika, naona muda sijui kama unakaribia, lakini nitasema kwamba kidogo habari ya vijana kwenye masomo, mimi ninachosema katika vijana sasa hivi elimu yetu hapa hapa Zanzibar hasa elimu hizi za vyuo vyuo imekuwa vigumu vijana wetu kupata na imekuwa vigumu kwa bei, hawa vijana wakiachiwa ndio wanaokula unga, hawa vijana wakiachiwa ndio wenye maneno ya mtaani.

Mhe. Spika, mimi ningeona tungefanya kama vile China wakapelekwa huko maeneo wakasoma zaidi tu kama nafasi haipo, wakalishwa tu kule, yaani wakawa wanasoma na wanalishwa tu, halafu tukitaka tunawachukua tunaleta huku, sio kuwaachia tu mitaani, maana yake tujenge mabweni au mambo makubwa ya kuwaweka vijana waliokwishamaliza *Form IV* na *Form VI* lakini kwa taaluma maalum, kule serikali inapeleka pesa za chakula na kila kitu ili tukitaka wanafunzi waliokwishahitimu tunabeba kule na tunaleta kwenye serikali na mambo mengine, tusiwaachie mitaani, ndio wanaoleta fujo hawa, ndio wenye mahangasha ya kula unga hawa na watakula tu kwa sababu ukishafika wakati akionja unga siku moja anajiona yeye ndiye mfalme...

Mhe. Spika: Naomba utumie dakika mbili.

Mhe. Suleiman Sarahani Said: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi, nawashukuru wajumbe wote waliochaguliwa kwa kura nyingi, Mwenyezi Mungu awasaidie katika majimbo yao, lakini pia nawashukuru zaidi na zaidi wale wote waliochangia kutufanikisha kuwa katika Baraza lako hili tukufu.

Mhe. Spika, Ahsante sana, nakushukuru sana na nawashukuruni wajumbe wote. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsanteni sana Waheshimiwa ambao mmepata kuchangia katika *session* hii ya asubuhi. Waheshimiwa Wajumbe kabla sijasitisha shughuli za leo asubuhi, naomba kwanza nitoe tangazo, nimeombwa niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe kwamba mara baada ya kuahirishwa kwa kikao hichi, basi tukutane ukumbi wa juu kwa elimu ya Benki ya Posta na *CRDB* pamoja na kikao cha michezo.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba pia niwatangazie majina ya wachangiaji ambao wataanza kuchangia jioni ili waweze kuwahi na kuja kuchangia, mchangiaji wetu wa mwanzo Mhe, Jaku Hashim Ayoub, atafuatiwa na Mhe. Haroun Ali Suleiman, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Shamata Shaame Khamis, Mhe. Said Soud Said pamoja na Mhe. Bihindi Hamad Khamis, halafu wataendelea, naomba niwataje hao sita tu wa mwanzo ili waweze kujipanga wawepo katika *session* ya saa 11:00 jioni itakapoanza.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba nisitishe shughuli za Baraza mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 Asubuhi Baraza liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Haroun Ali Suleiman: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuleta tena jioni ya *session* yetu ya pili kuendelea na kikao chetu hiki. Aidha, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema, uzima na *Alhamdulillah* tupo hapa kuendeleza kufanya shughuli hizi kwa niaba ya wananchi wetu.

Pili, naomba nichukue nafasi hii maalum kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ushindi wake alioupata tarehe 20 Machi, 2016 hakika ni kielelezo kwamba wananchi wana imani nae kubwa, sote tuliomuunga mkono na wale wapenzi wetu mbali mbali ambao waliunga mkono katika suala zima la kutupatia ushindi huo.

Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kukupongeza wewe, Spika wetu, Wenyeviti wote kwa kuchaguliwa kwenu kwa ushindi mkubwa mlioupata. Nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili la Tisa kwa kuchaguliwa, kwa kuteuliwa nafasi mbali mbali ambazo *Alhamdulillah* tumelijaza Baraza letu hili. Pongezi maalum kwa wale viongozi wetu, waheshimiwa wetu walioteuliwa jana na leo wameshaapishwa, nawapongeza sana kwani ni watu mahiri na tunatarajia *Inshaallah* tutashirikiana nao kwa hali na mali.

Mhe. Naibu Spika, kilichokuwa mbele yetu ni kuzungumzia na kujadili hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa kweli wataalamu wanasema; *This is a working document,* hiki ni kitabu cha kukifanyia kazi, ninahakika kunahitajia muda mrefu zaidi kukitafakari kitabu hiki. Kwa sababu Mhe. Rais ametumia ujuzi wake, uwezo wake mkubwa sana Mwenyezi Mungu aliomjaalia kipaji chake katika kukitayarisha kitabu hiki. Kitabu hiki kimegusa maeneo yote, sekta zote, kila mahali kusema kweli kimegusa. Maeneo ambayo makubwa yaliyoguswa tuliyoshuhudia sote ni maeneo yanayohusiana na suala zima la amani na utulivu katika nchi yetu (Utawala bora), masuala ya huduma za jamii, uchumi na mengineyo. Kwa ufupi kitabu hiki kimegusa maeneo yote.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli Mhe. Mmanga, leo asubuhi na Mhe. Mgeni, alipokuwa anachangia asubuhi, nasema walinigusa sana kwa sababu walitaja maeneo ambayo tayari nimeshayaorodhesha. Kwa sababu suala hili maana yake nini? Hivi sasa tunaamini kwamba wafadhili ndio wafadhili, anaweza kuamua akakupa au asikupe, lakini la msingi sisi wenyewe tusikae tukasubiri kwamba tufadhiliwe. Tujitahidi kufanya kazi kwa nguvu zetu zote ili tuhakikishe kwamba tunapata kujiimarisha na uchumi wetu unaimarika.

Mhe. Mmanga Mwakilishi wa Jimbo la Mkoani alisema kwamba hili maana yake nini? Sisi wawakilishi tuliokuwemo humu ndani, wawakilishi sote tujiulize kila mmoja ana mchango gani ndani ya hotuba ile. Akifika kwenye jimbo lake, kwenye eneo lake, kwenye Mkoa wake au kwenye sehemu yake anayowakilisha je, atizame kule yeye ana mchango gani, aitizame hotuba kifungu baada ya kifungu na si rahisi kupata tafsiri ya moja kwa moja, lazima akae aiangalie vizuri na ikibidi hata akitafuta wataalamu wamsaidie zaidi kukisoma kitabu kile kwa sababu kwa kukaa peke yako kwa siku moja huwezi kukifahamu. Kitabu hiki kimegusa maeneo mengi na maeneo makubwa. Mfano Mhe. Rais alipozungumza suala zima la huduma za jamii, mambo ya afya, mambo ya elimu, maji na mengineyo ni mambo mapana sana haya ambayo yanahitajia kusema kweli uhakika wa kuyazingatia.

Kwa hivyo, sote ni jukumu letu sasa tukiondoka hapa *Inshaallah, immediately* tukafanye hiyo kazi. Lakini nimekusudia kusema *Inshaallah* Mwenyezi Mungu katujaalia Mhe. Rais ataunda serikali watakuwepo Mawaziri na Manaibu Mawaziri, muna sekta zote zimeguswa humu. Kwa hivyo, watu wa afya wakae watizame kitu gani ambacho Mhe. Rais amekigusa, na amezungumzia *performance* yetu ya miaka mitano iliyopita na mwelekeo wetu wa miaka mitano inayokuja, iko *very clear* na ukitizama anaangalia sana utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. Kwanza aliangalia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi iliyopita na hiyo nyengine ambayo inakuja miaka mitano 2015-2020.

Lakini suala la msingi ambalo tunalipongeza sana Mhe. Rais amelisisitiza hapa ni suala zima la amani na utulivu na Mhe. Hamad Rashid, na yeye vile vile alilizungumzia kwa upana sana, hakuna amani, hakuna utulivu kama mahali popote hapatakuwa na salama. Kwa hivyo, tujitahidini sana jambo hili sote tulidumishe na tuliendeleze, suala la amani na utulivu halina mbadala tunashuhudia duniani matatizo chungumzima yaliyokuwepo kwa kukosa amani

hiyo. Lakini Mhe. Rais alizungumza suala hili la amani na utulivu ili tulidumisheni jamani, uchaguzi umekwisha kilichobakia sasa hivi tujenge nchi yetu.

La pili, suala zima ambalo Mhe. Rais amezungumza ni suala zima la huduma za jamii. Suala la afya *Alhamdulillah* tumefika hatua nzuri, hospitali za Wilaya, hospitali kuu ya Mnazimmoja na ile ya Abdalla Mzee zinaimarishwa na zinaendelea kuimarishwa. Kwa hivyo, na sisi huko katika maeneo yetu tutizame huduma gani muhimu wananchi wanazihitajia, kwa sababu tuna vituo vya afya kule, kuna hospitali, kuna *dispensary* kule, kuna vituo mbali mbali vya afya tuviangalie na sisi upande wetu kama ni wawakilishi wa majimbo hayo tutavisaidia vipi, tusingoje miaka mitano inamalizika ndio unakwenda kupitia kuuliza je, mna matatizo gani. Mimi nadhani tuwahi mapema, watu wanasema; ndege anayeamka mapema ndiye anayekula mapema vile vile.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala zima la elimu, tunashukuru Mwenyezi Mungu tumepiga hatua kubwa katika sekta ya elimu na mwenyewe Mhe. Rais anaiangalia sana sekta ya elimu vizuri sana. Lakini hapa tunaomba sana na mwenyewe kalizungumza kuimarisha vituo vya mafunzo ya amali. Vituo vya mafunzo ya amali wenzetu katika nchi nyingi duniani kusema kweli wametoa ajira nyingi sana kwa kuendeleza vituo vya mafunzo ya amali. Mafunzo ya amali kama kile ambacho kimejengwa Mkokotoni, kile ambacho kimejengwa Vitongoji na vyengine vitajengwa Daya, na kitajengwa kingine Makunduchi tukijaaliwa *Inshaallah*. Vituo hivi maana yake nini? Ni kwamba vifundishe mafunzo ya mikono, ya ujasiriamali ili baadae vijana hawa waweze kujitegemea.

Mimi nina imani kubwa kama tukiviendeleza vituo hivi vya mafunzo ya amali Unguja na Pemba, basi tutafika hatua kubwa sana. Na wanajifunza pale kwa muda wa mwaka mmoja au miaka miwili, baadae wakimaliza pale vijana wale basi wanatafutiwa mfuko sasa na *Alhamdulillah* Mhe. Rais ameazisha mfuko wa uwezeshaji ambao wakati ule ulikuwa chini ya wizara ile uwezeshaji. Kuna pesa hizi ambazo za uwezeshaji na Wizara ya Elimu wana fedha maalum kwa vituo vya mafunzo ya amali ukimaliza muda wako katika mafunzo yako unapewa na nyenzo unakwenda kufanyia kazi. Kwa hivyo, ni vizuri sisi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuyasimamie hayo na kuyaendeleza na pale ambapo tunahisi tunahitajia msaada wowote basi tusirudi nyuma kwenda kuuliza pale ambapo tunahisi tutapata jawabu yetu.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la barabara (miundombinu), *Alhamdulillah* tumefika hatua nzuri. Barabara kila eneo Unguja na Pemba imefika hatua nzuri na Mhe. Rais ametueleza nia ya serikali yetu ambayo inakusudia kufanya katika miaka mitano ijayo katika ujenzi wa barabara hizo. Tumpongezeni jamani Mhe. Rais amefanya kazi kubwa, Mwenyezi Mungu amemjaalia ni mtu msikivu, mtulivu hana haraka na maamuzi yake kila jambo ambalo ataliamua matokeo yake tunapata tija ndani yake. Kwa hivyo, sote tumuunge mkono jitihada zake anazozifanya ni kitu cha kupigiwa mfano, na ametuonesha njia sana kwamba sisi tukiwa na kiongozi kama huyu tunaweza tukafika nae mbali sana kimaendeleo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, habari ya ujenzi wa miji mipya, nia ya kuibadilisha Zanzibar na kuwa Zanzibar ya kisasa imezungumziwa katika kitabu hiki. Miji mipya inajengwa katika maeneo mbali mbali, tumeelezwa hapa Fumba, maeneo yale ya Matemwe kule kunajengwa hoteli za kisasa, maeneo ya Mtoni vile vile kunajengwa kule maeneo ya kisasa kabisa, hoteli ya *five star*. Kusema kweli Mwenyezi Mungu atupe umri mrefu na atuweke hai tuje tushuhudie haya na si miaka mingi tutashuhudia, miaka miwili au mitatu hii hii. Pia, bandari zinaendelea kuimarishwa, mfano bandari ya Mpigaduri pale tumeshaambiwa mipango yote imekamilika na Wachina tayari mambo yameshakaa sawa. Tunamshukuru sana na tunamuomba Mhe. Rais aendelee na sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tutawahakikishia wananchi tunamuunga mkono asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, suala zima limezungumziwa la rushwa. Rushwa kama tunavyoambiwa ni adui wa haki. Ni kweli, haielekei na Mhe. Rais amelizungumza kwenye kitabu hiki cha hotuba yake kwamba, amekemea na sio kitu kizuri hata kwenye vitabu vya dini, *Qur-an* tukufu tumeelezwa hayo, kwamba ni kitu ambacho Mwenyezi Mungu anakichukia, tena anakichukia kwa anayetoa, anayepokea na yule anayeshuhudia. Sasa mle imesemwa na anayeandika, ina maana kama kuna na mtu wa tatu hapo.

Kwa hivyo, kwa kifupi rushwa hii imelaanika kila upande; kwa anayetoa, anayepokea na hata yule anayeshuhudia. Jamani jambo hili linadhoofisha uchumi wa nchi sana, hatuwezi kufanya kazi leo maskini ya Mungu vijijini kule hatarajii kitu chochote zaidi ya msaada kutoka serikalini, kwa watendaji. Sasa wewe mtendaji jambo la kulifanya siku moja au pengine nusu saa au robo saa, kwanza anakuja pale unamwambia nisubiri, anakaa nje ya ofisi yako

anakusubiri siku mbili au siku tatu mpaka siku zinapita, njoo kesho, njoo mchana, utasikia tuko mbioni, hamfiki basi mbio hizi.

Mhe. Spika, watendaji lazima wafike mahali hizi mbio zifike mwisho wake katika kuleta maendeleo kwa wananchi wetu, wananchi wana matarajio makubwa juu yetu na tujitahidini sote kwa pamoja, kila mmoja awajibike kwa upande wake. Sisi kama ni wawakilishi tuna wajibu kwa wananchi wetu huko majimboni. Mimi nilisema mwanzo Mhe. Naibu Spika, kwamba tuna wajibu wa kuwatumikia wananchi wetu na hawana pakwenda kama wewe ni mwakilishi, kama wewe ni kiongozi wa eneo lile unawakilisha wanawake, unawakilisha vijana, unawakilisha jimbo, basi usione tatizo kuja watu wakakugongea milango, uliomba nafasi ile kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wale. Simu yako ikipigwa haipatikani, huo sio utawala bora. Hivyo, tujitahidini tutoe mashirikiano makubwa, wananchi hawa wanatusubiri na kama baada ya miaka mitano hatukuwatendea haki watachukua uamuzi wao. Kwa hivyo, ili tusije tukapata maamuzi ambayo hayatatufurahisha sote pamoja na mimi tujitahidini sana.

Mhe. Naibu Spika, suala zima la tenda za miradi mbali mbali, na hili pia ni kichocheo kikubwa cha kupatikana kwa hizo au pengine utoaji wa hizo rushwa. Leo kama kuna kampuni ni nzuri inaweza ikajenga, sasa haiwezekani kwamba basi kuna mtendaji au kuna maofisa fulani nao wanaongeza vitu vyao ndani yake. Haipendezi, matokeo yake wewe unafikiri kwamba unanufaika wewe lakini unaitia hasara serikali. Kuna miradi imekwama sasa hivi tunaijua imekwama, Skuli ya Kibuteni imekwama muda mrefu hatujui tatizo liko wapi, Skuli kama hii ya Kibuteni inajengwa kule Mkanyageni imeshafika hatua karibu kufunguliwa na hii ya Kibuteni ndio iliyoanza mwanzo hatujui mkandarasi yule amefikia wapi. Kwa hivyo, tunaomba sana Mhe. Naibu Spika, masuala haya yasimamiwe vizuri, yanaleta sura mbaya kwa wananchi, tunataka kuona kwamba maendeleo yanapoanza basi yaanze yawe yanaendelea na tufike mahali tujiridhishe sote.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo ningependa kulizungumza Mhe. Rais katika kipindi chake cha uongozi wake wa miaka mitano, kuhusu maslahi ya wafanyakazi amesema na ametuahidi hapa kwamba katika kipindi cha mwaka mmoja kima cha chini cha mshahara hapa kilipo kitafika mpaka 300,000/=. Lakini tujiulize kwani ndio kwanza kazidisha safari hii, uongozi wake wa miaka mitano amefanya mabadiliko ya mishahara mara tatu, jambo ambalo halijawahi kutokezea huku nyuma. Tumpongezeni sana Rais wetu, yameanzishwa maposho mbali mbali kwa masekeretari, kwa madereva na kwa kila eneo nyeti hata masjala wanapata posho maalum. Yote haya ni kuwafanya vijana wetu waweze kufanya kazi, sasa leo bado tunaambiwa kwamba na kweli inawezekana maofisini wanafanya kazi kwa mazoea.

Yaani mtu anaingia kazini pale, watu wanapiga ile honi ikukutie pale kazini, hapana, honi wewe tayari upo kazini, ile saa moja na nusu maana yake nini? Kwa taratibu zetu za kazi honi maana yake inakwambia kwamba saa moja na nusu ndio *official working time*, lakini haina maana kwamba basi honi ndio unapanda baiskeli au gari yako au unakuja mbio unatafuta daladala ukawahi kazini, itakuwa umechelewa sio utaratibu mzuri, sio utawala bora, sio uongozi mzuri vile vile. Sasa wewe umechelewa, waliokuwa chini yako watafanyaje, si watalala. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, tuwajibikeni sote, Mhe. Rais ameshatia nia nzuri yakutuendeleza na kutengeneza maslahi yetu mazuri. Na mimi nina hakika kabisa kwamba haya kayasema na atayafanya kwa sababu Mhe. Rais akisema ndivyo anavyofanya, hata siku moja hajenda kinyume na kauli zake, Mwenyezi Mungu kamjaalia *Inshaallah* aendelee kuwa na kauli kama hizo.

Mhe. Naibu Spika, jengine nataka nizungumze suala zima la uwajibikaji wa ujumla katika suala zima hilo hilo la katika maofisi yetu. Mimi bahati nzuri nilikuwa Waziri wa Kazi na Utumishi na hasa upande wa mahoteli ya kitalii nimepata malalamiko mengi kwamba vijana wa Kizanzibari hawapati nafasi. Siku moja mimi nikawaita Mameneja wale wa mahoteli nikawaambia jamani tatizo lenu ni nini hamuwachukui watu wa Zanzibar. Unajua sababu waliyotoa mimi sikuridhika nayo, kwa sababu nikasema basi mtu mmoja kama kafanya kosa, wote ndio wamefanya makosa yale. Anasema siku ya kwanza anakuja anakwambia mzee wake amefariki, siku ya pili na ya tatu anakuja anakwambia mdogo wake amefariki, mpaka anakuja anakwambia jirani wa ndugu yake, anakwenda vile vile kila siku dharura, kazi zinaharibika matokeo yake ndio hayo sasa, wale hawaridhiki kwa sababu wale wanafanya biashara ya hoteli ili wapate pesa, wapate uchumi uimarike upande wao na upande wetu wa kiserikali. Sasa kama kazi haziendi, hivyo, biashara itakuwa haiendi, tuwajibikeni sana jamani, ndugu zetu tuwahimize vile vile wasichague kazi. Utaona kwamba zile kazi ambazo ni za kufanya Mzanzibari wakati mwengine kapewa mtu wa

Kenya, kapewa mtu wa Uganda au sehemu nyengine, hivyo haipendezi. Hivyo kweli hata kutandika kitanda kunataka kusema Kiingereza au kufyagia kunahitajia Kiingereza.

Pia, sababu nyengine wanayotoa ni kwamba Kiingereza hawezi kujieleza, tunakwenda katika nchi sisi Mhe. Naibu Spika, kama Uchina, Uingereza na kwengineko, wanazungumza lugha zao na tunafahamiana. Tunakwenda kule Ufaransa, unapokwenda hufahamu chochote, ukiambia *bonjour* unauliza kitu gani hiki, lakini wenzetu wanatumia lugha zao na wanaendelea kiuchumi. Kwa hivyo, ajira za vijana zilikuwepo na zipo na zitaendela kuwepo na ndio maana yake Mhe. Rais, akaanzisha mfuko wa uwezeshaji. Mfuko huu wa uwezeshaji maana yake nini? Maana yake ni kuwaendeleza vijana wetu wale ambao kwa bahati mbaya hawakupata fursa ya kupata ajira ndani ya serikali au katika maeneo mengine ya taasisi, matokeo yake mfuko umeanzishwa.

Mhe. Naibu Spika, wewe unafahamu ulikuwa Mwenyekiti wa Kamati ile ya Ustawi wa Jamii na *Alhamdulillah*, vijana wengi wamenufaika. Tukitizama hotuba hii ya Mhe. Rais imesema karibu vijana 25,000 au wananchi 25,000 wamenufaika na ajira hizi, na serikalini katika kipindi kilichopita karibu 5000 wameajiriwa. Lakini nafasi katika serikali ni chache hatuwezi kuajiri watu wote, matokeo yake Rais ameanzisha mfuko huu wa uwezeshaji, *Alhamdulillah*, tumefika mahali pazuri vijana wengi wamenufaika. Vikundi vya ushirika vya *SACCOS* na vyenginevyo, hivi ni tafsiri tosha ya kwamba ni sehemu ya ajira, vikundi vingi sana tunavyo katika majimbo yetu. Waheshimiwa Wawakilishi, siri kubwa ya mwakilishi kuendelea kwenye jimbo lake, mimi nakwambieni, nataka mfahamu, ukiweza kushirikiana na vikundi vya ushirika hasa vya kinamama, ukiendeleza vikundi vya ushirika wa vijana, utakaa kipindi cha kwanza, cha pili, cha tatu, hata cha nne. Tusione tabu kuwasaidia wananchi wale Mhe. Naibu Spika, wananchi wale hawana pakwenda ndio wako tayari wameshakuchagua wana matumaini makubwa, msiseme anatuchongea leo kwa wananchi huko, aah, ndio utaratibu wenyewe ulivyo, tujitahidini. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nimalizie malizie kwa sababu mengi kwa bahati yalikuwa yameshasemwa na sitaki tena kurejea yale yale. Nizungumze kwamba ni wajibu wetu…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwia, zimebakia dakika tatu.

Mhe. Haroun Ali Suleiman: Nitazimaliza *Inshaallah,* ni wajibu wetu sote waheshimiwa tushirikianeni ndani. Mimi napenda niwahakikishie kwa bahati nzuri si mkongwe wa humu ndani lakini tayari *Alhamdulillah* vipindi vitatu vimeshanifikia humu ndani na hiki cha nne *Inshaallah* na pengine cha tano kinakuja.

Mhe. Naibu Spika, niunge mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na ninamuahidi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Makunduchi, Mhe. Rais tutamuunga mkono katika jitihada zake zote anazozichukua ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inaelekea katika njia iliyokuwa sahihi kabisa na tunafanikiwa katika uchumi wetu katika maendeleo yetu ya kijamii na huduma mbali mbali *Inshaallah*.

Baada ya hayo naunga mkono hotuba ya Mhe. Rais na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie tufanikiwe sote, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana, nashukuru na mimi kunipatia nafasi hii, lakini kabla ya kuanza mchango wangu Mhe. Naibu Spika, ningekuomba kwa ridhaa yako utakumbuka Baraza lililopita tulikuwa na wenzetu ndani ya Baraza hili, lakini kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu aliwahitaji. Kwa hiyo, ningekuomba ridhaa yako ya kusimama dakika moja kwa kuwakumbuka wenzetu hawa kwa dua akiwemo mwenzetu Mama Asha Bakari Makame, tulikuwa na *PS* wetu wa Naibu Spika, lakini pia tulikuwa na Dereva ambaye alikuwa anafanya kazi katika Baraza hili. Ni vyema wenzetu hawa wakishatangulia tuwe tunapata wasaa wa kuwakumbuka ili na sisi tupate wasaa huo wa kuja kukumbukwa na wenzetu wakati wetu utakapofikia.

Mhe. Naibu Spika, naomba ridhaa yako hii.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Panya Ali Abdalla, kwa kuwa hilo nafikiria ni jambo zuri la kuwaombea wenzetu, sasa Waheshimiwa Wajumbe, naomba tusimame kwa muda wa dakika mbili kwa ajili ya kuwaombea wenzetu dua.

(Hapa Wajumbe walisimama kwa dakika mbili kuwaombea dua wenzao waliotangulia mbele ya haki)

Mhe. Naibu Spika: *Amin*, tuendelee Mheshimiwa.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana, nishukuru na namuomba Mwenyezi Mungu na sisi muda wetu ukifika atupe *Husni-lhatima*.

Mhe. Naibu Spika, nami nianze mchango wangu kama walivyoanza wenzangu kwa kumpongeza Mhe. Rais ambaye ameweza kupata ridhaa kubwa kwa wananchi kwa kupata ushindi uliopata asilimia 91.4. Hii ni ishara tosha kwa wananchi kuweza kumuamini sana Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein. Pia, nichukue fursa hii kumshukuru Spika wetu ambaye naye tulimchagua na amepata kura nyingi, lakini wewe mwenyewe pia Naibu Spika na Wenyeviti wetu wa Baraza wote wameweza kupata ridhaa nzuri. Kwa hivyo, nichukue fursa hii kuwapongeza sana.

Pia, nichukue fursa hii kuwapongeza wale makamishna ambao tumewachagua nao ni chombo muhimu katika Baraza hili. Nachukua fursa hiyo kuwapongeza sana najua wataweza kufanya kazi vizuri katika Baraza hili.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu nianze katika hotuba hii ya Mhe. Rais, ambayo imeletwa mbele yetu katika uzinduzi juzi, niseme kwanza hotuba nzuri na mwanana ambayo imeweza kusheheni vipaumbele vyenye umuhimu kabisa katika nchi yetu.Vipaumbele hivi ambavyo vimeainishwa katika hotuba hii tutakapofanya juhudi ya kuvitekeleza ipasavyo nchi yetu itaweza kupiga hatua kubwa kabisa ya maendeleo.

Kwa hiyo, niungane na wale wenzangu wote ambao wameanza kuchangia kwa kuiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja tukielewa kwamba ni dira katika utendaji wa majukumu yetu yote.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze kwa kushukuru nilipoona katika vipaumbele miongoni mwao iko elimu na afya. Mheshimiwa, nishukuru na niseme kweli tukijikita katika kutafuta elimu bora na kujenga afya za wananchi wetu ni hakika Taifa letu litaweza kupiga hatua moja kubwa, kwa sababu mwenye kutafuta elimu lazima pia awe ana afya. Kwa hiyo, tukiweza kuwakimu watu wetu katika afya basi Taifa letu hili litaweza kwenda vizuri.

Mhe. Naibu Spika, niseme tena juu ya afya hasa pale Mhe. Rais alivyoonesha kipaumbele chake kwa afya ya mama na mtoto. Hili ni jambo kubwa kwetu na lenye faraja kubwa, kwa sababu tumekuwa tukishuhudia kinamama wenzetu wakipoteza maisha kwa kukosa huduma hii ambayo ni bora. Lakini kwa kuwa Mhe. Rais anaelewa umuhimu wa mama na mtoto na akaliweka hili katika kitabu hiki, ni lazima tuchukue juhudi ya kumuunga mkono Mhe. Rais katika kuliendeleza hili ili iweze kupatikana afya ya mama na mtoto kwa kizazi kitakachokuwa bora ili tuweze kupata watoto ambao watakuwa wanazaliwa na afya bora lakini pia mama ambaye atajifungua katika uzazi salama basi anaweza kuwa na nguvu kazi nzuri ya kuendeleza na kuijenga nchi yake kwa pale alipo.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea pia Mhe. Rais aliwataja wanawake kama ni kipengele maalum, nampongeza kwa kuuona umuhimu wa kinamama na ni kweli kinamama kama alivyoeleza katika hotuba yake ni kichocheo kikubwa cha maendeleo. Pahala popote utakapoona mafanikio kama ni baba amepata mafanikio basi mwanamke yupo nyuma yake.

Kwa hiyo, Mhe. Rais alilolisema ni la kweli na la uhakika, sasa niiombe serikali kwa sababu kinamama wana jitihada kubwa hasa tukijua siku hizi wamekuwa wajasiria mali wakubwa wanajishughulisha na mambo mengi tu ya kiuchumi ili kuona familia zao zinaendelea kuboreka.

Mhe. Naibu Spika, niiombe serikali kwa kuwaona kinamama hawa kuwawezesha zaidi kwa taaluma mbali mbali hasa katika ujasiria mali ambapo wanaonekana wanajitahidi kufanya shughuli hizo, lakini pia niiombe serikali kuwatafutia masoko kwa sababu kinamama wanahangaika sana, wanajituma vya kutosha lakini mwisho wake wanavunjika tamaa kwa kutokuwa na masoko. Kwa hivyo, serikali ijikite masoko ya ndani yapo tukiacha ya nje, lakini bado hatujalenga ile dhamira yetu hasa kuona tunatafuta masoko haya na zile bidhaa wanazozizalisha basi zinakuwa hazina matatizo ya masoko. Kinamama wanafuga sana kuku na sisi tuna mahoteli mengi hapa, kwa hiyo, tukihakikisha tunawatafutia soko la kuwauza kuku wao wale, wataweza kupiga hatua moja kubwa. Kinamama pia ni wavuvi, wanavua madagaa, wanafuga chaza, wanafuga kaa, kwa hiyo, tukiwa na uhakika wa kuwapatia masoko haya, naamini wataweza kufanya vizuri na serikali ijipange kuwasaidia ili waweze kuendelea kupata mikopo hii inayotokana na serikali na mikopo yenyewe iweze kukua ili na wao waweze kufanya mambo makubwa ya kuinua uchumi wa nchi yao.

Mhe. Naibu Spika, niende katika suala zima la mazingira. Mazingira bado kweli ni tatizo kwetu na kama walivyosema wenzangu na mimi napenda niungane nao katika hili tusije tukamuelekezea kidole mtu mmoja, vyengine vitakuwa vinaturudia. Kwa hiyo, naomba tuungane kama sisi tukiwa ni wasaidizi wa Mhe. Rais, ili tushirikiane katika kuona tatizo hili tunalikabili kwa pamoja na kulitafutia ufumbuzi wa pamoja. Sisi tuliko kokote katika wilaya zetu, mikoa yetu na majimbo yetu tuhakikishe suala la ukataji wa miti ovyo, uchimbaji wa michanga ovyo basi tunaukemea na kwamba lazima ufuate utaratibu uliowekwa ili kuepusha majanga ya kimazingira.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia niseme katika huu ukataji wa miti, niiombe serikali basi iangalie ipo miti mingine inahitaji kukatwa, lakini ile inayoonekana iko karibu ya kuhatarisha uhai wa wananchi wetu. Kwa sababu kuna miti unapita iko njiani lakini mti wote umeshasukuka na umeshaelekea njiani, kwa hiyo, huo tunaona unaweza ukahatarisha maisha ya watu wakati wowote. Kwa hiyo, serikali pia ichunguze juu ya hili ili tuone pale penye athari ya kuhatarisha basi mti huo tuuondoshe na tupande mwengine mpya ambao utakuwa bado una afya nzuri na utaweza kuishi kwa muda mwengine.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye kilimo. Kilimo ndio uti wa mgongo wetu. Mimi naiomba serikali na ni punde tu Mhe. Rais, ataweza kutuchagulia mawaziri wetu, kwa hiyo, niseme bado tunahitaji wataalamu waweze kufanya kazi vizuri kwa sababu ardhi tuliyonayo ni ndogo. Lakini siku hizi Mheshimiwa, kuna utaalamu mwingi, kwa hivyo, utaalamu huo huwa tunakwenda kuusoma katika nchi za wenzetu lakini bado hatujautumia.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba niseme kwamba Baraza hapa lilinipeleka Malaysia na niliona utaalamu wa kilimo kinacholimwa juu kwenye maghorofa huko, watu wanalima tangawizi tuliziona, tungule, lakini pia kulikuwa na ufugaji wa samaki, tulikuta matangi huko ya samaki wanafugwa. Kwa hiyo, bado elimu hizi wataalamu wetu au wenzetu wanapokwenda kusoma mambo fulani kwa wenzetu basi tukirudi tusiyaache katika vitabu yakabaki kumbukumbu tu, ni lazima elimu hiyo tuliyokwenda kuisoma kule kwa wenzetu tuitumie ili iweze kuleta manufaa katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, niiombe serikali kujikita katika suala zima la viwanda, kwa sababu tunajua tuna changamoto nyingi za ajira. Lakini tunaamini tukiweza kupata viwanda hata kama hatujawa na uwezo wa kujenga viwanda vile vikubwa vikubwa lakini viwanda vidogo vidogo navyo vinaweza kutusaidia kwa asilimia kubwa katika kupunguza wimbi la vijana wetu ambao wanahangaika kwa ajira.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme kulikuwa na kiwanda cha chakula cha kuku *ZAPOCO* kule Maruhubi. Kiwanda kile kilikuwa wafugaji wengi ndio kimbilio lao, sasa na sisi tunavua madagaa wenyewe, kwa nini kiwanda kile kisijirejee ili tukawa tuna uzalishaji ambao ungeweza kuwapatia unafuu wale wafugaji wetu ambapo kiwanda kitakuwa kipo hapa hapa kwao, lakini pia kingeibua chachu nyengine ya wakulima wa mahindi ambapo wangejua kama zile pumba zitakuwa zinahitajika katika kutengeneza chakula. Kwa hivyo, hii ingeweza kutusaidia baada ya kilimo fulani cha mpunga watu wangejikita pengine katika kulima mahindi wakijua baada ya mahindi haya tukila tunapata na faida nyengine ya uzalishaji wa chakula cha kuku.

Mhe. Naibu Spika, na mimi niungane na wenzangu katika kuvipongeza vikosi vyote vya ulinzi na usalama ambavyo vimeweza mpaka muda huu kusimamia usalama wa Taifa letu hili katika kuwalinda wananchi na mali zao. Mhe. Naibu Spika, nawapongeza sana, sana.

Vile vile, naiomba serikali kuangalia maslahi ya askari wetu hawa ili waweze kufanya kazi vizuri zaidi, lakini pia na vitendea kazi kwa sababu wanafanyakazi katika mazingira magumu kabisa. Kwa hivyo, wakiweza kupatiwa vitendea kazi wataweza kufanya kazi yao kiuhakika zaidi.

Mhe. Naibu Spika, niungane na wenzangu kwamba hotuba hii imesheheni kila kitu na ni wajibu wetu sasa kila mmoja kwa sekta yake pale alipo kuweza kumuunga mkono Mhe. Rais katika utekelezaji wa mambo haya.

Mhe. Naibu Spika, penye nia panakuwa na njia, tukiweka nia thabiti katika utekelezaji wa mambo haya Mwenyezi Mungu ataweza kutuwezesha na tunaweza tukapiga hatua kubwa na tukawafanya wananchi wetu kuwa na moyo mkubwa juu ya serikali yao. Naomba tujikite sote katika kumsaidia Mhe. Rais katika utekelezaji wa kazi hizi kila mmoja pale alipo.

Mhe. Rais, ameweza kusema kwa ukali kabisa katika kuwakemea wazembe, wala rushwa, wabadhirifu wa mali za umma na amesema hili sio kwa maneno tu, atalitekeleza kwa vitendo. Mimi naomba Waheshimiwa wenzangu na wahusika watendaji wenzetu popote pale mlipo nikuombeni basi tusingoje kuwajibishwa, tujiwajibishe sisi wenyewe katika kujibadilisha katika kuachana na ule ufanyaji kazi wa mazowea, ili tuweze kujirekebisha na kuweza kulipatia Taifa letu hili maendeleo makubwa kabisa ili mwaka 2020 basi CCM iweze kushinda bila ya kikwazo chochote. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mwisho niendelee kumshukuru Mhe. Rais kwa kuwateuwa wajumbe saba ambao tumewaapisha hapa leo. Namshukuru sana kwa uteuzi wake na naamini tutaweza kupiga hatua moja kubwa ya maendeleo katika Baraza hili, kwani linaainisha kwamba hili ni Baraza la wananchi wote wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Rais kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Naibu Spika, na mimi napenda nichukue fursa hii kwa kukushukuru wewe nami kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Rais katika jioni hii ya leo. Vile vile, napenda nichukue fursa hii kukupongeza wewe kwa mara ya pili kwa dhati kabisa na kumpongeza Mhe. Spika, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi ambazo zimeonesha kuwa ni dhahiri kwamba wamemridhia. Vile vilem naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Rais kwa kutoa hotuba hii ambayo ndio dira na mwelekeo wa shughuli zetu ambazo tunatarajia kwamba tuweze kuzifikia katika kipindi hiki cha awamu ya pili ya uongozi wake Mhe. Rais.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo napenda nichukue fursa hii kwa kujipongeza mimi mwenyewe binafsi na vile vile, kuwapongeza sana wananchi wangu wapiga kura wa Jimbo la Micheweni kwa kunipa ridhaa kuwepo hapa leo ili na mimi nije niwawakilishe wao katika kuwatetea kwa yale ambayo yamekuwa ni kero katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi napenda niende moja kwa moja kuchangia hotuba hii kwa kuangalia ile dhamira ya kitabu hiki cha hotuba ya Mhe. Rais kama vile ambavyo kimeeleza, ambacho kinaonekana kina *page* 80, kimesheheni muelekeo na uchanganuzi wa kina kabisa katika kuona kwamba Mhe. Rais amekuwa na dhamira ya kweli kutaka kuendeleza juhudi za mapambano katika kupunguza suala zima la umasikini na kuongeza kipato kwa wananchi wetu.

Ukiangalia katika dhamira na muelekeo wa serikali nianze kuangalia kwamba katika hotuba yake Mhe. Rais ameonesha katika kipindi cha mwaka 2010/2015 katika suala zima la ukusanyaji wa mapato ilikuwa ni 362.8 bilioni na kuna muelekeo ifikapo mwaka 2020 muelekeo wa makusanyo ya bilioni 800. Hili Mhe. Naibu Spika, linaweza likafikiwa iwapo kutakuwa na dhamira ya kweli juu ya kusimamia utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku kwa kila sekta.

Kwa upande wangu mimi nahisi kwamba dhamira ya Mhe. Rais ni nzuri na inaonekana ina muelekeo na inahitaji kuungwa mkono kwa hatua zote. Lakini bado inaonekana kwamba kuna watendaji ambao au kuna watu ambao kwa njia moja au nyengine bado hawajaweza kubadilika na kufanya kazi kwa mujibu wa muelekeo na majukumu ambayo wamepangiwa na badala yake wanafanya kazi kwa mazoea na kupelekea serikali kulaumiwa na kuona kwamba kama haijafanya kitu, na kumbe kunatokana na sababu na uzembe wa mtu binafsi na sio serikali.

Mhe. Naibu Spika, vile vile naomba nielekee katika kuangalia katika masuala mazima ya kilimo. Katika kitabu hichi kimeelezea vizuri katika mkakati wa Mhe. Rais kuhusu kilimo chetu ambacho ni uti wa mgongo wa taifa hili, kumeonekana kwamba kuna dhamira ya kweli na hii imeonekana kwamba kwa mfano Chuo cha Kilimo Kizimbani ndicho chuo ambacho kwa sasa hivi kinasaidia katika juhudi za wakulima katika nchi hii iweze kuonekana kwamba uzalishaji unaongezeka siku hadi siku, lakini bado Chuo hichi kina changamoto nyingi ambazo Mhe. Rais ameziona, na kwa vile changamoto hizi tayari zimeainishwa ni vyema kwamba wale wahusika ambao Mwenyezi Mungu atawajaalia kupata fursa ya kuteuliwa kuwa mawaziri basi waongeze juhudi katika kuona kwamba wanasimamia jambo hili ili Chuo hichi kiweze kuonekana kwamba kinapiga hatua kwa kadiri itakavyowezekana, ili kuweza kuleta tija zaidi katika kutatua matatizo ya wakulima katika nchi yetu.

Kwa mfano ikiwa sasa hivi katika kipindi hichi ambacho ni kipindi cha makulima imeonekana kwamba juhudi ambazo zilifanywa na ambazo zina muelekeo wa Rais sasa hivi anazotaka kufanya lakini bado kuna mapungufu

katika maeneo yetu. Mfano katika Wilaya ya Micheweni. Katika Wilaya ya Micheweni kwa sasa hivi kuna mabwana shamba ambao hawazidi wanne, na katika kipindi hichi cha makulima kunaonekana wananchi na wakulima wanahitaji kupata huduma za utaalamu ili waweze kuzalisha vizuri na kuweza kuzitumia pembejeo za kilimo vizuri ili hatimaye waweze kuongeza pato na uzalishaji katika nchi yetu.

Hivyo, hili linaonekana kutokana na idadi hii ndogo ya mabwana shamba. Uwezekano wa kuongeza katika uzalishaji wa kilimo unaweza kuleta changamoto nyingi na usiweze kufikiwa kama vile ambavyo Mhe. Rais amelenga katika kufikia hatua hizo ambazo zimeelekezwa au zimeainishwa katika kitabu hichi.

Mhe. Naibu Spika,vile vile ukija katika masuala ya miundombinu katika masuala ya miundombinu tumeona katika hotuba ya Mhe. Rais kuna barabara ambazo zimeainishwa ambazo zimetajwa tayari zimepangiwa mkakati wa kuweza kujengwa katika kiwango cha lami, lakini vile vile bado kunaonekana kuna changamoto ambazo zinaonekana na Mhe. Rais ameziona katika kuona kwamba barabara hizi zinazojengwa kwa sasa hivi bado kuna matatizo katika masuala mazima ya usimamizi wa rasilimali hizo ambazo zinakuwa zinatumika katika masuala mazima ya ujenzi wa hiyo miundombinu ya barabara.

Mhe. Naibu Spika, vile vile katika changamoto katika sekta ya mifugo. Katika mifugo Mhe. Rais aliweza kuzungumzia uhaba wa ardhi ni tatizo ambalo limeonekana linakuwa na changamoto, na changamoto hizi zinatokana na kuongezeka katika shughuli za kiuchumi na vile vile na shuhuli za kimaendeleo. Hivyo kwa kupitia sekta hii iwapo kama mikakati itaweza kufanikiwa kwa uwajibikaji basi kunaweza kukapelekea tija na kuongeza kipato kitakachotokana na mazao ya kilimo na mifugo katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, katika sekta hii ya mifugo katika masuala mazima ya kuangalia sera na sheria zilizopo zinasimamiwa vizuri na kuongeza mikakati ya kuimarisha vituo vya huduma za mifugo kwa kuweka vitendea kazi na kuwasomesha wataalamu zaidi na kuwaajiri wafanyakazi wapya, ili kuongeza uzalishaji na katika suala zima la taaluma na utoaji wa huduma za mifugo.

Mhe. Naibu Spika, katika suala la kilimo cha mwani hotuba ya Mhe. Rais imezungumzia zaidi katika lengo ambalo na dhamira ambayo inatarajiwa kufanyika kwamba vihori na visaidizi vya kubebea mwani kutoka baharini na idadi ya vihori ambavyo Mhe. Rais amesema vinaweza kununuliwa ni 500, ambavyo vitaweza kutoa huduma kwa wananchi wapatao elfu tatu, hivyo sera ya uvuvi ya bahari kuu pia vile vitaweza kuongeza kuwavutia wawekezaji sambamba na kujenga viwanda vya kusindika samaki katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wangu napenda niseme kwamba kitabu hichi kimeweza kukidhi mahitaji na kimesheheni kwa kadiri ambavyo nchi hii inaweza ikafikia malengo yake kwa kupitia muelekeo huu ambao Mhe. Rais ameweza kuanza kuonesha. Hivyo Mhe. Naibu Spika, ningependa kwamba kwa sasa wananchi wa Jimbo la Micheweni kwa sasa wamechoshwa na kusikia hadithi mbali mbali ambazo hazina utelekezaji ndani yake.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, ningependa kuchukua fursa hii kwamba sasa niombe watendaji wa serikali hii ambao watabahatika kuteuliwa kuwa Manaibu Waziri na kuwa Mawaziri, basi waweze kuona kwamba wanafanya kazi kwa kuendana na mazingira ya sasa, na si kuendana na mazingira ambayo walitoka nayo au mazingira waliyoyazoea. Hivyo wananchi wa jimbo la Micheweni pia wanatarajia kuiona serikali yao inaweza kutimiza yale mahitaji ambayo imeahidi katika njia mbali mbali na kupitia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache naomba mimi nichukue nafasi hii kwa kushukuru hotuba hii nzuri ambayo imejaa hekima na busara ambazo kama itatumika ipasavyo inaweza ikaleta tija katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache naomba niunge mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Said Soud Said: Mhe. Naibu Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumjaalia Dkt. Ali Mohamed Shein kuniteuwa kuwa Mwakilishi ambaye nitakuwa tayari kumsaidia katika hali ya kuiendeleza Zanzibar na Wazanzibari wote katika nchi hii. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, pia nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kumchagua tena Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kuwa Makamu wa Pili wa Rais. Nakupongeza sana Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, kuchaguliwa kwako ni maendeleo makubwa ya demokrasia Zanzibar na ni matumaini makubwa kwa Wazanzibari. (*Makofi*)

Halkakdhalika nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Spika, pamoja na Mhe. Naibu Spika, kwa kuchaguliwa kwao kuliongoza Baraza hili. (*Makofi*)

Vile vile sina budi kuchukua nafasi kuwashukuru wanachama wa Chama cha Mapinduzi Unguja na Pemba kwa uvumilivu mkubwa waliouonesha mpaka kufikiwa kwa uchaguzi wa marudio, na uvumilivu wao uliwezesha kuchukua tena nafasi ya kuwa walimu wa demokrasia Zanzibar, na nasema hivyo kwa sababu ya ushahidi. (*Makofi*)
Mhe. Naibu Spika, mara baada ya uchaguzi kufutwa mimi nilisusiwa na Wapemba wote, na nikazuiwa hata kunywa kahawa katika vijiwe vya kahawa. Lakini napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wanachama wa Chama cha Mapinduzi waliamua kwa makusudi kupika kahawa kwa ajili yangu. (*Makofi*)

Kwa maana hiyo bado nahitaji kusema kwamba Chama cha Mapinduzi kina kazi kubwa ya kuelimisha demokrasia Zanzibar, na kwa mpango huu tunaokwenda nao hakuna chama chochote cha siasa kitakachochukua serikali zaidi ya CCM. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nataka nichukue nafasi ya kwanza kusema kwamba hotuba hii ni *GPS* inayoongoza meli watu wakafika salama. Mhe. Naibu Spika, meli haiwezi kwenda ikafika salama kama hakuna *GPS,* na serikali yetu hii itakayoundwa basi *GPS* kubwa ni hii hapa tukikubali kufanyakazi kwa kufuata *GPS* hii, basi nina uhakika kabisa kwamba Zanzibar itapiga hatua na hata hao wanaodai kuzuia misaada yao wataona ajabu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ningetaka niseme kwamba hotuba hii imezungumzia mambo mengi yanayowahusu Wazanzibari na nchi yao. Lakini na mimi sina budi kusema kwamba kuna mambo ambayo ni muhimu sana ya kuzingatiwa tunaweza tukapiga hatua kubwa.
Kwanza ni suala la elimu. Suala la elimu katika nchi hii ni kipaumbele kikubwa cha kwanza kabisa ambacho kitazalisha wanasayansi watakaoweza kukidhi haja katika kuisukuma serikali na nchi yao kuifikisha kwenye maendeleo. Ni jambo la ajabu sana kwamba elimu inayotolewa katika nchi yetu inafikia hadi Chuo Kikuu lakini hawezi kutengeneza Panadol. Sasa ni wajibu serikali kutumia nafasi yake na maabara kuzidumisha ili kuhakikisha kwamba wanaotoka wanaweza kujiajiri wenyewe pasi na kutegemea serikali. Kwa hivyo, elimu inahitajiwa kuzungumzwa na kusomeshwa kwa umakini zaidi, ili nchi hii ipige hatua kubwa.

Mhe. Naibu Spika, hotuba hii imezungumzia kilimo. Ni kweli kabisa nchi yetu imezoea kilimo hasa cha kujikimu. Lakini kilimo cha biashara bado hakijapewa nafasi, na kwa sababu gani basi Wizara hii ya Kilimo ina wataalamu wakubwa, wazuri, lakini waliojikita kwa sababu ya kungojea serikali eti ijayo waje wafanye kazi. Sasa nataka niseme hayo ni majipu, watumbuliwe, tukiwa na utaratibu wa kuyaondoa majipu na kuyapara, maana kuna majipu mengine hayawezi tena ni tenzi, yameshageuka tenzi, sasa yakatwe hasa. (*Makofi*)

Kwa vile kulingana na hali hiyo Mhe. Naibu Spika, wataalamu tulionao lazima wawe wanatoa ripoti kwa umahiri kabisa kwenye serikali za wilaya na mkoa, kazi gani waliyoifanya kwa mwezi na mabonde mangapi wameyatembelea, wamewasaidia wakulima nani na nani na nani, hapo basi ndio tutaweza kusema kwamba kilimo sasa kinashughulikiwa na hata tukisema kwamba tunaondokana na kilimo cha kujikimu tunakwenda kwenye kilimo cha biashara basi halikadhalika serikali nayo itakuwa na wajibu wa kuliangalia tena zao la hiliki ambalo liliboreshwa wakati wa Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi, likaangaliwa tena zao la Vanilla ambalo lilikuwa linataka kuanzishwa katika wakati ule, na hayo ni mazao ambayo yanaweza kuwapatia wananchi wetu pesa nyingi sana za kuweza kuendesha maisha yao. Kwa vile kilimo kinahitajika katika fani mpya sasa na tuachane na kile kilimo cha kujikimu twende katika kilimo cha biashara.

Mhe. Naibu Spika, mimi chama changu ni Chama cha Wakulima, nimegundua kule Tanzania Bara kuna *NGO* moja inapeleka muhogo Marekani, Thailand, Hong Kong wanapeleka Japan muhogo mbichi kabisa, wanaupeleka huko tani sitini elfu wanapeleka mpaka Marekani. Sasa wakulima wetu hapa wanangojea serikali ijayo waje waelekezwe hayo. Serikali hii ina uwezo wa kuwaeleza, serikali hii ina uwezo wa kuwapeleka Marekani wakauza mihogo yao, serikali hii ina uwezo wa kuwapeleka China na Japan wakauza mihogo yao. Kwa hiyo, kinachotakiwa sasa ni

kuwaboresha wakulima wetu na kuwafanya waondokane na ile dhana ya kupokea *drip,* maana sasa wanakula *drip* tu, watu hapa waachane na ile dhana, kidonge kitakachowatibu sasa hivi BLW, Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kidonge hicho ni *antibiotic,* kitatibu tu hicho, utatibika tu, Baraza la Wawakilishi kitatibu. Kwa hiyo Mhe. Naibu Spika, nataka niseme kwamba wakati umefika wa kumsaidia Mhe. Rais, maelezo yake yote haya yafanyike kwa vitendo ili nchi ipate kwenda tunakotaka. (*Makofi*)

Halikadhalika Mhe. Naibu Spika, nchi yetu hii ya Zanzibar ni sawa na nchi nyengine zote duniani. Nchi hii ilikuwa na *traditional* ambazo zinatambulika na watu walikuwa wanavutika nazo, lakini tamaduni zimekufa. Yaani tamaduni zimekufa zimebaki sasa za watu kukaa kwenye vijiwe wakazungumza siasa tu, tena siasa zenyewe za *drip* si siasa za maendeleo. (*Makofi*)

Kwa vile mimi ningeomba tu kwamba Mhe. Rais atakapowateua Mawaziri wake wa Mila na Utamaduni, basi suala la *tradition* lirudiwe ili nchi hii watu wacheze ng'ombe kama kawaida, ng'ombe yule ng'ombe, watu wacheze gonga, wacheze beni, maradhi yataondoka ya sukari.

Mhe. Naibu Spika, ile kujikalia tu watu wakachukua uongo huu na huu umezalisha maradhi ya sukari nchi nzima, lakini kama watu watakuwa wanacheza ng'ombe, beni, midundiko na wanakwenda kwenye *sports* kikweli kweli, mimi naamini maradhi yataondoka. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ni vizuri tukasema kwamba *traditional* ya visiwa vya Unguja na Pemba irudishwe kwa nguvu zote kama ni sehemu moja ya burudani kwa watalii, kwa sababu watalii wanakuja hapa mpaka wanaondoka hawaoni hata ngoma moja, labda iwe kile kipindi cha Jahazi ndio pale utakwenda kuwakuta watu wanaona angalau ngoma zetu. Lakini zamani ilikuwa watu wakivuna chooko, mpunga na korosho wanacheza ngoma za kuonesha utamaduni wao. Sasa mambo kama haya yarudiwe, Zanzibar ni ile ile haijabadilika, wanaobadilika ni vizazi kwa vizazi, lakini Zanzibar isipoteze uwezo wake wa kihistoria kwa sababu zisizokuwa na msingi. *(Makofi)*

Halikadhalika Mhe Naibu Spika, ningetaka niseme kwamba mambo mengi katika nchi yetu hii ya Zanzibar yameharibika kwa sababu ya kitu kinachoitwa *corruption* ya muhali. Bora *corruption* ya nyuma ya meza kuliko *corruption* ya muhali. Tukiwa tunataka kweli kuboresha hoja hii na hotuba hii ya Mhe. Rais, ni lazima muhali uondoke, bila ya kuondoa muhali hatuwezi tukapiga hatua ya maendeleo hata hatua moja, pia kama tutaendelea kulindana labda huyu mtoto wa nani na huyu mtoto wa yule au huyu mwenzangu au tumesoma pamoja, tutaifanya nchi hii siku zote tunamalizia maneno haya.

Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Rais pamoja na msaidizi wake Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ambaye mimi nasema ni Makamu wa Rais wa Zanzibar, pamoja na mawaziri watakaoteuliwa kuongoza serikali basi watembee na mikasi katika makoti, kuta jipu kata, kuta kipele kata, kuta nini kata. *(Makofi/Vicheko)*

Mhe. Naibu Spika, anachokifanya Mhe. Rais John Pombe Magufuli, nataka niseme ni sera ya Chama cha Mapinduzi, hafanyi kitu cha ajabu, na hapa Chama cha Mapinduzi kipo na bado kitaendelea kuwepo kwani ndicho kinachotawala. Sasa leo kwa nini CCM wa Zanzibar muendelee kulindana, watu wafuje mapato ya nchi, wafuje rasilimali za nchi, kila mtu anajilimbikizia mamali tu, majumba, magari na kila kitu, kwa sababu gani watu wetu wanapata tabu.

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais nakuomba pamoja na Mhe. Naibu Spika, zana zote zinazotumbua majibu akabidhiwe yule mzee, ahsante sana. Naunga mkono hotuba hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Tunakushukuru sana Mhe. Said Soud Said kwa mchango wako mzuri. Waheshimiwa wanaofuata sasa ni Mhe. Bihindi Hamad Khamis, na baadae atakuja Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi na ajitayarishe basi Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pili nimpongeze Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa uteuzi wake ambao aliteuliwa na Mhe. Rais. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kupata ushindi wa kishindo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tatu niwapongeze wananchi wangu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, kwa kuweza kuniteua na kunichagua nikawa Mwakilishi wa viti maalum Mkoa wa Kaskazini Pemba, na nikaweza kuingia kwenye Baraza hili Tukufu kwa mara yangu ya tatu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa niipongeze hotuba hii ya Mhe. Rais ambayo aliisoma jana kuweza kutekeleza majukumu yake ambayo amepewa kama Mhe. Rais. Vile vile niweze kuchangia kwenye sekta ya habari.

Nimpongeze Mhe. Rais kwa kuweza kuzungumzia kwenye hotuba hii vipaumbele ambavyo vinahusiana na sekta ya habari. Mhe. Rais amezungumzia kuhusu sekta ya habari kwenye Shirika la Utangazaji ZBC, alisema kuwa atatekeleza vipaumbele vya kuweka vifaa vya *digital*, ili wafanyakazi wetu wawe na uwezo mkubwa wa kuweza kufanya kazi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea kwenye sekta hii hii ya habari, Mhe. Rais ameelezea vipaumbele kwenye mambo ya historia na makumbusho na mambo ya kale. Amesema atajenga makumbusho na mambo ya kale na majengo ya historia, na mapango yote yalioko Unguja na Pemba kuweza kufanyiwa utafiti ili watalii wetu waweze kutembelea kwenye mapango yale na maeneo ya historia. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende kwenye utamaduni na michezo. Mhe. Rais kwenye kipaumbele chake kwenye michezo, alisema ataendeleza michezo na utamaduni wa Kizanzibari, na ataendeleza matamasha ambayo yanafanyika mwaka hadi mwaka.

Mhe. Said Soud hapa alichangia vya kutosha kuhusu mila na desturi za Kizanzibari. Mila na desturi za Kizanzibari zinaingia kwenye utamaduni wa Kizanzibari pamoja na mila na desturi. Mhe. Rais pia kwenye hotuba yake hii alielezea kuwa ataendeleza matamasha na mambo mengine yanayohusiana na mambo ya utamaduni. Kwa kweli nimpongeze Mhe. Rais kwa kuweka vipaumbele hivi kwenye sekta ya habari.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea mbele nije kwenye eneo la kilimo. Mhe. Rais kwenye kipaumbele chake kwenye maeneo ya kilimo, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita aliyaendeleza mabonde mbali mbali yalioko kwenye Mkoa wa Kaskazini Pemba, lakini kuna kipaumbele kimoja amekitaja kwenye hotuba yake, bonde lilioko Mkoa wa Kaskazini Pemba, mwanzo ilikuwa ni Wilaya ya Micheweni, lakini sasa hivi imeingia Wilaya ya Wete kwa sababu ya kukatwa majimbo. Eneo hili ni bonde la Makwararani, nampongeza Mhe. Rais kwa kuweka vipaumbele hivi kwa sababu wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, hususan Wilaya ya Wete ikiambatana na Wilaya ya Micheweni watafaidika na kilimo hiki cha umwagiliaji maji.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea niende kwenye Sekta ya Miundombinu. Mhe. Naibu Spika, hotuba hii kwa kweli imeeleza kwa kina na ina ufafanuzi wa kutosha Mhe. Rais alivyotufafanulia kwenye hotuba hii. Kwa kweli nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wenzangu, kama ni *mas-ul* hapa sote ni wajumbe wa CCM tuweze kuisaidia serikali ili kusimamia ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Maana yote haya yaliyomo kwenye hotuba hii ni usimamizi wa ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye upande wa SACCOS, kama alivyoeleza Mhe. waziri mstaafu Mhe. Haroun Suleiman na yeye tunampongeza kwa kusimamia juhudi kubwa kwenye mambo ya SACCOS.

Kwa kweli Mhe. Rais akishirikiana na wanawake wa Mikoa yote ya Unguja na Pemba na wanawake ambao wamesimama imara kuweza kutekeleza majukumu yao kwenye SACCOS. Tunampongeza sana Mhe. Rais, na kwa kweli tumefarijika sana wanawake wa Mikoa yote ya Unguja na Pemba kuweza kuwa na SACCOS na kuwa na benki ambazo zinajitegemea wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende kwenye sekta ya afya. Sekta ya Afya nayo Mhe. Rais kwenye kipaumbele chake ambacho alikitangaza miaka mitano iliyopita. Sisi ni wanawake tunajifungua na tunaumwa, hivyo tunampongeza Mhe. Rais kwa kuondosha lile tatizo la kulipia tunapojifungua mahospitalini, hilo

pia tunampongeza Mhe. Rais kwa juhudi zake hizo ambazo amezichukua na ameweza kutekeleza majukumu yale kwa upande wa wanawake. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu hotuba hii ina mambo mbali mbali kwenye sekta zote, imeeleza kina na ufafanuzi mkubwa basi Mhe. Naibu Spika, nimesema nifikie hapo. Lakini pia naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wote wa Unguja na Pemba kwa kuchaguliwa kwa ushindi wa kishindo, na tukaweza kuingia kwenye Baraza hili Tukufu na tukasimamia majukumu ya serikali pamoja na majukumu ya majimbo yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu nilisema sitochangia sana, isipokuwa nimesimama kwa ajili ya kumpongeza Mhe. Rais na hotuba hii, basi naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia juu ya mia, ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Bihindi Hamad Khamis. Anayefuatia sasa ni Dkt. Makame Ali Ussi, na baada ya hapo atafuatia Mhe. Abdalla Maulid Diwani na ajitayarishe basi Mhe. Zulfa Mmaka Omar.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Mhe. Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo hii kusimama hapa katika Baraza hili la Wawakilishi kutoa niliyonayo yanayohusu hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Spika, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana kwa chaguzi zote mbili, ile iliyofanyika kichama na hii iliyofanyika hapa katika Baraza la Wawakilishi. Namtakia utekelezaji mwema sana wa majukumu yake katika Baraza hili la Wawakilishi.

Pia nakupongeza Mhe. Naibu Spika, kwa kuchaguliwa kwa mfumo huo huo aliochaguliwa Mhe. Spika. Nategemea sana, na nina hakika, sisemi nategemea bora niseme nina hakika kabisa kwamba utakuwa msaidizi mzuri sana wa Mhe. Spika, pamoja na Wawakilishi sote.

Vile vile naupongeza uamuzi wa Mhe. Rais wa kumteua Mhe. Balozi Jemedari wetu huyu, kumchagua kuwa Makamu wa Pili wa Rais na mimi naungana na wenzangu kusema kwamba huyu ni Makamu wa Rais, kwa sababu hakuna Makamu wa Kwanza wa Rais.

Pia napongeza uteuzi wa wenzetu hawa waliochaguliwa katika uteuzi wa Rais, wale wenzetu wa Chama cha Mapinduzi, wametuongezea nguvu kubwa sana katika Baraza hili na wale wenzetu kutoka vyama vya upinzani, pia na wao wametuongezea nguvu sana katika Baraza letu hili, kwani wana uzoefu mkubwa sana wa siasa kama tulivyowasikia walivyochangia hapa.

Mhe. Naibu Spika, pia napenda tujipongeze sisi Wawakilishi sote kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana kuwawakilisha wananchi wetu majimboni na viti maalum. Kwa kweli mimi nawashukuru sana wananchi wangu wa Mtopepo, nawaambia kwamba mimi ndio mwakilishi wao, lakini na wao pia ni wawakilishi wangu, kwa hivyo sote tunawakilishana.

Kwa hivyo, katika mambo ya maendeleo sote tutakwenda bega kwa bega, nawaambia kwamba kura walizonipa kwa wingi nitazitendea haki na nitafanya yote yale ambayo yanatakiwa kufanywa ili maendeleo katika jimbo lile yaweze kupatikana.

Mhe. Naibu Spika, naelewa kuna matatizo ya maji, barabara, zahanati ya serikali kule hakuna, kuna matatizo ya kijamii mengi sana. Kwa mfano, matatizo ya walemavu, vijana na kadhalika yote hayo tutayashughulikia, na ninasema tutayashughulikia kwa kushirikiana na Wawakilishi wenzangu katika Baraza hili ili kuyatatua matatizo haya. Nasema kwa kweli tumetoka katika hali ngumu sana.

Mhe. Naibu Spika, mambo yaliyotokea katika kipindi hiki cha miezi 6 au 8 iliyopita, kwa kweli hayajawahi kutokea katika Taifa letu hili la Zanzibar tangu Mapinduzi. Kuna ubadhirifu umefanyika, wananchi vimenunuliwa vipande vyao, yaani kuwakosesha haki ya kupiga kura, hiki ni kitendo ambacho kwa kweli tunakilaani kwa nguvu zote.

Mhe. Naibu Spika, jengine napenda niwapongeze sana ndugu zangu kutoka Pemba, kwa kweli kwa kipindi kirefu sana tangu kuanza vyama vingi wamekuwa wakishiriki katika mapambano haya ya kutaka kugombea uwakilishi, lakini kwa bahati mbaya wamekuwa wakikosa nafasi kutokana na mazingira yaliyokuwepo ambayo yalikuwa hayaruhusu wao kufanikiwa.

Pia nawapa pole kwa sababu majimbo yao yote kule wale wabunge wao ni wapinzani. Sasa nina wasi wasi kama watapata mashirikiano mazuri sana na wale. Lakini hata hivyo, tutasaidiana kutoa ushauri kwa pamoja katika Baraza letu ili na wale nao washiriki katika mambo ya maendeleo kwa faida ya wananchi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikiingia katika hotuba sasa. Kwa kweli hotuba ni nzuri na mimi kabla sijasema lolote naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nimeipitia hotuba hii ukurasa kwa ukurasa, mstari kwa mstari, koma kwa koma, na nukta kwa nukta nimeifahamu. Kwa hivyo, kama tutaweza kutekeleza yaliyomo kwenye hotuba hii, nadhani lile lengo la kufikia uchumi wa kati na kati tunaweza tukalivuka. Kwa hivyo, nawashauri sana Wawakilishi wenzangu pamoja na watendaji wote serikalini huko, tufuate miongozo iliomo kwenye kitabu hiki na tuweke mikakati ambayo itatuwezesha kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Kwa jumla hotuba hii imeweza kutufundisha mambo yafuatayo.

Mhe. Naibu Spika, imeweza kutufundisha kwamba ni lazima tunapofanya kazi zetu tuwe na umoja, yaani tuwe wamoja.

Pili, imetufundisha kwamba tunapofanya kazi zetu ni lazima tuwe na ushirikiano.

Tatu, imetufundisha kwamba lazima tuwe na mshikamano. Lakini zaidi ya yote haya ni lazima tuwe na upendo, urafiki miongoni mwetu au baina yetu, ni lazima tuwe majirani wema tusaidiane. Pia ni lazima tudumishe usalama, amani na utulivu kwani hivi peke yake ndivyo vitakavyoweza kutuletea maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nikiingia katika majimbo nasema majimbo yetu yamegawika sehemu mbili. Kuna majimbo magumu kiuchaguzi na magumu kimaendeleo. Moja katika majimbo magumu ya namna hiyo ni Jimbo la Mtopepo. Kwa kweli, kule hivi sasa kuna kipindupindu, barabara si nzuri, maji hakuna isipokuwa kuna mabomba yalilazwa wakati huo wa CCM ilipokuwa inaongoza, na mabomba yale mpaka hivi sasa hayakupata huduma yoyote na yamekatikakatika na maji yanapofunguliwa yanavuja.

Kwa hiyo, tuna kazi kubwa sana ya kuimarisha miundombinu ya maji na barabara, ili njia zile ziweze kupitika. Vile vile, tuna kazi kubwa sana ya kufanya utafiti wa kina kwa nini kipindupindu kimehamia kule Mtopepo zaidi kuliko sehemu nyengine.

Mhe. Naibu Spika, nikizungumzia masuala ya uwekezaji. Kwa kweli, kuna haja kubwa sana ya uwekezaji na mengi yamezungumzwa kuhusu uwekezaji, lakini naomba kutilia mkazo sana uwekezaji wa kujenga vituo vya afya ambapo huko ulaya kuna watu wana fedha zao wanapata *frustrations*, hivyo wanapenda wafike mahala wapumzike ili ile hali yao ya kiafya iweze kurudi. Sasa hawa hupenda sana sehemu kama visiwani kuja kutembelea. Kutokana na hali hiyo, kama tutaweza kuwa na vituo vya afya basi tunaweza kupata watu wa aina hiyo kwa wingi na tutaongeza utalii wetu.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie suala la uimarishaji wa miji. Jambo hili limetiliwa mkazo sana tena ni muhimu. Mhe. Naibu Spika, nashauri uimarishaji wa miji hii iambatane na ujenzi wa bandari ndogo ndogo. Kwa mfano, Mkokotoni hapo zamani palikuwa na bandari kubwa tu, lakini bandari ile ni kama haipo, kwa sababu hailingani na mahitaji ya uchukuzi wa mizigo ya hivi sasa. Kwa hivyo, kama pataweza kujengwa bandari ambayo itaisaidia bandari ya Zanzibar, ili pasiwe na msongomano mkubwa nadhani itakuwa ni jambo la busara sana.

Vile vile, na sehemu nyengine za miji kama vile Makunduchi na nyenginezo tukijenga bandari ndogo ambayo wananchi wanaweza kuzitumia, kwa ajili ya kuegesha vyombo vyao nafikiri itakuwa ni vizuri.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la biashara. Kwa kweli, tunazo biashara na zinakwenda vizuri, lakini tuangalie sana aina za bidhaa zinazoletwa, yaani zinakuja bidhaa hapa ambazo zimeshachakaa na kupitiwa na muda na wala hazifai kwa matumizi ya binadamu, na hizi zinaweza kutuletea madhara makubwa kwa afya za binadamu. Pia, kama walivyosema wenzangu kuna biashara za kibaguzi hivi sasa, kwamba huyu tusimuuzie au tumuuzie kwa bei kubwa ama tufanye nini. Kwa hivyo, naomba sana watu wa aina hii washughulikiwe ipasavyo, ili waweze kutoa huduma za biashara kwa kila mtu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kuna biashara za mafuta; *engine* zetu hizi za magari ninafahamu kwamba zinaungwa kwa *specification* maalum, kwamba *engine* hii itatumia mafuta ya aina fulani, na *engine* hii itatumia mafuta ya aina fulani, yaani hiyo *petrol* inaweza kuwa iko ya aina mbili ama tatu. Lakini hapa tunapata mafuta ya aina moja tu sijui ya rangi nyekundu na yale sijui ndio *super* au *ordinary* hatuwezi kujua ni ya aina gani.

Kutokana na hali hiyo, *EWURA* pamoja na wote wanaohusika walitilie maanani suala hili na tupate mafuta ya aina zote zinazohitajika kwa *engine* za aina tofauti, kwani hali hii peke yake ndio itakayowezesha vyombo vyetu vidumu kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie suala la utalii. Umesisitizwa sana utalii kwa wote na mimi naunga mkono sana utalii kwa wote, kwani ndio njia moja ya kukuza uchumi, yaani utalii wa ndani pamoja na utalii kwa wote. Hivyo, nashauri sana tuimarishe utalii wa ndani, na siku hizi kuna mtindo vijana wanapenda sana kwenda *day out* na hii ni aina moja ya utalii. Mhe. Naibu Spika, ni vyema hii tuimarishe, ili vijana waweze kwenda kupumzisha nafsi zao pamoja na kubadilishana mawazo.

Mhe. Naibu Spika, sasa nizungumzie kuhusu suala la kilimo na ninakwenda haraka haraka ili na wenzangu wapate kuja kuchangia. Suala la kilimo zamani tulikuwa tunasema uti wa mgongo, na hivi sasa utalii ndio uti wa mgongo, kwa sababu ndio uko mbele kwa uchumi, lakini bado ipo haja ya kukiendeleza kilimo.

Kwa mfano, wenzetu Malaysia nilipata nafasi ya kwenda Malaysia nikaona kuna mafenesi, madoriani, yaani kuna kila zao linalopandwa hapa, sasa niliona mafenesi yao kule linakuwa fenesi ambalo hata yale mashabuka kwa kule kaskazini tunaita hivyo, unakuta fenesi nyama tupu na limeviringika vizuri. Vile vile, madoriani nayo halikadhalika, yaani wenzetu wanafanya halua ya madoriani ambayo ni nzuri sana, ukiachilia mbali mipunga inayozalishwa kwa kiwango kikubwa sana, na hapa kwetu bado uzalishaji wa mazao hayo ni mdogo sana. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nashauri si vibaya tukaiga, kwa sababu nadhani wengi sana tumepata nafasi ya kwenda huko Malaysia, kama mbegu zetu haziruhusu kama vile basi tuchukue mbegu kule, kwa sababu naona hakuna tofauti ya hali ya hewa, yaani hali ya hewa ya kule ni sawa na ya hapa na kila mazao yaliopo hapa na kule yako, kama vile minazi na mengineyo. Hivyo, naomba sana tuige mifano kutoka kwa wenzetu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, umebakisha dakika tatu.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Mhe. Naibu Spika, sawa nitajitahidi. Sasa naomba nizungumzie suala la mazingira na sote sisi tunategemea mazingira lakini pia mazingira yanatutegemea sisi. Kwa mfano, ingekuwa hakuna binadamu ni miti tu inaota, nadhani ingesongomana na kusokotana na mwisho wake ikawa haipo, lakini mwadamu anakata na hasa akikata kwa uangalifu basi miti ile inazidi kunawiri, vile vile sisi tunategemea hiyo miti kwa ajili ya kupata hewa ya *oxygen* na afya zetu kuwa nzuri.

Kwa hivyo, ni vizuri tuyatunze mazingira, na visiwa vya wenzetu vimezama kwa mfano kisiwa cha Kiribati kimezama na wala si miaka mingi iliyopita kwa sababu ya kuharibu mazingira. Kutokana na hali hiyo, kuna haja ya kuvihami visiwa vyetu, ili visije vikakutwa na janga hilo la kuzama.

Sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la ajira. Kwa kweli kuna haja kubwa sana ya kuweka mkazo mkubwa kwa vijana kuwaajiri, kwa sababu hii itatusaidia kuwaepusha vijana hawa kuingia kwenye madawa ya kulevya na shughuli nyengine ambazo hazina tija.

Kwa maana hiyo, naunga mkono wenzangu waliosema kwamba viwanda viwemo na ile *SME's*, yaani kuna mtaalamu wa *SME* nafikiri Mhe. Haroun Ali Suleiman anamfahamu Dkt. Rajim yupo hapa ametoka Burundi,

amefanya kazi Rwanda na amefanya kazi nzuri sana, na ujasiriamali Rwanda kule umechukua nafasi nzuri na wajasiriamali kule wanafanya kazi vizuri sana. Hivyo, nafikiri tukimtumia mjasiriamali huyu tunaweza kupiga hatua nzuri.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nizungumzie kuhusu sekta ya afya. Kwa kweli, mtu ni afya na bila ya afya binadamu huwezi kufanya lolote. Tunavyo vituo vyetu vya afya vingi sana, lakini ukiangalia vile wanavyoziweka zile takataka za hospitali utakuta *plaster* pamoja na mabendeji zimetupwa tu katika mazingira ya hospitali.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, muda wa ku-*wind up* umekwisha, hivyo malizia.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hotuba ya Mhe. Rais kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi, ahsante sana. Sasa mchangiaji mwengine atakayekuja ni Mhe. Abdalla Maulid Diwani, atafuata Mhe. Zulfa Mmaka Omar na ajitayarishe Mhe. Mihayo Juma N'hunga.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kuchangia hotuba ya Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia uzima wa afya wakati huu kuwepo hapa kwa ajili ya kuendeleza shughuli zetu za Baraza la Wawakilishi.

Vile vile, Mhe. Naibu Spika, nataka nikupongeze wewe kwa ushindi wako wa kuteuliwa kuwa Naibu Spika katika Baraza hili la Tisa, hongera sana, umeonesha imani kwa wapiga kura wako kiasi gani kwamba kweli wanawake wanaweza bila ya kuwezeshwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Spika Zubeir Ali Maulid kwa kupata nafasi hiyo, najua ni kijana mwenzetu tumempa imani na tunajua kwamba na yeye hatotuangusha. Naomba niwapongeze na wenyeviti wetu waliopata nafasi hiyo pamoja na makamishna wetu wa Tume ya Bajeti. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naomba kuchukua fursa hii kwa dhati kabisa kuwapongeza wananchi wangu wa Jimbo la Jang'ombe kwa kunipa ushindi wa kishindo wa asilimia 93.7, na leo hii nikawepo hapa katika Baraza la Wawakilishi, ambacho ni chombo muhimu kabisa cha kutunga sheria katika nchi hii, kwa ajili ya kumsaidia Mhe. Rais wa Zanzibar na kuendeleza mbele gurudumu letu la maendeleo Zanzibar. *(Makofi)*

Nikiendelea na pongezi sasa naomba nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar kwa ushindi wa kishindo wa asilimia 91, kuonesha wazi kwamba na mwaka huu aliahidi kuwa atafanya maajabu na atahakikisha upinzani Zanzibar unapotea, na kweli umepotea.

Mhe. Naibu Spika, nafikiri hivi sasa wako nje wanapeana dripu ambazo hazina msingi, ukitembea utaambiwa uchaguzi utarudiwa mwezi wa 10, lakini mwezi wa 10 huo ni mwaka 2020 na sio mwezi wa 10 mwaka huu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nichangie kuhusiana na hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar. Nianze mchango wangu na kujikita katika vyombo vyetu vya kukusanya mapato *TRA* na *ZRB*.

Kwa kweli, ni vyombo ambavyo vinafanya kazi vizuri sana na vinajitahidi kwa upande wa *TRA* hivi sasa kila siku wenzetu Tanganyika wanavuka malengo mpaka wamefika kukusanya trilioni 1.7. Vile vile, na kwa upande wa Zanzibar na wao wanajitahidi wamefika kukusanya bilioni 300 na kitu kwenda bilioni 400. *(Makofi)*

Lakini, kuna changamoto ambazo ni kushindwa kuwahudumia wananchi katika *level* moja, nina maana gani kusema hiyo. Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwamba kuna baadhi ya wananchi katika nchi hii wanapata huduma tofauti na wengine sijui kutokana na uwezo au umaarufu wao. Kwa mfano, kwenye *TRA* kuna falsafa moja kuna fomu ya C35, ambayo ni *Central Transportation*, ambapo Wazanzibari kwa asilimia 90 hawawezi kuitumia fomu hii, lakini Mzanzibari mmoja anatumia na kufanya anavyotaka katika nchi hizi mbili, yaani Tanzania Bara na Zanzibar.

Kwa maana hiyo, kuhusu masuala ya kusafirisha magari yetu, sisi au wapiga kura wetu wanazo gari wanahitaji kwa namna moja au nyengine kuvusha magari yao kwenda sehemu ya pili ya muungano. Lakini kwa bahati mbaya inakuwa ni tatizo ambalo haliwezi kuepukika, ukifika pale utaambiwa lazima uweke *deposit* fedha nyingi tu, lakini mwenzetu huyo anavusha gari zake kwa mujibu anavyotaka mwenyewe, leo anaipeleka hapa, kesho Pemba na kesho kutwa Unguja. Sasa sijui huyu kwa utaratibu gani anafanya unaomuwezesha kufanya hivyo na wengine wasiweze.

Mhe. Naibu Spika, hilo sio jipu nafikiri ni kumri kabisa ambalo linataka kutolewa mpaka moyo, japokuwa Mjumbe aliyepita alisema atatembea na mikasi kwa ajili ya kukata pia kuna na makumri. *(Makofi)*

Sasa naomba nizungumzie kuhusu sekta ya viwanda. Kwa kweli, tumesema tuboreshe viwanda, lakini viwanda vyetu vya Zanzibar kwa kutegemea soko la Zanzibar ni tatizo sugu, hivyo ni lazima tutegemee soko la upande wa pili ambapo kule ndio kwenye mahitaji mengi.

Kwa mfano, leo hii kuna changamoto ya viwanda vya maji Zanzibar viko zaidi ya sita au saba, lakini hakuna mfanyabiashara hata mmoja wa kiwanda cha maji mwenye uwezo wa kutengeneza mali yake kwa ajili ya kutengeneza na kupeleka Tanzania Bara kwa biashara, lakini tujiulize kuna viwanda vingapi Tanzania Bara ambavyo bidhaa zake zimetapakaa katika visiwa vya Zanzibar. Sasa hizo ni kero za muda mrefu sana na kila siku tunaambiwa kero. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nafikiri kitabu hiki cha hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar kimemaliza kila kitu. Hivyo, kama tutakuwa makini sana bila ya kufuata ule mwenendo wetu wa *business as usual,* tutakuwa hatufanyi kitu. Lakini hiki kitabu kama tutakisimamia kweli, basi itakuwa msahafu tosha wa kutupeleka huko ambapo wanakohitaji wenzetu na japo wao walitaka kwenda Singapore na sisi nafikiri tutakwenda Brunei kwa kitabu hiki, kwa sababu yamo mambo mengi mazuri ambayo Mhe. Rais ameyaona. *(Kicheko/Makofi)*

Naomba kutoa ushauri kwa watendaji watakaoteuliwa na Mhe. Rais kwa nafasi za uwaziri tuondoshe muhali kama Mjumbe aliyepita alivyozungumza, kwamba ni kweli kuna mambo tukiondosha muhali tunaweza kuiondoa Zanzibar hapa ilipo sasa na tukajisifia hasa kama Baraza la Wawakilishi la Tisa limefanya kazi kubwa sana kuweza kuing'arisha Zanzibar. *(Makofi)*

Sasa naomba nizungumzie suala la Bandari. Mhe. Naibu Spika, bandari yetu ya Zanzibar hivi sasa kusema kweli haikidhi haja nafikiri kama ni ndoo basi inamwagika, kwa sababu mpaka hivi sasa ndani ya bandari yetu ya Zanzibar kuna kontena zaidi ya 2,374, ambapo uwezo wa bandari ile ni kontena 1,500 na kuna meli zaidi ya tano ziko nje muda huu na nyengine zinatishia kutoshusha mzigo Zanzibar kuondoka na kuelekea Tanzania Bara kutokana na kwamba nafasi ndogo na vitendea kazi vya bandari havipo.

Kwa hivyo, wakati tunapanga au tunaizungumzia hotuba ya Mhe. Rais na tunaisifu sana sisi kwamba ni hotuba nzuri, lakini tunatakiwa tuwe waadilifu katika kuisimamia hotuba hii, kwa sababu imechambua kila kitu.

Mhe. Naibu Spika, katika hilo nafikiri watendaji watakaoteuliwa warudie ule mpango wao maalum wa kuweza kupunguza ule mizigo uliomo ndani ya bandari, yaani zile kontena *at least* zitafutiwe sehemu ziwekwe na zile zilizomo kwenye meli ziweze kushushwa, ili watu wetu wapate huduma sawa sawa na kupata mizigo yao. Nafikiri kama hatukufanya hivyo Mhe. Naibu Spika, si muda mrefu sana ujao tunaweza kukosa biashara kubwa tu na ukilinganisha hivi sasa tunategemea lango letu lile kwa ajili ya kuendeleza uchumi wetu wa Zanzibar.

Vile vile, kuhusiana na suala la maji safi na salama Mhe. Naibu Spika huku ndio jipu ambalo halina hata mfano. Katika vitabu vyetu tunaambiwa huduma za maji hivi sasa zinapatikana kwa asilimia 87 kwa mjini na asilimia 70 kwa vijijini. Jambo ambalo kwenye makaratasi au vitabu ni kweli, lakini hali halisi haiko hivyo, yaani uhalisia wa mali katika miji yetu ni bado na mimi naweza kusema kwamba hata asilimia 50 hatujafika, lakini kwenye vitabu vyetu tunaambiwa zaidi ya asilimia 87.

Kwa kweli, jambo hili nadhani tulichukulie maanani katika serikali itakayoundwa kupitia mawaziri na suala hili lisiwe linaimbwa tu na liwe linasimamiwa ipasavyo, ili haya yanayozungumzwa hapa yaendane na ukweli na wala yasiwe kama hivi ambavyo tumeambiwa kuna asilimia 87, lakini ukienda katika mitaa yangu kule kama vile Matarumbeta, Kidongochekundu, Jang'ombe suala la maji ya mfereji imekuwa historia. Kutokana na hali hiyo,

wananchi wetu wale wanachimba visima, waheshimiwa waliopita pamoja na waliopo hivi sasa kwa ajili ya huduma za maji. Sasa tunapoambiwa kwamba maji yanapatikana kwa asilimia 87 mjini inakuwa kidogo haingii akilini.

Mhe. Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu suala la ajira. Kwa kweli, katika suala hili ni ghasi zaidi, kwa sababu kila siku tukikaa tunaambiwa kwamba kuna ajira hazitakiwi kufanywa na wageni katika nchi hii, lakini jambo la kushangaza katika nchi hii ndio watu hao walioko kwenye nyadhifa zao wanatoa vibali (*work permits*) kwa watu ambao ni wageni wako Zanzibar.

Lakini tukikaa huku tunasema ajira wageni wasipewe au mgeni aje ambaye *more educated*, yaani mwenye uwezo mkubwa ambaye hapa hayupo, lakini utakuta kwenye taasisi zetu unakuta watu kwa mfano *human resource* pia atoke Kenya, inakuwaje *human resource* atoke Kenya wakati sisi wenyewe Wazanzibari wapo wengi tu ambao waliosoma masuala ya *human resources* na wala sio hayo tu mengi sana, lakini tukikaa humu tunasema ajira zisitoke, hamna, kumbe vile ajira zipo tunazitoa tofauti na tunavyotaka.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la uwajibikaji. Mhe. Naibu Spika, ndio maana huku mwisho kunahitaji uwajibikaji wa dhati kabisa, tutakapokuwa kweli ni wawajibikaji na kila mmoja akatimiza wajibu wake nafikiri hizi kelele tunazopiga hivi sasa zitakuwa ni historia na wala hatutazisikia tena, na badala yake tutasikia kinyume chake kwamba watu wamefanya mambo mazuri katika nchi hii. Kwa kweli, haya yote Mhe. Naibu Spika, yanawezekana kila mmoja akitimiza wajibu wake. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la michezo na Mhe. Rais wa Zanzibar alizungumzia. Hivyo, nathubutu kusema kwamba nimefurahi sana kuona kitu ambacho nilikitoa mimi mwenyewe kwa akili zangu na leo hii kimekuwa ni kitu cha kitaifa. Kwa kweli, suala la bonanza la mazoezi ya viungo Mhe. Naibu Spika, mimi ndiye niliyebuni wazo lile na mpaka leo hii limekuwa ni suala la kitaifa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi ni Msaidizi Mwenyekiti wa *Club* ya Mazoezi ya Kitambinoma, tulikaa kwa nia safi kabisa tukaona tufanye kitu gani kwa Zanzibar *at least* tuweze kuwakusanya watu wetu wawe wenye kufanya mazoezi ndio nikabuni wazo hili, na leo hii ndio limekuwa suala la mazoezi. *(Makofi)*

Kwa kweli, suala hili linasaidia Wizara ya Afya kupunguza mahitaji ya dawa, kwa sababu utakapokuwa unafanya mazoezi na kufuata miiko ya mazoezi basi matatizo mengi yanakuondoka, kwa mfano ugonjwa wa sukari, *pressure* pamoja na mambo mengine kama *obesity*. Kwa hiyo, badala ya kutumia dawa mazoezi inakuwa dawa tosha, kupunguzia mzigo serikali yetu kuagiza madawa kwa wingi na hata kuwapeleka wagonjwa wetu kwenda kutibiwa India, lakini sasa nalo limekuwa tatizo, kwa sababu wale wa kwenye mazoezi hawafanyi mazoezi yanayohitajika. Sasa tunaomba vile vile kwa Wizara ya Michezo itakapokamilika basi watafutwe walimu maalum kwa ajili ya mazoezi ya viungo, kwa sababu haiwezekani mtu una kilo hamsini bado unafanya mazoezi sawa sawa na mtu mwenye kilo sabini au thamanini, nini unapunguza, ina maana unajiumiza mwenyewe nafsi yako, elimu kwa wafanya mazoezi haijatosha na haijatolewa kwa kiwango cha kukidhi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile katika suala la rushwa. Rushwa kweli ni adui wa haki, ni adui mkubwa sana ambaye kwa kumuimba humu tunamuimba sana lakini kwa kutekeleza na kumsimamia bado. Sasa hivi imefika *time* mtu ununue haki yako ndio na wewe uweze kupata huduma yako, hilo suala linajulikana, lakini cha kushangaza mpaka dakika hii tumeunda hapa chombo cha kuzuia rushwa Zanzibar lakini naona kidogo kama meno yake hayana makali, kwa hivyo tunaomba kupitia Baraza hili au Wizara itakayoundwa nafikiri chini ya Makamo wa Rais kwamba ile taasisi ifanye kazi na iwe na meno.

Rushwa ziko za aina nyingi sana, kuna mpaka rushwa za ngono katika nchi hii zinafanyika katika wale wenzetu wanaoomba kazi mahotelini, mbali sehemu nyengine za utoaji wa huduma kama bandarini na sehemu nyengine. Rushwa zimetawala na kila siku tunarudi nyuma katika suala kama hilo.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, sitaki niseme mengi sana unajua muda sio rafiki sana, lakini mimi nasema naunga mkono hotuba ya Rais kwa asilimia mia moja. Kwa niaba yangu na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo langu la Jang'ombe tunaisimamia na tunaikubali kwa pamoja kushirikiana na Rais kuhakikisha tunaleta maendeleo katika nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi kabla ya kumaliza napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa familia yangu kwa kuwa sambamba na mimi katika harakati zote hizi tokea mchakato mpaka kuniwezesha leo kuingia katika Baraza la Wawakilishi.

Vile vile shukurani za pekee zimuendee mke wangu anayenipendezesha mpaka nikawa humu leo katika Baraza hili na kuniondosha wasi wasi, hofu ya nafsi yangu na kuwa mtulivu. Naunga mkono hoja ahsante sana.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia katika Baraza hili. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *subhana wataala* kwa kutuwezesha leo kufika hapa katika hali ya uzima tukiwa na furaha katika Baraza hili.

Nianze kwa kuwapa pongezi umoja wa vijana na kuwashukuru kwa kunichagua kuwa ni Mwakilishi ambaye nitawawakilisha vijana katika Baraza hili.

Pili niwashukuru Umoja wa Wanawake Tanzania kwa kuniamini na kunipa kura nyingi ili niweze kushirikiana na ambao wamo humu katika kutetea maslahi ya nchi yetu, pia niwashukuru familia yangu kwa kuwa pamoja na mimi bega kwa bega kipindi chote cha harakati za kutafuta uhuru wa nchi yangu, nawashukuru sana na nawaahidi tupo pamoja.

Mimi naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Rais kwa asilimia mia moja na nina sababu zangu. Mhe. Rais nishukuru kwa kuzungumzia suala la ajira, suala la ajira ni tatizo kubwa sana hasa kwa vijana wengi sana wanapigia kelele suala la ajira.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais kuna nafasi mbali mbali ambazo zinatolewa ili vijana waende kuomba katika Tume ya Utumishi, ila kwa masikitiko makubwa Tume hiyo ya Utumishi inatangaza hizi ajira wanataka watu waombe lakini wakishakuomba hawa watu haifanyi haki hata kidogo.

Mhe. Naibu Spika, Tume hii ya Utumishi inatangaza ajira zao lakini wakati wa *interview* unakuta watu wengi wanafanya ila sasa wakati wa matokeo ajira zile zinatoka kwa watu ambao wanajulikana, wana uhusiano na zile Afisi ambazo zimetoa zile ajira. Kwa hivyo namuomba Mhe. Rais namuomba sana huko katika Tume ya ajira atupie jicho kidogo vijana wanalilia sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimpongeze Mhe. Rais kwa kuwataja watoto na nimpongeze kwa kuweka Mahakama ya watoto kwa sababu watoto ndio furaha yetu. Sisi wazazi, kwa sababu mimi pia ni mzazi, tunakuwa tunapata maumivu makubwa sana pale watoto wetu wanapofanyiwa masuala ya uharibifu inatuuma sana, lakini sasa naamini Mhe. Rais alipoweka hii Mahakama ya watoto naamini sasa hizo kesi zitafuatiliwa kwa undani zaidi na hao ambao wameamua kufanya uharibifu wa watoto watakomeshwa na wataacha.

Mhe. Naibu Spika, mimi nigusie suala la miundombinu. Nimpongeze Mhe. Rais kwa kulitaja hili suala, kwa kweli tunashukuru sana wananchi wote kwa sababu hapo kipindi cha nyuma ilikuwa safari ya meli mbili unaiona kama safari ya meli kumi, lakini kwa sasa barabara zote unazikuta ni mgongo wa ngisi.

Mhe. Naibu Spika, kule Pemba barabara nyingi sana sasa hivi unaweza kuendesha gari huku unasikiliza mziki bila ya matatizo yoyote, kwa sababu barabara zote ni laini kabisa tumshukuru Mhe. Rais na tunamwambia kwamba sisi wananchi tunafurahi na mambo hayo na tunamuahidi kuzilinda.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia nimshukuru Mhe. Rais kwa kutuwekea viwanja vyetu vya ndege vizuri, kwa sababu Pemba kipindi kikubwa sana ndege zilikuwa zinaishia saa kumi na moja na nusu, kwa kweli mgonjwa anaweza kuumwa akaambiwa asafirishwe ilikuwa ni ngumu sana hadi asubiri siku ya pili saa mbili ndio ndege inatua, lakini kwa sasa hivi Pemba yang'ara, *time* yoyote sasa hivi ndege inashuka tunapanda tunakwenda zetu Tanga, tunakwenda Unguja, namshukuru Mhe. Rais kwa kuliona hili tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia nimpongeze Mhe. Rais kwa sehemu ya elimu kiwango cha uandikishaji kimezidi hadi kufikia asilimia mia moja kwa mwaka 2020 tumpongeze sana.

Pia nampongeza kwa kuzidisha mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kwa sababu hapa tunaona hadi kufikia mwaka 2020 kuna wanafunzi elfu ishirini na mbili, mia nne na nne (22,404) ambao wanatarajiwa kupata mikopo hii, kwa hivyo hiyo ni hatua kubwa na tunampongeza sana.

Mwisho niseme kwamba mimi na vijana wenzangu tunaipongeza hotuba hii kwa asilimia mia moja, na tutaifanyia kazi na tutayaendeleza yale yote ambayo wametutaka tuyafanye. Tunaahidi kwamba sisi tupo kwa ajili ya kazi. Ahsanteni. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Tunakushukuru sana Mhe. Zulfa kama mwenyewe unavyosema sana sana sana, kwa hivyo tunakushukuru na tunakupongeza kwa mara ya kwanza kuweza kuchangia vizuri sana katika hotuba ya Rais. *(Makofi)*

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona nami kuweza kunipa fursa hii ili kuweza kuchangia katika hotuba hii ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye yeye kwa hekima yake na busara zake ameendelea na ametuweka kwa pamoja mpaka kufikia muda huu.

Pili nitumie fursa hii kuwapongeza wananchi wote wa Zanzibar wenye itikadi tofauti za vyama vyao, kwa kuliweka Taifa letu katika hali ya amani mpaka kufikia muda huu, lakini pia naomba nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa jimbo langu la Mwera kwa kunisaidia, kwa kunikubali na kwa kuhangaika katika kipindi chote cha kampeni kwa chaguzi zote mbili. Kama ambavyo nimezungumza mwanzo nawashukuru sana wananchi wangu wa jimbo la Mwera, wote; vijana, kinababa na kinamama sambamba na wazee ambao walionesha mshikamano kwa kijana wao ambaye wameweza kunilea kwa kipindi chote na kunipa ridhaa ya kuja kuwawakilisha katika mhimili huu mkubwa katika Taifa letu, kwa hili nasema nashukuru sana. *(Makofi)*

Pia nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wawakilishi wote waliochaguliwa kutoka katika majimbo yao na wale ambao wameteuliwa kutoka katika jumuiya za wanawake, taasisi za walemavu, na hata wale ambao Mhe. Rais ameweza kuwateua jana bila ya kutizama itikadi ya vyama vyao ili kuja kuungana nasi katika kupigania na kutetea maslahi ya Taifa hili, kwa ujumla niseme hongereni sana.

Aidha nichukue fursa hii kutoa pongezi kwa Mhe. Spika, Mhe. Zubeir Ali Maulid, kwako Mhe. Naibu Spika, sambamba na Wanyeviti wetu kwa kuliendesha Baraza hili, maana Baraza limewaamini na tuna imani, imani mliyoipata ni kubwa na mumeonesha weledi mkubwa wa kuweza kuendesha mhimili huu kwa misingi iliyokuwa mizuri, kwa hili hongereni sana.

Mhe. Naibu Spika, nitumie fursa hii ya kuwapa pongezi tena na kulishukuru Baraza hili maana katika mara hii tumeona Baraza ambalo limeweka uongozi kwa kuangalia *gender balance* Spika, mwanamme lakini pia tuna Naibu Spika, mwanamama hodari ambaye anajua majukumu yake kwa kufuata kanuni na sheria, hongera sana.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba niende moja kwa moja katika hotuba iliyotolewa jana na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Tuna kila sababu ya kusifia hotuba hii iliyotolewa jana na Mhe. Rais, kwangu mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mwera, na kwa niaba ya salamu za vijana Mkoa wa Magharibi wanasema Mhe. Rais amewakonga nyoyo sana Wazanzibari. Kwa jumla, Mhe. Rais ametoa dira mpya ya Wazanzibari ya mwaka 2016 kuelekea mwaka 2020, maana kwa yale yote yaliyomo katika kitabu hiki ukweli yanasadiki dira ya maendeleo na mabadiliko hasa katika Taifa ambalo linataka kutoka katika uchumi tegemezi kwenda katika uchumi wa kati.

Imani yangu kwamba kama kitabu hiki kitapata fursa za kupelekwa na kugaiwa kwa watendaji wote wa idara na Taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, basi tunaweza kufikia katika hatua nzuri ya kuleta maendeleo kwa kutumia dira ambayo Mhe. Rais ameweza kutuonesha hapo jana.

Mhe. Rais katika hotuba yake ameweza kugusia mambo mengi kwa manufaa na maslahi ya taifa hili, mambo ambayo kiukweli kama yataweza kutekelezwa bila ya kutizamwa mtu, bila ya kutizama itikadi ya mtu na bila ya

kutizama kujuana ama ile wanayosema muhali katika Taifa letu, tunaweza kupiga hatua moja kubwa sana, miongoni mwao ni sambamba na haya ambayo nitayagusia kama ambavyo Wajumbe wenzangu wameweza kuyagusia.

Mhe. Rais aligusia maeneo ya Miradi hasa miradi ya Fumba na kule Micheweni miradi ambayo kwa namna moja au nyengine itakapoweza kutekelezeka itaweza kuleta taathira nzuri na sura mpya ya taifa letu na nchi yetu ya Zanzibar hasa katika kipindi hichi, lakini katika kipindi chote cha miradi wakati inatekelezwa itaweza kutoa nafasi na fursa nyingi za ajira hasa kwa vijana wenzetu na watu tofauti ambao watakuwa wakihitaji kujipatia kipato kwa namna moja au nyengine katika kipindi chote cha utekelezaji wa miradi hiyo.

Pili nipongeze fursa ambayo aliitangaza rasmi jana Mhe. Rais kama ambavyo alikuwa akipita katika mikutano yake ya kampeni ya kusema kwamba katika Serikali hii ya kipindi cha 2016/2020 atakuwa na kila sababu ya kuhakikisha kima cha mshahara wa chini wa kila Mzanzibari aliyekuwepo katika nafasi ya ajira basi kinaongezeka mpaka kufikia kima cha shilingi laki tatu, kwa hili naomba tumpongeze sana Mhe. Rais, lakini kwa hili pia lazima tuweke miundombinu ambayo itaweza kusimamia katika mirija na maeneo yetu yote kwa kuweza kukusanya kodi na mapato ili kuweza kutimiza azma hii, maana dhamira hii njema ya Mhe. Rais katu haitaweza kubadilika kama hakutokuwa na makusanyo mazuri ya mapato katika taifa letu, lakini kama hakutokuwa na utekelezaji mzuri wa ilani ya Chama cha Mapinduzi katika idara mbali mbali pia lengo hili la Mhe. Rais linaweza lisitokee, tunaomba sana watendaji ambao watapata fursa, Mawaziri na Manaibu Waziri kwa kushirikiana na watendaji wa Idara za Serikali kuweza kuyafanya haya katika jukumu la kukusanya kodi na mapato katika taifa letu ili kuja kuongeza kima cha mishahara katika taifa letu.

Pia nchi yetu tupo katika mazingira ya visiwa tunasema maeneo yote tumezungukwa na bahari, hivyo mpaka kufikia sasa tuna kila sababu leo Taifa letu la Zanzibar likaweka uwekezaji makini hasa katika shughuli za uvuvi wa bahari kuu. Tunajua miundombinu mingi ya uvuvi bado haijawekwa katika hatua zilizokuwa nzuri, maana fursa hii ya uvuvi ni miongoni mwa mambo ambayo yanaweza kutoa fursa nyingi za ajira hasa kwa watu ambao wapo katika maeneo yote ya pwani. Na Serikali sasa kama ambavyo Mhe. Rais ameweza kubainisha itaweza kutoa mikopo nafuu kwa watu kupata vyombo vizuri kwa ajili ya uvuvi katika maeneo yetu, na hii itaweza kusaidia sana kwa kuzalisha fursa mbali mbali za ajira katika maeneo yetu, jambo ambalo litaweza kuipunguzia Serikali mzigo wa kubeba watu ambao wanaweza kupata fursa nyengine za kuweza kuwajibika na kuisaidia Serikali na taifa kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala zima la ajira kwa vijana. Hapa Mhe. Rais aliweza sana kulisemea suala hili sambamba na kinamama na vijana. Bahati nzuri na Mheshimiwa Mjumbe ni miongoni mwao waliopita wameweza kulizungumzia suala hili la mikopo kwa vijana na kinamama, 2010 mpaka 2015 tumeona kwa kiwango kikubwa sana Mawaziri wetu wameweza kusaidia akinamama zaidi ya asilimia 90 kupata mikopo katika vikundi vyao vya ushirika, jambo ambalo ni jema na linafanya angalau kinamama hawa katika maeneo yetu kuweza kujitegemea na kuacha kuwa tegemezi hasa kwa kinababa ndani ya familia zao.

Pia mara hii tunaomba jukumu la nguvu zile ambazo ziliwekwa hasa kuweza kuwekeza kwa kinamama basi tunaomba elimu ile na hekima zile pamoja na busara zile zianze sasa kwenda kuwaelimisha vijana kuhusiana na elimu hii ya mikopo na shughuli za kufanya, maana Taifa hili zaidi ya asilimia 65 sasa linaongozwa na vijana. Sasa kuliacha tabaka hili lenye idadi kubwa ya watu katika Taifa letu, bila ya kuwa na misingi mizuri ya ajira itakuwa ni suala gumu na kitu ambacho kitaweza kutufikisha pabaya kwenye Taifa letu hili.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Rais jana amezungumzia suala la amani katika Taifa hili, na mimi nitumie fursa hii kuvipongeza sana vikosi vyetu vya ulinzi na usalama; vile vya SMZ na SMT. Ni kwamba vimefanya kazi kubwa, vimefanya kazi nzuri na vimefanya kazi ngumu ya kuhakikisha Taifa hili linaendelea kubaki katika hali ya usalama pasi na kutetereka kwa namna moja ama nyengine. Tunawashukuru sana sasa sambamba na hilo kadri ambavyo Mhe. Rais aliweza kuviongeza vikosi vyetu hivi vya SMZ tuna kila sababu navyo sasa angalau kuviongezea mishahara yao ikaweza kulingana na ile ya wenzetu wa SMT. Kwa kufanya hivyo tutaweza kuzalisha ari mpya ya kazi na ulinzi hasa kwa vikosi vyetu hivi, lakini kwa kuwawezesha na kuwatekelezea maslahi yao katika maeneo yao ya kazi kutaweza kuisaidia na kutaweza kuwafanya hata wao wale ambao walikuwa wakiichukia serikali yao, na waliokuwa wakifanya *sabotage* kwa namna moja ama nyengine kutokana na kima kidogo cha mshahara kitarudisha *morality* nzuri na kulifanya taifa hili likawa katika misingi bora na mizuri hasa katika mambo ya usalama.

Mhe. Naibu Spika, vile vile Mhe. Rais jana amezungumzia pia masuala ya miundombinu hasa ya barabara na mengine. Wakati tunazungumzia suala la miundombinu ni sawa na kusema ni pale ambapo ameweza kuzungumzia suala la mipango miji. Hatutakuwa na mipango miji mizuri kama hatutokuwa na miundombinu mizuri ya barabara, lakini tunapoweka miundombinu mizuri ya barabara pia tunaweka mazingira mazuri ya kuwa na *public transport* hasa katika maeneo yetu.

Mhe. Naibu Spika, hapa tunaona katika kipindi cha 2010 kuja 2015 katika kuelekea kutafuta mambo mazuri ya uwekezaji, serikali iliamua kulichukua eneo la Darajani hasa pale kwenye kile kituo cha daladala. Leo kituo kile kimeweza kuhamishwa na kuwekwa pale Kisiwandui Michenzani.

Ukweli wakati tunapeleka sera katika mipango miji lakini mipango miji bila ya kuwa na kituo kizuri cha daladala, mipango miji bila ya kuwa na kituo cha uhakika cha daladala ukweli ni kwamba Mhe. Naibu Spika watu wetu wananyanyasika, watu wetu wanasumbuka kwa hili lakini Wazanzibari wengi wanahangaika kutokana na kutokuwa na *stable stand* ya daladala, maana pale walipo hawana uhakika hasa na shughuli zao wanazozifanya. Vile vile eneo lile pia bado ni dogo kana kwamba haliwezi likakidhi haja ya vipando vyote ama daladala zote ambazo zinafika katika eneo lile kuweza kutoa huduma za jamii.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende katika suala la umeme na maji, tunamshukuru Mwenyezi Mungu Mhe. Rais kajitahidi sana na serikali yake yote kwa ujumla katika eneo hili la kufanikisha kusambaza huduma za maji na umeme maana ni msingi na ni miongoni mwa mambo ya maendeleo katika Taifa letu. Taifa ambalo bado halitakuwa na umeme wa uhakika hatuwezi kufikia katika uchumi wa kati kama hatutokuwa na miundombinu ya uhakika hasa ya umeme, lakini hatuwezi kufikia katika uchumi wa kati hasa kama hatutokuwa na vyanzo vya uhakika vya maji.

Mhe. Naibu Spika, mimi naumwa sana na suala la maji, maana maji ndio kila kitu tunasema maji ni uhai, maji ndio kila kitu katika maisha yetu ya kila siku. Ukweli usiofichika katika maeneo yetu mengi ya Zanzibar hili suala la maji bado lina tatizo sana, na lina tatizo kwa namna mbili ambazo mimi nimeweza kuziona. Moja, kama ambavyo Mhe. Soud aliweza kubainisha kwamba bado kuna muhali katika mashirika yetu haya, ule muhali tulionao unaweza kuwafanya wale watendaji wadogo wadogo kufanya *sabotage* za makusudi kwa serikali ili kuonekana idara zile kuwa hazifanyi kazi na wala hazitendi majukumu yao hali ya kuwa serikali ina dhamira njema ya kuhakikisha huduma hizi za msingi za maji na umeme zinawafikia wananchi wote kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, bahati nzuri Shirika letu hili la Maji (*ZAWA*) limekuwa na utaratibu wa kuchimba visima, na katika kipindi kirefu tuna visima vingi na bado tunaendelea kupokea misaada mingi ya kuhakikisha tunaweza kuchimba visima vingi kwa ajili ya kutatua na kupunguza tatizo la maji katika taifa letu. Lakini katika vile visima vya zamani tumeweza kuona kutokana na watu kukua na kupata maendeleo katika maeneo, tumeweza kuona watu sasa hivi wameweza kufika katika yale maeneo ambayo yalikuwa na visima, jambo ambalo kwa namna moja ama nyengine inapelekea ule upatikanaji wa maji kuwa mdogo, lakini inapelekea ule upatikanaji wa maji katika vyanzo asilia ikapungua hasa kama kile cha Mwanyanya na hasa katika vile visima vya maeneo ya kwetu ya Mwera.

Mhe. Naibu Spika, kwa wananchi kufanya hivi kukimbilia katika vyanzo vya maji kunapelekea hatari kubwa mno. Moja, upungufu wa kina cha maji unazidi kuongezeka hali yakuwa mahitaji pia nayo yanaongezeka. Lakini pili, hali ya afya inakuwa pia ni hatari maana katika maeneo haya ndio maeneo ambayo kuna *drainage system* za maji machafu yanaweza kupenya katika maeneo yetu haya ya visima. Na sisi tumezoea maji yale ya kuchimba katika visima tunaamini kwamba ni bora na safi.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hili kwa faida ya Wazanzibari hasa katika kipindi hiki sote tunafahamu sasa hivi taifa letu limevamiwa na ungonjwa hatari wa kipindupindu, jambo ambalo kila siku tunaendelea kupoteza watu kwa ugonjwa huu hatari wa kipindupindu. Kituo chetu cha Chumbuni kimeshazidiwa na wagonjwa wa kipindupindu hali ya kuwa wamepelekea kufungua kituo kipya katika maeneo ya Mwera Kidogobasi, jambo ambalo kila siku serikali inapokea wagonjwa wapya wanaougua kipindupindu. Lakini haya yote inatokana na kutokuwa na miundombinu mizuri, sambamba na hili nitoe wito ama nitoe rai ni vyema katika kipindi hiki tutoe elimu kwa wananchi wetu kwamba ni vyema tukatumia na tukahamasishana kuweza kuchemsha maji kabla ya kunywa, yale yanayotoka katika mabomba yetu kwa wale wote ambao wananufaika kupata maji haya.

Maana kwa kutegemea usafi wa kule ambako yanatoka hali yakuwa *contamination* ya jamii sasa hivi na makaro haya ya sehemu za kuhifadhia maji machafu hayako katika hali nzuri. Ni vyema mashirika yetu haya, na kwa kutumia taasisi na vyombo vya habari na kuwatumia wanahabari wetu, magazeti, redio pamoja na televisheni wakatumia kipindi hiki kutoa vipindi maalum kwa ajili ya kutoa elimu ya suala zima la kuchemsha maji maana tukishindwa kuzingatia hilo itapelekea kupoteza watu wengi katika taifa letu, tukazidi kupoteza nguvu kazi ya watu jambo ambalo ni la msingi na lenye kuleta tija na maendeleo, maana taifa bila ya kuwa na nguvu kazi ya watu katu hatutoweza kupata maendeleo ya aina yoyote.

Mhe. Naibu Spika, sasa ni vyema na Waheshimiwa Wawakilishi wote tuliokuwemo humu wale ambao wametokana na majimbo yao na wale ambao wamepata fursa…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika tatu.

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana namalizia kidogo.

Na wale ambao wamepata fursa ya kuteuliwa na jumuiya ni vyema tukatumia kipindi hiki tukaenda kutoa elimu hii kwa watu wetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie katika eneo zima la viwanda, kama taifa hili sasa litaweza kutengeneza mazingira mazuri ya kuweka *investment* nzuri hasa katika maeneo ya viwanda, ni ukweli ulio dhahiri kwamba sasa tutaweza kutengeneza nafasi nyingi za ajira, tutaweza kupunguza ule mzigo ambao tuna vijana wenzetu wengi sana mitaani hawana shughuli za kufanya. Maana unapokosa shughuli za kufanya kunapelekea na kuhamasisha kuingia katika mambo mengine maovu na yasiyokuwa na tija katika taifa hili.

Mhe. Naibu Spika, yapo mengi ingawa ninaamini na wenzangu wameweza kuyachangia, lakini nimalizie na hili la mwisho.

Mhe. Rais jana wakati anawasilisha hotuba yake katika taifa hili alizungumzia suala zima la rushwa. Rushwa kweli ni adui wa haki, na tunasema ukweli kama ni majipu yaliyoiva katika taasisi na idara zetu za serikali, suala hili la rushwa lipo katika maeneo mengi sana.

Ukifika pale maeneo ya Bandari ukweli kama hujatoa chochote huwezi kufanikiwa kwa jambo lolote. Sasa Mhe. Naibu Spika, ni vyema tu kwa wale ambao Mhe. Rais ataamua kuwaona kuwa miongoni mwa wasaidizi wake tukalipa kipaumbele suala hili la rushwa, maana suala hili halitakuwa katika idara moja. Suala hili linagusa katika idara zote na kadri ambavyo watu watakuwa wakifanya mambo ya rushwa, ni kadri ambavyo tutaendelea kupoteza pesa nyingi jambo ambalo lingeweza kusaidia taifa letu kwa ujumla.

Baada ya kusema hayo niseme nashukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kupata fursa hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumshukru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima na kutuwezesha kukutana hapa leo hii tukijadili hotuba ya Mhe. Rais.

Pili nichukue nafasi hii kumshukuru sana kwanza kumpongeza Mhe. Rais kwa kuchaguliwa kwa kishindo kwa kura nyingi sana, wastani wa asilimia 91.4.

Vile vile nimpongeze Mhe. Rais kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa jana kwenye Baraza hili, hotuba ambayo imegusa maeneo yote ya kiuchumi, maendeleo ya kijamii, makundi maalum lakini hata masuala ya Baraza letu hili. Kwa kweli hotuba ile ni ya mfano na kama ilivyokwishakusemwa na Wajumbe wengi Barazani hapa kwamba ni hotuba ya aina yake, na kwa kweli ni ya mwaka. Tunampongeza sana Mhe. Rais kwa hotuba ile. (*Makofi*)

Nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, nimpongeze kwanza kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Mahonda, jirani yangu tuko jirani na Jimbo la Donge kwa hiyo namshukuru sana na nampongeza sana kwa ushindi huo. Lakini vile vile nimpongeze Mhe. Balozi kwa imani aliyonayo Mhe. Rais ya kumteua tena kuwa Makamu wa Pili wa Rais. Ni imani yangu na kwa bahati nzuri nilipata nafasi ya kufanya kazi

naye, najua uwezo wake, najua umakini wake, na mimi nasema yeye ni *inspiration* kwangu, na mpaka nikaweza kugombea nafasi hii ya siasa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii pia kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Zubeir Ali Maulid Spika wa Baraza letu. Lakini nikupongeze na wewe Naibu Spika niwapongeze Wenyeviti wetu wote wawili na naamini kabisa kwa uwezo mlionao, uzoefu mlionao mtaliongoza Baraza letu hili kwa umakini mkubwa. Nawapongeza sana.

Vile vile nichukue nafasi hii kuwapongeza Wajumbe saba ambao Mhe. Rais amewateua kuungana nasi katika Baraza hili. Naamini kabisa sifa na uwezo walionao wajumbe hao ndio iliyompelekea Mhe. Rais kuwateua kuwa Wajumbe wa Baraza hili. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kuwapongeza sana wananchi wa Jimbo la Donge kwa kunichagua kwa kura nyingi, kura za kishindo, na kwa kweli niahidi kwao kwamba nitawapa utumishi uliotukuka katika jimbo lile.

Mhe. Naibu Spika, nianze kuzungumzia suala la hotuba ya Rais, na kweli nitazungumza katika maeneo sio mengi, maeneo machache.

Kwanza niseme kwamba tumevutika sana na hotuba ile na hasa kwenye eneo ambalo Mhe. Rais ameligusia kwamba kutakuwepo na vipaumbele katika kipindi cha miaka mitano tunayokwenda nayo. Vipaumbele hivyo vitajikita zaidi kwenye ilani ya CCM ya mwaka 2015-2020, lakini pia naamini vipaumbele hivyo vitajikita kwenye dira ya Zanzibar, Dira ya Maendeleo pamoja na MKUZA. Sasa kwenye maeneo yote hayo Mhe. Naibu Spika, ni lazima na hapa nashauri kwa sekta zote kuhakikisha kwamba hotuba hii na mikakati iliyoelezwa na Mhe. Rais inazingatiwa kikamilifu katika mipango ya kisekta.

Zile *sectoral plans* ni lazima zizingatie vipaumbele ambavyo Mhe. Rais ametuwekea kama dira ili tuweze kusonga mbele. Na hilo nalisema hivyo kwa sababu hivi karibuni tutakuwa na *session* ya bajeti, na bila shaka Waheshimiwa Wajumbe tutahitaji kuona kwa kiasi gani hotuba hii, na kwa kiasi gani vipaumbele vya serikali vimezingatiwa katika bajeti za kisekta.

Hilo ni jambo muhimu sana, maana yake bila ya kuhakikisha kwamba vitu hivyo vimezingatiwa kwenye bajeti inayokuja na kwenye mipango ya kisekta itakuwa hotuba hii hatukuitendea haki hata kama tutasema kwa kiasi gani.

Ni muhimu kuhakikisha kwamba kila kilichozungumzwa kinawekewa utaratibu wa utekelezaji, na kwa kuanzia tunaanzia mwaka huu wa 2016. Miaka mitano sio mingi, tusipoanza 2016 basi huko mbele tunaweza tukachelewa kwa sababu pia hatuelewi matokeo ya mbele, tunaona hapa katika kutekeleza haya aliyoyazungumza Mhe. Rais lakini na vipaumbele ambavyo tunavyo katika taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, la pili ambalo nilitaka nilizungumze mbali ya kuwa na vipaumbele na kuhakikisha kwamba tayari vimewekwa kwenye *sectoral plans* na bajeti, lakini la msingi kabisa ambalo naomba hili Waheshimiwa Wajumbe tukubaliane kama ni ushauri wangu ninautoa na pia nautoa ushauri huu kwa sekta kuhakikisha tunaimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini.

Tunaweza tukawa na mipango mizuri, lakini kama hatuna utaratibu wa kufuatilia utekelezaji wa mipango hiyo na kuitathmini, inawezekana ikawa hatuelewi tunaelekea wapi. Na katika mifumo hiyo ambayo naamini ipo inahitaji kuimarishwa, tuna ulazima wa kuwa na shabaha; ziwe *clear*, ziwe wazi na watu wote tuwe tunazielewa kwamba kwenye vipaumbele hivi malengo yetu, *targets* zetu ni hizi. Lakini vile vile tuwe na utaratibu wa pengine kila mwaka kujitathmini, na katika kujitathmini ambayo hiyo tunaita *sectoral review* itatuelezea kwa kiasi gani tumeweza katika mwaka mmoja kabla ya kuingia mwaka mwengine. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, lakini ili hilo liweze kufanyika vizuri, mifumo yetu ya ukusanyaji wa takwimu na kuzitumia takwimu hizo ni lazima ipewe kipaumbele, huwezi kujitathmini kama huna takwimu sahihi, wakati mwengine unaweza kusema kwamba unaendelea kwa kutumia takwimu ambazo pengine si sahihi ikawa unajivuruga wewe mwenyewe.

Kwa hiyo ni muhimu sana tuweke utaratibu mzuri wa kuasisika na hii ni *investment*, takwimu ni *investment*, tuwekeze katika kukusanya takwimu sahihi lakini vile vile tuwekeze katika kuzitumia takwimu hizo ili kuwa na tathmini nzuri na ufuatiliaji mzuri wa utekelezaji wa mipango.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala jengine ambalo nataka kulizungumza na ambalo limo kwenye maelezo ya Mhe. Rais katika hotuba yake, suala la ukuaji wa uchumi. Mheshimiwa kwanza hapa niipongeze serikali yetu kwa kuwa na kazi nzuri ya ukuaji uchumi.

Tumeelezwa hapa kwamba katika mwaka 2015 uchumi wetu umekua kwa wastani wa asilimia 6.6, lakini malengo kwa miaka mitano ijayo kwa mujibu wa hotuba ya Mhe. Rais ni kwamba tuwe na ukuaji wa wastani wa asilimia 8 mpaka 10. Hayo ndio malengo, lakini malengo haya hayawezi kufikiwa kama kwanza hatuna nia ya dhati, ni lazima sote tukubaliane tuwe na nia ya dhati na tukubaliane kubadilisha mtizamo wetu, *(change of mindset),* na hii inaanzia kwa viongozi tukiwemo sisi Wajumbe wa Baraza hili, lakini vile vile *change of mindset* kwa wananchi wetu nalo hilo linahitajika.

Kwa sababu kwenye suala la maendeleo ni suala ambalo linahitaji kuwashirikisha watu wote, makundi yote na katika ngazi zote, lazima tujenge uelewa pamoja na sote tukubaliane kwa dhati kwamba sasa tunaelekea katika kuimarisha nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hilo nilikuwa nataka kuongezea kitu kwenye hilo la ukuaji uchumi. Ni muhimu sana vipaumbele ambavyo tunataka kuviweka vikaainishwa na vikawekwa bayana, lakini hivyo navyo lazima vioane na uwekaji wa *resources* zetu tulizonazo. Unaweza ukawa na vipaumbele lakini haviwi-*reflected* sawa sawa na bajeti ya serikali. Kwa hivyo, vile vipaumbele ni lazima tuhakikishe na bajeti inayowekwa inalingana na umuhimu ambao kipaumbele kile kimepewa.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ni mapato, bila ya kuwa na ukusanyaji mzuri wa mapato, mipango yetu yote tutakayoiweka itafifia utekelezaji wake kwa kukosa *resources*. Niipongeze serikali kwa kuwa na mipango madhubuti kabisa ya kuimarisha mapato katika nchi yetu.

Tumeelezwa kwa mwaka 2014/2015 kupitia *TRA* na *ZRB* tuliweza kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 362.8 bilioni. Ni kiwango kizuri, kiwango kikubwa ukilinganisha na kile ambacho kilifanywa mwaka 2010/2011 cha shilingi 181.4 bilioni. Pamoja na kwamba tumekusanya vizuri na kuna ongezeko kubwa lakini kwa malengo tuliyojiwekea ya ukuaji wa uchumi kwa wastani wa asilimia 8 mpaka 10 tunahitaji kuongeza mapato haya kwa wingi zaidi. Kwa hiyo, juhudi kubwa zaidi inahitajika katika ukusanyaji na kwenye hilo tunahitaji kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato, ile *starting base* yetu lazima ipanuke.

La pili, kuhakikisha kuwa na mipango madhubuti ya yale mapato yanayokusanywa nayo yasivuje, kusiwe na uvujaji wa mapato hayo, lakini ili tuweze kufikia malengo yale ni muhimu sana kwamba lazima tuwe na mpango madhubuti wa kusimamia matumizi ya fedha zinazokusanywa. Kwenye eneo hilo mkazo zaidi ni katika ununuzi wa vifaa lakini pia na udhibiti wa mali za serikali, hapo panahitaji kuwekewa mkazo zaidi ili kuhakikisha yale mapato yanayokusanywa basi yanatumika vile yanavyostahiki.

Mhe. Naibu Spika, sina hakika kwa hili, lakini nadhani ukusanyaji wa mapato yetu uko kwenye wastani wa asilimia 18 mpaka 20 ya pato la Taifa. Hili tunahitaji kuliongeza angalau basi tuwe na wastani wa asilimia 23 mpaka 25 ya pato la taifa.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo ningependa kulichangia ni mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi (*PPP*). Hapa niipongeze sana Serikali kwa kuja na sheria mpya ya *PPP*, sheria namba 8 ya mwaka 2015. Sheria tunayo na kwenye hili napongeza sana mpango wa serikali wa kuwa na miradi kumi ya *PPP* ambayo hiyo itatekelezwa baada ya kufanyiwa upembuzi yakinifu. Lakini kwenye hili Mheshimiwa nilikuwa naomba serikali iwe na mipango madhubuti ya kuhakikisha sekta binafsi ya ndani inashiriki kikamilifu katika miradi hii ya *PPP*, na kwenye hilo kunahitajika kwanza kushajihishwa sekta binafsi ya ndani, naamini kabisa wapo wafanyabiashara wakubwa wenye uwezo mkubwa na wao wanahitajika sasa kushajihika kushiriki katika utunzaji wa miradi hii ya *PPP*.

Pia kuna haja na kama inavyoelezwa katika MKUZA ya kuimarisha sekta binafsi, lazima tuisaidie tuwe na mikakati madhubuti ya kuisaidia sekta binafsi ambayo kwa ndani iko changa bado, ili nayo kukua na kuweza kutoa ushirikiano mkubwa katika uendeshaji na usimamiaji wa miradi ya *PPP*.

Mhe. Naibu Spika, katika suala la uimarishaji wa miji kwa kuzingatia mkakati wa matumizi ya ardhi ambalo Mhe. Rais nalo hili alilizungumza na alizungumza kwamba tayari kuna miji 14 ambayo tayari imeshapangwa.

Kwenye hili Mheshimiwa ningeomba serikali ikawa na mpango wa kuwajengea uelewa wadau wakuu wote, na nikisema wadau wakuu wote wakiwemo Wajumbe wa Baraza hili. Ni muhimu sisi Wajumbe tukajua miradi hiyo tukapata semina ikiwezekana ya kueleweshwa na hata kufanya ziara ya kuiona miradi hiyo ili kujua kwa uhakika miradi hiyo inaendeleaje na mipango ikoje katika utekelezaji wake.

Vile vile lakini wananchi wetu nao wanahitaji kujengewa uelewa ili waweze kujua katika miradi hii inayowekezwa na serikali kupitia programu ya *PPP* inaendaje na miradi hiyo ni ya aina gani, inaelekea kwamba miradi ipo, programu nyingi zipo, lakini wananchi uelewa wao mdogo katika programu hizi.

Chengine ambacho ningependa nikizungumze hapa katika masuala hasa haya ya uwekezaji ukiacha hii *PPP* ni utaratibu wa ku-*maintain* hii miradi au *public investment* ambazo zinafanywa. Sasa hivi nipongeze sana juhudi ya serikali inayofanyika katika kuweka taa za barabarani naona kabisa kwamba kuanzia Amani kuendea Mwanakwerekwe sasa hivi hali imebadilika mandhari ya usiku ni nzuri na inapendeza sana.

Miradi ile naamini itaendelea katika maeneo mbali mbali ya mji wetu, lakini ni vizuri sana tukawa na mipango ya kusimamia miradi ile baada ya kumalizika kuwepo. Kwa sababu sasa hivi utakuta katika maeneo ya Michenzani taa ambazo zimewekwa hivi karibuni zinazotumia *solar* nyingi zao haziwaki. Sasa huku tunaendelea kuweka taa nyengine lakini huku taa zile ambazo zimewekwa katika kipindi kifupi tu tayari haziwaki. Kwa hivyo, ningeomba hasa sekta zinazohusika kuwa na utaratibu mzuri wa kusimamia miradi, na *investment* ambazo zinawekwa na serikali hasa katika *maintenance* ya miradi hiyo.

Sasa hivi pia kuna uwekezaji mkubwa wa miradi ya misingi ya maji machafu nayo pia inahitaji uangalizi baada ya kumalizika miradi ile ili tatizo ambalo tunalo hivi sasa lisiweze kutokea huko mbele tunakokwenda.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala la matumizi ya ardhi, suala hili linazungumzwa na mara nyingi sana limekuwa likizungumzwa tokea mimi sijaingia katika Baraza hili, linazungumzwa suala la migogoro ya ardhi na katika maeneo mbali mbali bado tatizo hili linaendelea.

Mhe. Naibu Spika, ningeomba serikali ikaendelea na lile zoezi ambalo limeanzishwa la usajili wa ardhi, tukiweza kusajili ardhi yetu na watu kupatiwa hati zao tatizo hili kwa kiasi kikubwa litaweza kuondoka. Lakini kwenye usajili huu ni lazima kuwe na uadilifu mkubwa, kwa sababu mingi ya migogoro hii inasababishwa na sisi viongozi katika ngazi mbali mbali. Wananchi wanaweza wakawa ni sehemu ya tatizo lakini kwa kiasi kikubwa tatizo hili linasababishwa na viongozi na sisi kama viongozi lazima tutoe ushirikiano mkubwa sana katika ngazi zote kuhakikisha tatizo hili haliendelei, tunalikomesha kabisa na wananchi wanapata fursa ya kuitumia ardhi kwa masuala ya uzalishaji na uwekezaji.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa kuna matatizo katika baadhi ya maeneo, na mimi nina ushahidi wa kwamba hata zile ardhi zilizotolewa eka tatu tatu zilizotolewa na Mhe. Rais wa Kwanza wa Zanzibar tayari nyengine ziko kwenye migogoro. Watu wanakuja wanazidai ardhi zile zile kwamba ni mali yao wakati hawa watu tayari wana hati walizopewa mwaka 1964 kwa ajili ya kuziendeleza kwa kilimo na kuendesha maisha yao. Hilo ni tatizo, ushahidi ninao, ni imani yangu kwamba viongozi watalisimamia suala hili kwa uadilifu kabisa katika ngazi zote, lakini napongeza sana hotuba ya Mhe. Rais aliposema kwamba, tutaimarisha Mahakama za Mikoa, nadhani hili ni suala muhimu sana na linahitaji kufanyiwa kazi kwa haraka sana, kwa sababu matatizo mengi yako huko katika wilaya na mikoa yetu.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala la utumishi na kwenye utumishi mimi ningependa niseme tu kwamba, kunahitajika uwajibikaji, na uwajibikaji wa kweli katika utendaji, wale watakaopata nafasi ya kumsaidia Mhe. Rais katika ngazi

za uwaziri, unaibu waziri lazima wasimamie suala hili lakini ni muhimu sana katika utumishi wa umma kujenga nidhamu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe muda wako umebakia dakika mbili.

Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed: Ahsante Mheshimiwa. Nidhamu ni kitu muhimu sana, bila ya kuwa na nidhamu na kuheshimu sheria, taratibu, kanuni zilizopo Mhe. Naibu Spika haya yote tunayoyapanga hayawezi kufikiwa, lakini nilitaka kusema la mwisho kabisa ni suala la ajira.

Kwenye makundi maalum yamezungumzwa na yote nayakubali kama yalivyozungumzwa na Mhe. Rais, lakini suala la vijana ambalo linawaingiza vijana wanawake na wanaume hili ni suala muhimu sana, na suala hili hatutakiwi kabisa kulifanyia mzaha. Kwa sababu ninavyoamini mimi vijana ndio nguvu kazi ya Taifa hili, lakini vijana ndio amani ya nchi hii, bila ya vijana hakutakuwa na amani katika nchi hii; vijana hawa hawa ndio siasa katika nchi hii, na ndio viongozi wa leo na viongozi wa kesho, ni lazima matatizo yao na hasa tatizo la ajira linahitaji kufanyiwa kazi kwa juhudi kubwa.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hotuba ya Mhe. Rais kwa asilimia mia moja, nakushukuru sana.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kunipatia fursa hii ya mwisho kabisa. Pia nichukue fursa hii nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha leo hii kutukutanisha hapa tukiwa katika hali ya uzima na furaha na amani katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenirejesha tena ndani ya Baraza hili la Wawakilishi kwa mara ya pili. Vile vile nichukue nafasi hii niipongeze hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar ambayo imewasilishwa jana ndani ya Baraza letu hili tukufu katika uzinduzi wa kulizindua Baraza hili la Tisa la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii niwashukuru vijana wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa imani yao waliyonionesha kwangu na kuweza kunirejesha ndani ya Baraza hili Tukufu. Pia nichukue nafasi hii niwapongeze UWT Taifa wale wote walionipigia kura na kuweza kurudi tena humu ndani ya Baraza.

Mhe. Naibu Spika, shukurani za pekee ziende kwa wazazi wangu wapenzi mama na baba kwa dua zao ambazo walikuwa wananiombea kila siku wakati wa kipindi cha swala. Vile vile nichukue fursa hii nimshukuru mume wangu mpenzi Ali Seif kwa kunivumilia kipindi chote nilichokuwa katika kampeni zangu ili kuhakikisha Chama cha Mapinduzi kinashinda kwa ushindi mkubwa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, pia nichukue fursa hii nimshukuru mama yangu Mhe. Bihindi Hamad Khamis kwa mawaidha yake aliyokuwa ananipa siku hadi siku na kuniliwaza.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nianze kwa kuchangia hotuba hii ya Mhe. Rais wa Zanzibar. Hotuba hii ndio dira ya mwelekeo wa kipindi cha miaka mitano, nimpongeze Mhe. Rais katika hotuba yake alisema kwamba vijana, wanawake, wazee na watoto wamepewa kipaumbele katika hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, vijana ndio muhimili wa Taifa hili, vijana ndio watunza amani wa nchi hii. Sisi vijana tuna changamoto nyingi ambazo zimetukabili, vijana wengi sasa hivi Zanzibar wamekuwa ni wasomi, lakini wana malalamiko mengi baada ya kumaliza masomo yao huwa wanasumbuka mitaani kwa tatizo la ajira.

Tatizo la ajira sio Zanzibar tu, limeenea dunia nzima lakini kutokana na kitabu hiki cha Mhe. Rais na miradi ambayo ameibainisha katika kitabu hiki kuna mradi wa *PPP* ambao utaweza kuleta ongezeko la ajira kwa vijana. Nimshukuru sana Mhe. Rais.

Mhe. Naibu Spika, pia nimshukuru sana Mhe. Rais kwa kuwaona wazee, wazee wameitumikia sana nchi hii. Mhe. Rais aliahidi Mhe. Waziri wa Fedha aliyepita aliahidi katika Bajeti yake ya Serikali kuwa wazee ambao wamefikia miaka 70 watakuwa wanapatiwa posho. Hii ni dhamira nzuri ya serikali yetu na inaonesha dhahiri kuwa wanawajali wazee.

Mhe. Naibu Spika, kuna masikitiko makubwa sana wananchi wa Zanzibar takriban ni miaka mitano wanasumbuka na usumbufu wa kituo cha daladala. Kituo hiki kimechukua miaka mitano tangu niingie kwenye hili Baraza mwaka 2010 hili tatizo lilikuwa tayari limeshaanza.

Mhe. Naibu Spika, niipongeze serikali kwa kuonesha kuwajali wananchi wa Zanzibar. Kwenye kitabu hiki mna mradi wa *PPP* ambao utajenga kituo cha daladala Zanzibar hapa Unguja. Mhe. Naibu Spika, wananchi wote ni sawa wanahitaji kuenziwa.

Mhe. Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha mtu anatoka Bandarini analibeba polo lake au begi mpaka Kisiwandui muda mwengine mpaka Michenzani unakuja kutafuta usafiri. Niiombe serikali katika bajeti yake hii ya mwaka 2016/17 iweke kipaumbele katika ujenzi wa kituo cha daladala.

Mhe. Naibu Spika, niipongeze serikali kwa kuona umuhimu wa zao la karafuu. Zao la karafuu limepewa kipaumbele na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kutaka kuwakomboa wakulima wa zao hilo. Niwaombe wakulima siku za kipindi cha zao la karafuu kuna wakulima ambao wanaenda kuuza karafuu wengine wana magunia mpaka ishirini ya karafuu.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa una dakika tatu za kumalizia.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Wakulima hawa huwa wanashauriwa pesa zao wafungue *account* ili ziingizwe moja kwa moja benki kwa usalama zaidi lakini hawa wakulima huwa wanakataa. Niwaombe wakulima waweze kuisikia serikali yao iliyo makini kwa kutaka kuwaletea maendeleo ambayo ipo tayari kuimarisha zao hili la karafuu, wawe wasikivu, waweze kuchukua pesa zao benki moja kwa moja. Na niipongeze serikali kwa kuwakopesha wakulima wa zao la karafuu pesa, ambapokuwa watashindwa kidogo na pesa za kuanikia karafuu, majamvi na vifaa vyengine.

Mhe. Naibu Spika, mwisho niipongeze serikali katika kujenga vituo vya afya. Afya ni muhimu kwa binadamu, lakini cha kusikitisha sisi wananchi wakati wa kipindi cha kampeni huwa tunabadilika. Nina kituo changu cha afya Kiuyu Minungwini wakati wa kampeni kituo kile kiliunguzwa moto na wananchi ambao hawajulikani. Niwaombe wananchi waangalie maendeleo zaidi waache jazba zao katika kuharibu maendeleo ambayo serikali ipo tayari kuwasaidia.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa niipongeze...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa malizia muda umekwisha.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa kwa niaba ya vijana wa Mkoa wa Kaskazini Pemba tunaipongeza hotuba ya Mhe. Rais na naunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe bado kuna wachangiaji wengi wameleta maombi yao ya kuchangia na tunatarajia kwa wale walioleta maombi lakini hawajapata fursa basi tukijaaliwa Ijumaa wataweza kuendelea kuchangia.

Kwanza nishukuru sana kwa michango mbali mbali ambayo imetolewa hapa, na michango hii kwa kweli mingi sana ni *very constructive*, inajenga, na zaidi ni kwamba wengi wamezungumzia masuala ambayo yanawaathiri moja kwa moja katika maeneo yao.

Hivyo basi, ningeomba sana, kwa sababu bado hatuna mawaziri lakini ningeomba Utawala wa Baraza watengeneze kitabu cha *hansard* maalum kwa ajili hasa ya mawaziri wetu watakaoteuliwa ili wapate muda wa ku-*refer* yale maeneo makubwa ambayo yamezungumzwa katika hotuba ya Rais. (*Makofi*)

Waheshimiwa kabla ya kuahirisha kikao kuna matangazo mawili, tangazo la kwanza ni kwamba, Waheshimiwa wafuatao wanaombwa wafike katika Divisheni ya Utumishi sehemu ya mikopo ya Baraza la Wawakilishi. Waheshimiwa hao ni:-

Mhe. Hamad Abdalla Rashid
Mhe. Ali Suleiman Ali
Mhe. Suleiman Makame Ali
Mhe. Rashid Ali Juma
Mhe. Mussa Ali Mussa
Mhe. Abdalla Maulid Diwani
Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
Mhe. Ali Khamis Bakar
Mhe. Masoud Abrahman Masoud
Mhe. Yussuf Hassan Iddi, na
Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Tangazo jengine ni kuhusu siku ya Mashujaa.

Waheshimiwa Wajumbe wote tunaarifiwa kuhudhuria katika hitma ya kuwaombea dua viongozi wetu waliokwisha kutangulia mbele ya haki siku ya Mashujaa. Shughuli hiyo itafanyika kesho mnamo saa 2:00 asubuhi huko Afisi Kuu ya CCM Zanzibar Kisiwandui, shime Waheshimiwa Wajumbe wote tuhudhurie kwa wingi katika kisomo hicho.

Tangazo la mwisho ni la upigaji picha. Waheshimiwa Wajumbe ambao wameapishwa hii leo na wengine ambao bado hawajapiga picha kwa ajili ya vitambulisho hivi tunavyotakiwa kuvivaa wanaombwa kupiga picha hizo kesho kutwa Ijumaa kuanzia saa 3:00 asubuhi. Picha hizo zitapigwa katika chumba cha kusomea huko juu.

Waheshimiwa Wajumbe kufikia hapa tuahirishe kikao chetu hadi siku ya Ijumaa tarehe 08/04/2016.

(Saa 1:45 kikao kiliahirishwa hadi siku ya Ijumaa
tarehe 08/04/2016 Saa 3:00 asubuhi)